

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA NNE - TAREHE 11 JULAI, 2005

(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika, (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa mwaka wa Fedha 2005/2006

MHE. MBARUK K. MWANDORO (K. n. y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):

Maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

MHE. ADELASTELA E. MKILINDI (k. n. y. MSEMADI WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA):

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa Mwaka uliopita pamoja na Maoni yake kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 225

Tatizo la Usafiri kwa Watendaji wa Kata Vijijini na Madiwani

MHE. OMAR S. CHUBI (k.n.y. MHESHIMIWA PROF. SIMON M. MBILINYI) aliuliza:-

Kwa kuwa, lipo tatizo kubwa la usafiri kwa Watendaji wa Kata Vijijini na hata Madiwani ambalo limekuwa kero kubwa katika utendaji wa majukumu yao na kwamba gari ya Mbunge katika maeneo hayo ndiyo inayotegemewa sana hasa katika kubebia wagonjwa na kumfanya Mbunge kuonekana kuwa mhisani mkuu; na kwa kuwa Pato la Taifa limevuka shilingi Trilioni 3:-

(a) Je, hivi Serikali haiwezi kufanya utaratibu wa kuwapatia mikopo ya vyombo vya usafiri kama vile gari dogo za Suzuki, pikipiki au Baiskeli kwa wale wa Vijijini?

(b) Je, kama Serikali ikipunguza matumizi kwenye *centre hatuwezi* kuwapatia vyombo hivyo au kama ikishindikana Serikali haiwezi kuanzisha *Transport Pool* kwenye ngazi ya Wilaya kwa kuanzia na magari matatu au hata matano ili yaweze kusaidia viongozi hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi, Mbunge wa Jimbo la Peramiko, lenye Sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la usafiri linalowakabili Watendaji wa Vijiji. Hata hivyo utaratibu wa kuwakopesha Waheshimiwa Watendaji Kata na Vijiji haujaandalisha na Serikali. Halmashauri zinaweza kuandaa mpango wa kuwakopesha vyombo vya usafiri Watendaji wake na kurejesha mikopo hiyo kwa kuwakata katika mishahara yao. Mikopo kwa Waheshimiwa Madiwani itakuwa ni jambo gumu kutekelezwa kwa sasa kutokana na Madiwani kutolipwa mishahara kama Watumishi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gari la Mheshimiwa Mbunge kutumiwa kubeba wagonjwa, napenda kwanza kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutimiza wajibu wake kwa wananchi wa Jimbo lake kwa kutoa gari lake kusaidia wagonjwa wenye shida ya usafiri. Mungu akujalie uendelee na moyo huo.

Serikali inao mpango wa kununua magari ya kubeba wagonjwa kwenye hospitali na vituo vya afya kwa awamu kadri Bajeti itakavyoruhusu. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 Serikali imetenga kiasi cha Shilingi Bilioni 1.5 kwa ajili ya kununua magari ya kubebia wagonjwa kama njia ya kuboresha huduma za afya katika Halmashauri. (*Makofit*)

(b) Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali haina mpango wa kuanzisha *Transport Pool* kwa ngazi ya Wilaya. Napenda tu kuzishauri Halamashauri kufanya hivyo wao kwa kuiga mfano wa Mradi wa *District Rural Development Programme (DRDP)* uliofadhiwa na Serikali ya Uhlanzi. Mradi huu umeonyesha mafanikio makubwa sana katika

Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu na hivyo natoa wito kwa Halmashauri nyingine kutembelea hapo na kujifunza ili waweze kufanya hivyo.

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuuliza swalii la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inakubali kwamba gari la Mbunge linatumia kama *Ambulance* au gari ya wagonjwa, Je, unaweza ukafanywa utaratibu angalau wa kupata fedha za matengenezo kwa gari linalotumika kama *Ambulance*?

NAIBU WAZIRI , OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya si eneo linalohusiana na TAMISEMI moja kwa moja lakini nadhani Waziri anayehusika amesikia kama hilo kweli linawezekana nadhani yeche na nafasi nzuri ya kulitolea maelezo.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja la nyongeza. Kwa kuwa miaka yote tumekuwa tunaomba Madiwani wasaidiwe, na kwa kuwa sasa hivi Mabilioni ya pesa yanakwenda Vijijini na wao ndiyo wasimamizi. Je, ni lini Serikali itakubali au kuwaingiza Madiwani nao waanze kupata mshahara badala ya posho? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, tatizo la Madiwani ni tatizo la Kitaifa kwamba linatuhusu sisi wote na kama ambavyo tumekuwa tukieleza muda wote, dhamira ya Serikali ni nzuri isipokuwa kwa hali na mazingira yaliyopo hivi sasa ya kisheria na vile vile kiutaratibu jambo hili limekuwa muda wote linakwama na ndiyo maana mara ya mwisho nimesema Serikali hatimaye imekubali kuunda Kamati na imeishaanza kulifanyia kazi jambo hili na mimi naamini kabisa baada ya Kamati hiyo inayosimamiwa na Mheshimiwa George M. Lubeleje kumaliza kazi yake tunaweza tukapata matokeo mazuri. (*Makofî*)

Na. 226

Uboreshaji wa Maslahi – Makatibu Tarafa

MHE. IBRAHIMU W. MARWA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imeamua kupeleka madaraka Mikoani na kuwashirikisha wananchi kuitia katika Halmashauri zao; na kwa kuwa Madiwani ni Wasimamizi Wakuu wa shughuli za maendeleo kwenye Kata na vile vile wao ni nguzo kuu ya kusaidia Wabunge kutekeleza majukumu yao; na kwa kuwa suala la maslahi ya Madiwani ambayo ni duni limejadiliwa kwa muda mrefu kuitia *ALAT* na katika Bunge; na kwa kuwa Bajeti kubwa inaelekezwa katika Halmashauri zetu ambako mafanikio makubwa yamepatikana katika nyanja za Elimu (MMES, MMEM) barabara na huduma mbali mbali za jamii:-

- (a) Je, Serikali inachukua hatua gani ili ikiwezekana wakati wa Bajeti ya mwaka 2005/2006 kuboresha Maslahi ya Makatibu Tarafa na Madiwani pamoja na posho za vikao na viinua mgongo?
- (b) Serikali baada ya kufanya mabadiliko mbali mbali ya viwango kwa Watumishi wa Serikali. Je, kwa nini mabadiliko hayo yasifanyike pia kwa Madiwani?
- (c) Je, Serikali inakubali kuwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya Elimu hususan MMEM, yametokana na Usimamizi mzuri wa Madiwani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI
ZA MITAA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ibrahim W. Marwa, Mbunge wa Musoma Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema wakati nakijibu swalii namba 206 la Mheshimiwa John L. Mwakipesile tarehe 6/07/2005, Serikali imeishachukua hatua za kuhakikisha kuwa mafao ya Waheshimiwa Madiwani yanaboreshwili posho za vikao na viinua mgongo vilingane na uzito na umuhimu wa majukumu yao. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuteua Mtaalam Mshauri (*Consultant*) ambaye amepitia na kukusanya maoni, ushauri na mapendekezo kuhusu aina ya maslahi yanayopaswa kulipwa yamekwishaanza kushughulikiwa. Mtaalam Mshauri huyo anafanya kazi hiyo chini ya Usimamizi wa Kamati ambayo inaongozwa na Mheshimiwa George M. Lubeleje kama nilivyokwisha kusema.

Mtaalam Mshauri amekwishakusanya maoni karibu kwa Halmashauri nyingi pamoja na wadau wengine mbali mbali na tuko katika hatua za mwisho kuweza kuyaweka pamoja kwa lengo la kufanya maamuzi katika ngazi ya Serikali.

Kwa upande wa maslahi ya Makatibu Tarafa, maslahi yao yataboreshwaka kama yanavyoboreshwa kwa Watumishi wa Umma kwa kuwa Makatibu Tarafa ni Watumishi wa Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, viwango vya posho zinazotolewa kwa Watumishi wa Serikali haviwezi kutumika kuwalipa Madiwani kwa sababu Madiwani siyo Watumishi wa Serikali na kwamba makundi hayo mawili yaani Madiwani na Watumishi wa Serikali yana majukumu na masharti tofauti.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana kabisa na maoni ya Mheshimiwa Mbunge kuwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika sekta ya Afya, Elimu na nyinginezo na hasa MMEM, yametokana kwa kiasi kikubwa na usimamizi mzuri wa Madiwani kwa kupitia Kamati za maendeleo za Kata na Mabaraza ya Halmashauri.

MHE. WILLIAM H. SHELUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hiyo. Kwa kuwa, Serikali imebadilisha majina ya Makatibu Tarafa na kuwaita sasa Maafisa Tarafa. Je, si vyema wakakamilisha huo mtiririko wa Utawala ili wale wa Kata nao wakaitwa Maafisa Kata na wale wa Vijiji wakaitwa Maafisa Vijiji? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, Katibu Tarafa bado ni Mtumishi wa Serikali, kilichofanyika ni Serikali kukubali kumtengenezea kiungo kati yake na Serikali za Mitaa lakini kimsingi amebaki ni Mtumishi wa Serikali. Watendaji wengine hawa wa Kata na Vijiji ndiyo ni Watumishi wa Serikali kwa maana ya Serikali za Mitaa.

Serikali inachofanya ni kuongeza ruzuku kwa ajili ya mishahara yao. Lakini kwa maana ya jina na pengine kuleta mtiririko mzuri, nadhani ni ushauri mzuri tutajaribu kuutazama tuone kama hilo linaweza kufanyika bila kuathiri jambo lingine lolote. (*Makofî*)

MHE. JAMES P. MUSALIKA: Mheshimiwa Spika, nafurahi kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imesema na naipongeza kwamba kuna Tume inayoshughulikia masuala ya posho na maslahi ya Madiwani, lakini kwa kuwa ziko Tume huwa zinafanya kazi muda mrefu miaka miwili mitatu, minne bila kumaliza kazi.

Je, Tume hii iko tayari kumaliza kazi mwezi wa kumi ili mwezi wa kumi na moja Madiwani wapya waanze na viwango hivyo vya posho? (*Makofî*)

SPIKA: Mheshimiwa Lubeleje amesikia. (*Kicheko*)

(*Hapa Mheshimiwa George M. Lubeleje Alisimama*)

SPIKA: Hapana hapana, Mheshimiwa Naibu Waziri. (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kama ulivyosema ninahakika Mheshimiwa Lubeleje amesikia, lakini naomba nirudie tu kauli yangu ya juzi kwamba Kamati hiyo itakutana tarehe 13 mwezi huu kutazama hayo ambayo Mtaalam amekwisha yakusanya. Kwa hiyo nataka nikuhakikishie naamini kabisa zoezi litakwisha kabla ya Bunge hili. Lakini kama wataweza kweli kulipwa hayo yatakayokuwa yamependekezwa ndani ya kipindi hiki, hilo siwezi nikasema kwa sababu lazima lipite katika mikondo mingine ambayo kwa dhamira ya Serikali ninavyoijua pengine tunaweza tukafanikiwa.

Na. 227

Mikopo kwa Watumishi wa Serikali

MHE. KHALID S. SURU aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Serikali imeisharuhusu Watumishi mbali mbali wa Serikali kuchukua mikopo kwenye Benki mbali mbali hapa nchini, hususan *NMB* na kadhalika; na kwa kuwa dhamana yao ni mishahara yao kupitia kwa waajiri wao:-

- (a) Je, ni lini Watumishi wa Serikali hasa Walimu wa Wilaya ya Kondoa wataanza kupata mikopo hiyo?
- (b) Je, Serikali imetenga kiasi gani cha fedha kupitia *NMB* kwa ajili ya kuwakopesha Watumishi hao?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Khalid S. Suru, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, *National Microfinance Bank* Makao Makuu Dar es salaam imetoa kibali kwa Maafisa Tawala na Makatibu Tawala wa Mikoa yote Tanzania Bara kwa maana ya *RAS* na hao ma-*RAO* kuingia mkataba na *NMB* ili kuwezesha wafanyakazi wa Ofisi zao kufaidika na mpango wa mikopo.

Uongozi wa *NMB* Makao Makuu kwa kushirikiana na Ofisi za Kanda wamefanya ziara rasmi za kukutana na kubadilishana mawazo na Wateja au Watumishi. Mambo yaliyozungumzwa ni pamoja na kutangaza na kuelimisha Watumishi juu ya mikopo inayotolewa na *NMB*. Uongozi wa Kanda ya Magharibi na Tawi la *NMB* Kondoa umefanya ziara kwenye Wilaya ya Kondoa. Baada ya ziara hiyo Walimu 275 na Watumishi wengine 447 wamejaza fomu za mikopo kutoka Benki ya *NMB*. Fomu hizi zipo katika hatua mbali mbali za kukamilishwa ikiwa ni pamoja na kupitishwa na Wakuu wa Idara na hatimaye Mkurugenzi wa Halmashauri ili hatimaye zipelekwe *NMB* kwa hatua zaidi za mikopo.

- (b) Mheshimiwa Spika, Serikali hajatenga fedha za kuwakopesha Watumishi ila imeruhusu Watumishi kukopa katika Benki kwa dhamana ya mishahara yao kupitia kwa waajiri wao. Napenda kuwaagiza kwa mara nyingine tena Waajiri wote katika Halmashauri zote za Wilaya kuwasilisha makato ya fedha za mikopo kwenye asasi za fedha mara moja baada ya mikopo kutolewa. Napenda pia kuwaelekeza Waajiri hawa kutumia fursa hii kukopa fedha kwenye Taasisi za fedha ili kuboresha maisha ya Watumishi ili kupambana na umaskini.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kupata nafasi hii ya kuuliza swal la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri kabisa kutoka Serikalini, ningependa kuuliza swal la msingi. Kwa kuwa majibu yaliyotolewa yananufaisha zaidi Watumishi walioko Wilayani wanaolipwa mishahara na Serikali, lakini wale ambao wapo Wilayani wanalipwa mishahara na Halmashauri za Wilaya, ningependa nipate ufanuzi hawa nao utaratibu wao ukoje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, katika ngazi ya Wilaya tunayo makundi matatu ya Watumishi kwa maana ya Watumishi wa Serikali kuu ambao wako chini ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Watumishi ambao wameajiriwa na Halmashauri za Wilaya na wanlipwa mishahara na Halmashauri yenyewe. Lakini tunao Watumishi ambao wameajiriwa na Halmashauri lakini wanlipwa fedha na Serikali Kuu kwa njia ya ruzuku. Wote hawa makundi yote matatu wanayostahili kabisa ya kukopa fedha kutoka *NMB*. Kwa hiyo, nadhani kama nilivyosema kwa sababu Makatibu Tawala wote wameishaarifiwa, Wakurugenzi wote wanalijua, nadhani ni kuwatia moyo tu Watumishi hawa wapate nafasi ya kutumia mwanya ambao sasa umepatikana.

Na. 228

Kuhusu Mzunguko wa Fedha

MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. LEONARD M. SHANGO) aliuliza:-

Kwa kuwa kiwango cha mzunguko wa fedha ni kigezo muhimu katika kupima ukuaji wa uchumi na utokomezaji wa umaskini kati ya jamii mbalimbali za taifa letu:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu kuendelea kupanua na kuimarisha mfumo wa kifedha kwenye uchumi katika eneo ya Vijijini?
- (b) Je, Serikali ina mipango gani kuwajibisha Taasisi za kibenki Vijijini pamoja na kufufua mipango ya huduma za *Mobile Banking Services Units* na kuzielekeza huduma hizo kwenye Vijiji vilivyopo mbali na barabara kuu, pembezoni na ambazo hazifikiwi kwa urahisi?
- (c) Je, kuna Vijiji vingapi katika Wilaya gani ambapo huduma ya kibenki ya *Mobile Banking Services* inaendelea kuwashudumia wananchi?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leonard M. Shango, Mbunge wa Iramba Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali inajitahidi kupanua na kuimarisha mfumo wa kifedha kwenye uchumi, kwa kuimarisha Miundo mbinu kama vile barabara, mawasiliano na usalama, zitakazovutia na kurahisisha upelekaji na upatikanaji wa huduma za kiuchumi na kijamii Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeweka mazingira mazuri yatakayorahisisha uanzishaji, upanuzi na uimarishaji wa mfumo wa kifedha kwenye uchumi kwa ujumla, kuanzia Mijini hadi Vijijini kama ifuatavyo:-

Kwanza, kiwango cha chini kabisa cha mtaji cha uanzishaji wa huduma za kibenki kijijini ni Shilingi milioni 50 ikilinganishwa na Shilingi milioni 500 zinazohitajika kuanzisha huduma hizo hizo kwa maeneo ya Mijini.

Pili, idadi ya chini kabisa ya wamiliki mtaji yaani *shareholders* ni watu hamsini na cha juu kabisa hakina mpaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba hadi sasa Benki kadhaa zimeisha funguliwa kukidhi mahitaji ya wakazi Vijijini, zikiwemo *Kilimanjaro Co-operative Bank, Kagera Farmers Cooperative Bank, Mbinga Community Bank, Mwanga Community Bank* na *Mufindi Community Bank*. Benki hizi zinasaidia sana kutoa huduma na zimekuwa chachu ya Maendeleo Vijijini katika sehemu husika. Aidha wananchi wengi sana Vijijini wameanzisha mifuko au vyombo vya kuweka na kukopa kidogo kidogo kulingana na sheria na taratibu zilizowekwa.

(b) Mheshimiwa Spika, shughuli za kibenki za *Mobile Services* hufanyika mahali ambapo Mabenki husika hutarajia kupata faida. Serikali haiwezi kuyalazimisha Mabenki kuendesha shughuli zao mahali ambapo hayatapata faida. Kama ilivyoelezwa katika majibu ya kifungu (a) uboreshaji wa Miundo mbinu zikiwemo barabara, mawasiliano, masoko, maduka na magulio katika hali nzuri ya usalama kutachochea shughuli za uchumi na fedha Vijijini. Ni mazingira hayo hayo ndiyo yanaweza kushawishi Mabenki kusambaza huduma za *Mobile Banking* Vijijini.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa sasa hivi hakuna huduma ya kibenki za *Mobile Banking Services* inayoendelea Mijini au vijijini hapa nchini. Hata hivyo baadhi ya Taasisi zetu za kifedha, tayari zimeishaonyesha nia ya kuanzisha huduma husika katika maeneo ya Vijijini na Mijini pia. Kwa sasa bado Taasisi hizi zinaendelea kufanya tathmini ya uanzishaji wa huduma hizo katika maeneo husika.

SPIKA: Samahani alichelewa kuamka aliyeuliza swali la msingi, sasa nampa nafasi kwanza halafu utafuata wewe.

MHE. MGANA I. MSINDAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema Benki zimeanzishwa Mwanza, Mufindi na ni maeneo yale ambayo yana mazao ya kudumu na Vyama vya Ushirika bado vinaendelea kwa nguvu. Je, Mikoa kame kama Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma wana mpango gani wa kuwasaidia waanzishe hizi Benki?

(b) Kwa kuwa sasa hivi Serikali haiwatendei haki wafanyakazi wake kama Walimu na wengineo kwa kutowapelekea mishahara kule walipo. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuongea na haya Mabenki ili wapeleke mishahara kwa ajili ya Watumishi wake kitu ambacho ni faida hata kwa Mabenki?

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, kuanzisha Benki Vijijini sharti ni kuwa na Milioni 50, na Milioni 50 nafikiri siyo kiasi kikubwa kwa wamiliki mtaji yaani *share holders* 50. Ukiwa na wamiliki mtaji 50, maana yake ni milioni 50 na tayari unaanzisha Benki Vijijini. Mheshimiwa Mbunge akichangia pamoja na kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya wanaweza kabisa kuanzisha Benki kijijini. Hawa walioanzisha Benki nilizozitaja: Mwanga, Mufindi na kadhalika, wamejikusanya na wameweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuhamasisha wananchi wa Wilaya hata zile ambazo ni kame alizozitaja Mheshimiwa Mbunge, uwezekanao wa kuanzisha Benki uko mkubwa kabisa kwa sababu kiwango ni kidogo cha Milioni 50. Lakini pia kuna Benki Kata ambazo wanaweza wakaanzisha, lakini pia kuna *SACCOS* ambazo wanaweza kuanzisha na wakapata pia mitaji kutoka Taasisi mbali mbali za fedha. Kwa hiyo haifanyi makusudi kwamba hawa wameanzisha na hawa iwasaadie. Waanze kwanza na Serikali pamoja na Tasisi zake itawasadid kuendeleza. Kuna *SCAT* ambayo wanatoa mitaji mikubwa katika vyombo vinavyotoa fedha ni pamoja na Benki Kata na *SACCOS*.

Mheshimiwa Spika, Siyo kweli kwamba Serikali haiwatendei haki kutowapelekea mishahara. Utaratibu umeanzishwa kwamba wafanyakazi wote wafungue Akaunti kwenye Mabenki na kila Wilaya ina Benki. Sidhani kama kuna Wilaya ambayo haina Benki na siyo kazi ngumu wafanyakazi walioko Vijijini pamoja na walimu na wengine kwenda Benki katika Makao Makuu ya Wilaya kuchukua fedha. Kwa hiyo, naamini kwamba Serikali inawatendea haki wafanyakazi na mishahara inapelekwa mpaka Wilayani. (*Makofifi*)

MHE. TALALA B.MBISE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa kuna Makao Makuu ya Wilaya nyingine ambayo hayana huduma zozote za kibenki kama vile *Usa River* Wilaya ya Arumeru. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba huduma za kibenki zinapatikana katika sehemu kama hizi kama vile *Usa River*.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU): Mheshimiwa Spika, Ombi lake tumelipokea na tutawasiliana na mabenki husika ili huduma hiyo iweze kupelekwa pale, lakini *Usa River* na Arusha siyo mbali sana nafikiri ndiyo maana Mabenki yanasisi. Lakini kwa uhakika *Usa River* pamoja na mzunguko mkubwa wa fedha ulioko naufahamu siyo muda mrefu kuanzia sasa mabenki yatachangamkia sehemu hiyo.

Na. 229

Mbolea ya *Nitrogen*

MHE. LEONARD N. DEREFA aliuliza:-

Kwa kuwa nchi yetu inayo gesi huko Songo Songo ambayo pia inafaa kwa kutengeneza mbolea ya *Nitrogen* ambayo inafaa sana kwa ardhi/udongo wa Mikoa ya Kusini ambayo ina upungufu mkubwa wa mbolea hiyo. Je, isingekuwa busara kwa sasa

mbolea hiyo ikawa inatengenezwa hapa nchini ili kupunguza bei kubwa ya mbolea hiyo muhimu kwa ajili ya uzalishaji chakula katika Mikoa ile yenye mvua za kutosha na kuondokana na tatizo la njaa kwa nchi yetu?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Leonard N. Derefa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mbolea za aina ya *Nitrogen* hutengenezwa kutokana na gesi asilia. Katika miaka ya 1980 Mradi wa *Kilwa Ammonia Company (KILAMCO)* ulibuniwa ili kutengeneza mbolea aina ya *Ammonia* na *UREA* kwa soko la ndani na soko la nje. Mradi huu ungezalisha tani 1,725 za mbolea ya *UREA* na tani 1,300 za mbolea ya *Ammonia* kwa siku na kiwanda kingegharimu fedha za Kimarekani dola milioni 450.

Harakati hizo zilisimama baada ya Serikali kukosa fedha za kuwekeza kwenye mradi na vile vile bei ya mbolea kushuka katika soko la dunia. Katika miaka ya 1990 Kampuni ya *Deepak* kutoka India ilionyesha nia ya kujenga kiwanda cha mbolea aina ya *UREA* na *Ammonia* hapa nchini, lakini majadiliano yalivunjika kutokana na mwekezaji kutoa bei ya gesi chini ya dola moja kwa kila futi za ujazo. Wawezeshaji walio wengi wamekuwa wakihitaji bei chini ya dola moja kwa futi za ujazo milioni moja wakati katika soko la dunia ni dola 5.2.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa uamuzi wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea hutegemea sana bei ya gesi, ukubwa wa mashapo (*Proven Gas Reserve*) ya gesi yenye na upatikanaji wa mwekezaji. Mahitaji ya wastani ya gesi katika utengenezaji wa tani moja ya mbolea aina ya *Nitrogen* ni kadri ya futi za ujazo 33.5.

Hii ina maana ili kuzalisha kwa mfano tano 2,700 kwa siku kiwanda kitahitaji gesi kadri ya futi za ujazo milioni 90 au futi za ujazo bilioni 657 kwa kipindi cha miaka 20.

Kiasi kilichothibitika katika mashapo ya Songo Songo ni karibu futi za ujazo bilioni 500. Kiasi hiki kimepangiwa kutumika katika miradi ya umeme na viwanda. Kiasi hiki cha mashapo hakitoshelezi mahitaji ya gesi kwa miradi ya umeme na mbolea kwa pamoa.

Mheshimiwa Spika, ili kuthibitisha ongezeko la mashapo ya gesi ya Songo Songo takwimu za uzalishaji wa gesi kwa kipindi cha miaka mitano hazina budi kukusanya. Sambamba na juhud hizi Kampuni ya *Artumas* ya Canada inafanya tathmini ya mashapo ya gesi ya *Mnazi Bay*.

Endapo matokeo ya tathmini yatathibitisha kuwepo kwa mashapo ya gesi ya zaidi ya futi za ujazo 657 bilioni, kupatikana mwekezaji na kukubali bei inayokubalika na *Artumas* na wabia wake katika mradi wa mbolea, Serikali itakuwa tayari kufanya

mazungumzo nao kwa kuzingatia ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, Leonard N. Derefa.

SPIKA: Mheshimiwa Leonard N. Derefa haelewi Kiswahili cha mashapo ya gesi. Maana yake nini mashapo ya gesi? Endelea kuuliza mwenyewe Mheshimiwa Leonard N. Derefa. (*Kicheko*)

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa kilimo ni uti wa mgongo wa taifa hili na kwa kuwa mbolea inapokosekana uzalishaji unakuwa duni. Je, nchi ambazo tunanunua mbolea wenyewe wanatumia utaratibu na utaalamu gani mpaka mbolea inakuwa rahisi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza mbolea badala ya kutengeneza mbolea hizi hasa kwa kuzingatia sasa hivi kwamba *Raw Material* inapatikana hapa nchini.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, wakati natoa majibu kwenye swali la msingi nilieleza kwamba hivi sasa hapa nchini kuna Kampuni ya Uwekezaji ya ATUMAS kutoka Canada na wao ndiyo wanaoshughulika na mradi wa gesi ya *Mnazi bay*. Nimetoa majibu kuhusu matatizo yaliyopo au upungufu uliopo wa gesi ya Songo Songo na nikatoa matumaini kwamba endapo patakuwa na gesi ya kutosha katika utafiti unaofanyika hivi sasa katika gesi ya *Mnazi bay* basi Serikali itakuwa tayari kuanzisha majadiliano na hatimaye kufanikisha majadiliano ya uwekezaji katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, kwa majibu haya ni dhahiri kwamba Serikali ina dhamira dhabiti ya kuhakikisha kwamba endapo maliasili yetu ya gesi tuliyonayo itatosheleza, basi tutaitumia hii katika uzalishaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nchi ambazo amezitaja zinazotoa mbolea, kwa kweli inategemea na mpango wa nchi na nchi, lakini kwa ujumla kwa jinsi ninavyofahamu kama nchi haina mashapo ya kutosha au gesi yake yenyewe ni dhahiri kwamba itanunua kutoka nchi nyingine ili kufanikisha kilimo na hapa nchini sisi pia tumekuwa tukiagiza mbolea kutoka nchi zingine pale ambapo tumekuwa na upungufu wa hapa ndani.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kurudia swali kwa kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mashapo maana yake ni nini, maana hatuelewi lugha hii? Je, anawenza kufafanua tukaelewa ni kitu gani?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, hapa nadhani kuna tatizo la Kiswahili hasa kwa ndugu zangu wa Kisukuma kwa sababu mashapo ndiyo Kiswahili. Labda niseme Kiingereza ni *Proven Gas Reserve*. Yaani mnapojaribu kutafiti kujua kuna gesi ya kiasi gani, ingekuwa madini tungesema

uchorongaji, lakini ile kazi ya utafutaji wa gesi ni ya *drilling* inayofanywa na kuja ndani kule kuna gesi ya aina gani. Sasa, mashapo ndiyo Kiswahili, labda pengine tungetafuta neno lingine bora zaidi. (*Kicheko*)

Na. 230

Umeme Tarafa ya Ngwashi

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali kupitia Shirika lake la Ugavi wa Umeme (*TANESCO*) liliwahi kutenga Shilingi milioni 460 mwaka 1998 kwa ajili ya kupeleka umeme Tarafa ya Ngwashi kutoka Kata ya Mamba na kupitia Kijiji cha Kwesine, Baga, Wanga, Malomboi, Ngwashi, Nkongai na kadhalika na kwa kuwa fedha hizo zilitumika kushughulikia umeme Kitaifa wakati wa ukame mkali uliokuwa umetokea mwaka huo:-

- (a) Kwa kuwa mradi huo ultengewa fedha lakini zikatumika kwa dharura ya ukame. Je, ni lini fungu hilo litapatikana?
- (b) Wananchi wa Ngwashi wategemee kupata umeme lini?
- (c) Je, zile Shilingi bilioni 1.1 zilizotegwa katika Bajeti ya mwaka 2004 kwa ajili ya Umeme Vijijini zinatumika katika vijiji gani?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kama ifuatavyo:-

- (a) Ngwashi, iko kilomita 30 kutoka Mbelei, ambako njia ya umeme wa msongo wa kilovoli 11 inapita kuelekea Mponde. Vijiji vilivyo kati ya Mbelei na Ngwashi ni Kwesine, Baga, Waga na Nkongoi. Ili kupeleka umeme huko kunahitajika kujenga laini ya kilovoti 11 kilomita 30, kujenga *low voltage* kilomita 10, kufunga transfoma kama sita, tano kati yake zikiwa za ukubwa wa *kVA 51*, kwa *kVA 51*. Gharama inakisiwa kuwa Shilingi milioni 450. Hizi ni gharama za mwaka 1999 mpaka 2000, lakini kwa sasa hivi gharama hizi zitaongezeka kulingana na upandaji wa bei ya vitu.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* kwa sasa hivi haina Bajeti mahsus kwa kazi hii. Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu pamoja na mingine imeingizwa kwenye mradi unaotegemewa kufadhiliwa na Benki ya Dunia ujulikanao kama *ERT* kwa Kiingereza unaitwa *Energizing Rural Transformation*, lakini kwa Kiswahili chepesi tunaweza kusema kwamba ni Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini au wa Kuleta Maendeleo Vijijini.

Uundwaji wa Mfuko wa Nishati Vijijini na uundwaji wa Wakala Maalum wa Kupeleka Nishaji Vijijini ni matarajio yetu kwamba utaongeza kasi katika kufanya kazi hii na kazi nyingine kama hizi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kupeleka umeme vijijini katika maeneo mengi inavyowezekana. Tunaomba Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo amekuwa siku zote, atuvumilie kiasi wakati Serikali inatafuta fedha za kupeleka umeme kwenye maeneo haya na maeneo mengine vijijini.

(c) Umeme Vijijini inahusu upelekaji umeme Makao Makuu ya Wilaya ambayo hayana umeme, vinu vya kuchambulia pamba, maeneo ya uzalishaji na kadhalika. Kwa mwaka 2004/2005 Serikali kwa kushirikiana na Shirika lake la Umeme, TANESCO lilipeleka umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya za Ukerewe na sasa hivi kazi inafanyika, Serengeti na Urambo kazi bado inaendelea, Ngara na Biharamulo ambapo miradi ya Ngara na Biharamulo tayari imekamilika na umeme kuwashwa rasmi baada ya Mheshimiwa Rais kufungua mradi huu mwezi uliopita.

Mheshimiwa Spika, kutohana na taarifa hii, hivyo basi fedha zilizotengwa na Serikali kwa ajili ya Umeme Vijijini ambazo ni jumla ya Shilingi bilioni 1.1 zimetumika katika utekelezaji wa miradi hii ya kufikisha umeme vijijini.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ningependa kujua, kwa kuwa ametaja kwamba kuna mradi huo maalum wa umeme vijijini. Je, mradi huo utanza lini hasa?

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ni matumaini yetu kwamba mradi huu utanza mapema mwakani.

MHE. PHILLIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa vile usoefu wetu wa miaka mitano iliyopita unaonyesha kwamba upelekaji wa umeme katika miji midogo kama hii iliyotajwa inategemea zaidi uamuzi wa aidha *TANESCO* au wachache katika Wizara na imeonekana kwamba kuna dalili kubwa za upendeleo, jambo ambalo siyo zuri kwa manufaa ya Taifa letu. Je, ni nani katika miaka mitano hii aliyekuwa anafanya uamuzi huu ambao umeme unatawanywa katika Wilaya A lakini katika Wilaya B umeme haupatikani pamoja na kuwa na sifa sawa. (*Makofit*)

MBUNGE FULANI: Ni nani huyo, ni nani? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Miradi ya Usambazaji Umeme Vijijini ikiwa ni pamoja na Makao Makuu ya Wilaya ni miradi ambayo hupangwa na Serikalini na Shirika letu na umeme *TANESCO* hupewa kwa utekelezaji pale haswa miradi hii inapojumuisha fedha za wafadhili na fedha kidogo za ndani za uchangiaji.

Mheshimiwa Spika, miradi hii kama nilivyosema awali inapangwa na Serikali kwa mujibu wa taratibu zilizomo ndani ya Serikali hadi kufikia miradi kukubalika. Pengine ningesema tu kwamba, inawezekana pana hisia za upendeleo, lakini kwa upande wa Serikali na kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini tunajitahidi kadri tuwezavyo tuhakikishe kwamba miradi hii inapangwa kwa mujibu wa mahitaji yalivyo na kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha, tukiweka msisitizo wa awali kwa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengine kama ambavyo niliyataja katika kujibu swali la msingi.

Na. 231

Wagonjwa Wanaotibiwa Nje

MHE. USSI YAHAYA HAJI aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania imekuwa ikiipeleka wagonjwa wake kutibiwa nchi za nje kutokana na ushauri unaotolewa na Madaktari wetu Bingwa katika kipindi cha Julai 2000 – Juni 2004 na kwa kuwa wagonjwa hao hupelekwa kutokana na ukosefu wa baadhi ya vifaa na wakati mwingine wataalam: -

- (a) Je, Serikali imepeleka wagonjwa wangapi na wa jinsi gani katika nchi za Afrika Kusini, India na Uingereza na imegharimu fedha kiasi gani kwa kila nchi?
- (b) Katika nchi hizo. Je, ni nchi gani ina matibabu ya gharama nafuu na utaalamu bora zaidi ili iwe kimbilio letu?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa matibabu hayo yote yanafanyika hapa nchini ili kuokoa fedha za kigeni na kuwapunguzia usumbufu wagonjwa wetu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO
(k.n.y. WAZIRI WA AFYA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Yahaya Haji, Mbunge wa Chaani, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara yangu hupeleka wagonjwa nje ya nchi pale inaposhindikana kutibiwa kwenye hospitali zetu. Kwa wastani kila mwaka wagonjwa watano hupelekwa Afrika ya Kusini, wagonjwa 10 hupelekwa Uingereza na wastani wa wagonjwa 50 kila robo mwaka hupelekwa India. Kwa mfano mwaka 2004 pekee tulipeleka wagongwa 209 nchini India.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kilichotumika toka mwaka wa fedha wa 2000/2001 hadi 2003/2004 kwa kupeleka wagonjwa nje ni Sh.3,675,077,552/= bila kujali mchanganuo wa kila nchi.

(b) Mheshimiwa Spika, mpaka sasa nchi ya India imeonekana inatoa matibabu ya gharama nafuu sana licha ya ubora wa hali ya juu wa matibabu yake. Kwa mfano, operesheni ya moyo (*Open Heart Surgery*) kwa mtoto nchini India ni katika Dola za Kimarekani 1,500 hadi Dola za Kimarekani 2,500 kulingana na ukubwa wa tatizo. Nchi za Afrika ya Kusini na Ulaya hutoza katika Dola za Kimarekani 4,500 hadi Dola 10,000 kwa tatizo hilo hilo.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mpango wa kujenga Hospitali ya kisasa Jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali toka Japan liitwalo *TOKUSHUKAI*. Hospitali hii pamoja na mambo mengine matibabu ya magonjwa ya moyo.

Aidha, Taasisi ya Mifupa Muhimbili (*MOI*) imeanza kutoa huduma ambazo hapo awali zilikuwa zikitolewa nje ya nchi. Huduma hizo ni pamoja na kubadilisha mfupa wa nyonga (*Total Hip Joint Replacement*)

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya moyo (*Tanzania Heart Institute*) imeanza ujenzi wa Hospitali kubwa itakayokuwa ikitibu magonjwa makubwa ya moyo (*Open Heart Surgery*). Serikali itafanya makubaliano maalum (*Memorandum of Understanding*) kuhusu utumiaji wa huduma zake.

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niulize swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa Serikali inaingia gharama nyingi sana kwa kuwatibu wagonjwa mbalimbali. Je, ni kwa nini hatupeleki Madaktari wetu kwenda kujifunza huo utaalamu ili kuokoa hizi fedha tukatibiwa hapa hapa nchini?

NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA AFYA): Mheshimiwa Spika, kwa kweli jitihada zinafanywa za kuhakikisha tunapunguza gharama hii na tatizo letu siyo Madaktari. Madaktari hao tunao, tatizo letu ni vifaa vya utabibu, ndiyo maana tunaamua kujenga hiyo hospitali ya kisasa tushirikiane na hii Taasisi ya Moyo. Vifaa hivi vikishapatikana na hospitali ikishajengwa, nina uhakika tatizo la kupeleka wagonjwa nje litakuwa limepungua au limeisha kabisa.

Na. 232

Uharibifu wa Mazingira Kutokana na Wakimbizi

MHE. NAZIR M. KARAMAGI (k.n.y. MHE. GWASSA A. SEBABILI)
aliuliza: -

Baada ya wimbi kubwa la Wakimbizi kutoka Burundi mwaka 1993 na wale wa kutoka Rwanda Mwaka 1994 ilifanya Wilaya ya Ngara kuwa na wakimbizi karibu 1,000,000 mwaka 1996 na kwa kuwa kati ya madhara yaliyoletwa na Wakimbizi hao na ambalo lilishtua ulimwengu ni lile la uharibifu wa mazingira kwenye maeneo walimoingilia na kukaa kabla ya kujengewa makambi ya kuishi; na kwa kuwa maeneo ya Benaco, Musukula, Rukole, Lumas na Mbuba katika Tarafa za Nyamiaga na Rulenge yaliharibiwa sana na haitegemewi kama uoto wake wa asili utarudia tena kwa miaka ijayo kwani bado uharibifu unaendelea:-

- (a) Je ni hasara kiasi gani (kwa fedha) ambazo Serikali imepata kwa miaka tisa (9) ambayo Wakimbizi wamekuwepo Wilayani Ngara?
- (b) Je, Serikali inachukua hatua gani za makusudi za kuokoa hali hiyo ambayo inaendelea kuathiri hali ya hewa, maisha ya watu na viumbe hai?
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ili kuanzisha *operation* kabambe ya kupanda miti ili Jumuiya hiyo iweze kuridhika na Siasa ya Tanzania kuwa haki za binadamu zinalindwa na binadamu wote ni sawa na kwamba jambo hilo linatekelezwa kivitendo hata kama kwa kujinyima?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika napenda kujibu swalii na Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mbunge wa Ngara, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba wimbi kubwa la Wakimbizi kutoka Burundi na Rwanda la mwaka 1993 – 1994 lilisababisha uharibifu mkubwa wa mazingira. Serikali ilifanya tathmini kuhusu athari zilizotokea ambapo madhara yaliyobainika ni kama ifuatavyo: -

- Eneo la hekta 58,780 za misitu zilifyekwa katika Wilaya za Biharamulo, Karagwe na Ngara katika kipindi cha miaka 1994 - 2001;
- Kuharibiwa kwa vyanzo vya maji likiwemo bwawa la Benaco;
- Kuuawa kwa maelfu ya wanyama ndani ya hifadhi za Ibanda na Burigi; na
- Kuzagaa kwa silaha na kuongezeka kwa uhalifu.

Mheshimiwa Spika, siyo rahisi kupata hasara iliyopatikana kwa kipimo cha fedha. Ninachowenza kusema tu ni kwamba athari za kiuchumi na kijamii ni kubwa katika maeneo yanayohifadhi Wakimbizi.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya kutambua athari hizo Serikali kwa kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa ilianzisha miradi ifuatayo: -

- Mradi wa kuhifadhi mazingira na misitu. Mradi huu ulifadhiliwa kwa kiasi kikubwa na Shirika la *IFAD* na *UNHCR*.
- Mpango wa ukarabati wa miundombinu kama vile barabara, viwanja vya ndege na kadhalika, ambayo ilifadhiliwa na wahisani mbalimbali ikiwemo Umoja wa Nchi za Ulaya na *USAID*.
- Kuanzishwa kwa utaratibu wa kuimarisha ulinzi na usalama kwa kupeleka Askari Polisi wa ziada katika Wilaya zenye Makambi ya Wakimbizi, chini ya utaratibu wa unaoitwa *Security Package* unaogharimiwa na *UNHCR*; na
- Mradi wa ukarabati wa Shule za Msingi na Zahanati uliofadhiliwa na nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Misitu, miche ipatayo 8,500,000 ilipandwa katika Mkoa wa Kagera ili kukabiliana na athari za uharibifu wa mazingira.

Hata hivyo tathmini ya mradi huo inaonyesha kuwa nusu ya miti hiyo iliharibika kwa sababu ya uchomaji moto, jambo ambalo ni tatizo kubwa hasa katika Wilaya ya Ngara. Kuhusu miti iliyobakia, uhamasishaji unaendelea ili miti hiyo iweze kukua (itunzwe na ikue).

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Viongozi wa Wilaya ya Ngara waendelee kuwahamasisha Wananchi ili waendelee kupanda na kutunza miti kama Watanzania wengine pote nchini wanavyofanya chini ya Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji Miti ya kila mwaka.

MHE. NAZIR M. KARAMAGI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mazingira mengine yaliyoharibiwa hususan katika Mkoa wa Kagera ni mazingira ya watu kutembea kwa usalama. Tunajua Mkoa wa Kagera mpaka sasa hivi mapori yanayounganisha Karagwe na Ngara, Muleba na Biharamulo ni hatari kupita.

Je, Serikali ina mpango gani hasa wa kudumu kuangalia ushauri angalau hata wa kuweka Kambi za Jeshi ndani ya mapori hayo kusudi yawe salama kwa Wananchi kupita? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba, moja ya athari za Wakimbizi ni pamoja na silaha ndogo ndogo kuzagaa na uhalifu. Sasa Mheshimiwa Mbunge anauliza tuna mpango gani wa kudumu katika kutatua tatizo hili. Kwanza, mpango wa sasa hivi ni kuongeza ulinzi katika maeneo hayo. Kama nilivyosema, tunapeleka Polisi wa ziada katika makambi na maeneo yanayozunguka makambi. Jeshi la Wananchi liko katika maeneo hayo kwa kiwango cha kutosha kukabili tatizo hili. Sasa hatua hizi kwa hakika zimesaidia kupunguza athari za ulinzi na usalama.

Lakini suluhisho la kudumu kama ambavyo kila siku nasema ni hapo Wakimbizi wote wanaosababisha athari hizi watakaporudi makwao. Huo ndio ufumbuzi wa kudumu, lakini kama nilivyoarifu huko nyuma kwamba, zoezi la kurudisha Wakimbizi wa Burundi, limeanza na linaendelea vizuri na taarifa ambazo tumezipata ni kwamba, baada ya uchaguzi wa Wabunge kwenda vizuri, sasa hivi kasi ya Wakimbizi kurundi Burundi imeongezeka mara mbili. Kwa hiyo, nina hakika kabisa kwamba, tutamaliza hiyo ngwe ya Wakimbizi wa Burundi na mwezi huu tarehe 16 Julai, 200, yaani wiki ijayo, tutafanya mazungumzo kati ya Serikali ya Tanzania, Serikali ya *DRC Congo* na *UNHCR* vilevile kuweka utaratibu wa kuwarudisha Wakimbizi wa Congo. Kwa hiyo, kwa pamoja wakishaondoka kabisa, nafikiri katika eneo hili athari za kiusalama zitapungua sana.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Naibu Waziri, alikiri kwamba, Wakimbizi waliharibu misitu na akataja idadi ya miti iliyokatwa na alikiri kwamba, Wakimbizi walipanda miti ipatayo zaidi ya milioni moja, lakini mwisho alitoa wito kwa viongozi wa Ngara kwamba, wawahamasishe Wananchi wa Ngara wapande miti; hivi lini Serikali itabadilisha sera yake kufanya Wakimbizi usiwe mzigo iwe kama ni nguvu kazi na kuwashamasisha Wakimbizi wenyewe wapande miti ambayo wameiharibu? (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, miti iliyopandwa sio milioni moja, kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema, ni milioni nane na laki tano. Miti hii ilipandwa na Wakimbizi wenyewe kwenye maeneo yale ambayo waliharibu na mpaka sasa bado wanaendelea kupanda. Kwa hiyo, nilikuwa natoa wito kwamba, viongozi wa Ngara wawahamasishe Watanzania wengine kwanza, waache kuchoma moto, maana yake mioto hii haianzii kwenye makambi ya Wakimbizi inaanzia kwa wanavijiji kuanza kuchoma moto, lakini wenyewe waendelee kupanda miti na kuitunza.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa *UNHCR* na Umoja wa Mataifa, wanajaribu kumhifadhi na kumlinda Mkimbizi kwa kumpelekea chakula, mahema na mambo mengine; na kwa kuwa sisi pia ni Wajumbe wa Umoja wa Mataifa; kwa nini sasa hatuchukui juhudii za kutosha,

kulifanya Shirika la Umoja wa Mataifa liweze kuweka sawa matatizo ambayo yameachwa nyuma na Wakimbizi kama vile uporaji, uharibifu wa mazingira na mengine?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, *UNHCR*, pamoja na kwamba linahudumia Wakimbizi, hawa ni binadamu wenzetu ambao wamepata matatizo sasa wamekimbia kwao na sisi tumo humo humo kwenye *UNHCR*, tuna wajibu wa kuwasaidia kwa kipindi ambacho wako katika matatizo. Lakini vilevile nchi mbalimbali, pamoja na *UNHCR* yenyewe, imekuwa inatusaidia kupunguza athari zinazotokana na sisi kubeba mzigo wa Wakimbizi. Kwa mfano, ile miradi niliyoitaja ya kupanda miti, miundombinu, zahanati, mashule, wanafanya sana *UNHCR* wakisaidiwa na Mataifa mengine ya nje. Hata ule mradi tuliosema tunaapeleka Polisi wa ziada kwenye maeneo ya Wakimbizi, ambao kila baada ya miezi sita tunapeleka kikosi, gharama zote za kuwatunza wale askari za magari, *radio call* na kadhalika, zinabebwa na hiyo *UNHCR*. Kwa hiyo, tunataka kusema tu kwamba, ni shirika ambalo linatoa msaada mkubwa kutupunguzia athari za wakimbizi.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

Majibu ya nyongeza ni kwamba, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (*UNEP*), kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark, katika Halmashauri za Wilaya ya Kasulu, Kibondo na Ngara na hususan kule Halmashauri ya Kibondo, ninayoifahamu zaidi, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, yaani mwaka huu na mwaka kesho, katika juhudzi za kurekebisha mazingira yaliyoharibika, kila Halmashauri imepata shilingi bilioni mbili ili kusaidia kurekebisha maeneo yaliyoharibiwa na Wakimbizi. (*Makofit*)

Na 233

Ufunguzi wa Kituo cha Polisi Kibaigwa

MHE. JOB Y. NDUGAI aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali iliahidi Bungeni kufungua kituo kipy Cha Polisi kilichojengwa na Wananchi pale Kibaigwa kabla ya kipindi cha bajeti ya 2005/2006; na kwa kuwa, kituo kinahitaji askari wa kutosha na gari la doria; je, Serikali inasema nini juu ya jambo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:- Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa, Serikali iliahidi kufungua Kituo kipy Cha Polisi, kilichojengwa na nguvu za Wananchi wa Kibaigwa Wilayani Kongwa kabla ya kipindi cha bajeti ya mwaka 2005/2006, iwapo Wananchi wangekamilisha upatikanaji wa nyumba za kuishi askari. Hata hivyo, tunasikitika kwamba, hadi sasa kituo hicho bado hakijafunguliwa kwa sababu ya ukosefu wa nyumba watakamoishi askari na familia zao.

Tunatoa wito kwa Viongozi na Wananchi wa Kibaigwa kwamba, tuendelee kushirikiana ili zipatikane nyumba za askari na ndipo kituo kitafunguliwa. Baada ya kufunguliwa kituo, Serikali itakuwa na wajibu wa kupeleka askari na vitendea kazi muhimu kama vile vifaa vya mawasiliano, usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, aidha wiki iliyopita, kufuatia mwaliko wa Mheshimiwa Job Ndugai, nilitembelea Kibaigwa, ambapo tulishirikiana na Mheshimiwa Job Ndugai, Mkuu wa Wilaya Kongwa na Viongozi wa Halmashauri Wilaya ya Kongwa, kuhamasisha mchango wa kukarabati jengo la Kongwa litakalotumiwa kama nyumba ya kuishi askari. Katika uchangishaji siku hiyo zilipatikana shilingi 1,600,000/= na mchango inaendelea. (*Makofi*)

Kwa ari ambayo tuliiiona siku hiyo, tuna uhakika kwamba, upo uwezekano mkubwa kwamba, kazi ya kukarabati jengo hilo itakamilika ifikapo mwishoni mwa Septemba na hapo tutafungua Kituo cha Kibaigwa. (*Makofi*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii moja dogo la nyongeza. Nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutembelea Kibaigwa na kujionea mwenyewe hali halisi ya Kituo cha Polisi ambacho kilishajengwa na Wananchi sasa kinaanza kuliwa na mchwa.

Kwa vile Kibaigwa pana soko la Kimataifa ambalo lilizinduliwa tarehe 6 na Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein na hali ya usalama ni ndogo na Wananchi wako tayari kuungana na Serikali yao kujenga nyumba za askari. Je, Serikali itakuwa tayari angalau kutusaidia fedha za kujenga nyumba mbili au tatu kwa ajili ya Polisi na gari la doria? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kweli nitoe pongezi za dhati kwa msukumo anaoutoa Mheshimiwa Job Ndugai kwanza, kwa kuwezesha kile kituo kikamilike ambacho juzi nilikikagua, ni kituo kizuri na niliwasifu kwamba, ni kituo kizuri na kikubwa kuliko baadhi ya vituo vya Wilaya. Ni kweli kwamba, kwa sababu jengo halijaanza kutumika, mchwa wameanza kutembelea tembelea lakini nimekuta yuko pale Mtendaji wa Kata hodari ameshaanza kuweka dawa. Sasa kuhusu suala lake la nyumba ni kweli kwamba, tumeshapeleka ramani za nyumba pale, Wananchi wenyewe wameonesha ari kubwa ya kuanza kuchangia na tuliwaeleza siku ile jinsi ambavyo tulisaidiana katika kujenga Kituo cha Polisi. Maana yake na sisi Serikali tulichangia kwenye kujenga hicho kituo. Kwa hiyo, katika kujenga nyumba za askari, utaratibu ule ule wa ushirikiano kati ya Wananchi na Serikali utaendelea.

MHE. LYDIA T. BOMA (k.n.y. MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA)
aliuliza:-

Kwa kuwa, soko kwa korosho zilizobanguliwa ni kubwa na nono; na kwa kuwa, kasi yetu ya kubangua ni ndogo sana; je, kuna ugumu gani kama tukiweka utaratibu wa kuwazuia wafanyabiashara wa korosho wa Asia, kutosafirisha korosho ghafi na badala yake wanunue na kubangulia humu nchini?

NAIBU WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swal la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, Mbunge wa Mtwara Vijiji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, korosho zilizobanguliwa huongezeka thamani na kuvutia wanunuzi wengi na kwa bei nzuri zaidi ya ile ya korosho ghafi na kwa hiyo, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge ya kuwa, soko la korosho zilizobanguliwa ni kubwa na lina bei nzuri. Kwa kuzingatia ukweli huo, Serikali pia ingependelea zaidi uuzaji wa korosho zilizobanguliwa kuliko ule wa korosho ghafi, kama uwezo wetu wa kubangua korosho zote zinazozalishwa nchini ungelikuwepo. Lakini uwezo wa viwanda vyetu vya kubangulia korosho vilivyopo na vinavyofanya kazi bado ni mdogo sana ukilinganisha na wingi wa korosho yetu yote inayozalishwa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hivi sasa kati ya viwanda 12 vilivyorithiwa na Bodi ya Korosho kutoka kwa iliyokuwa Mamlaka ya Korosho Tanzania, ni viwanda viwili tu vilivyoko Kibaha na Masasi, ndivyo vimekarabatiwa na kila kiwanda kina uwezo wa kubangua tani 10,000 za korosho ghafi kwa mwaka. Aidha, kuna viwanda vingine vitatu vya kubangua korosho vilivyojengwa na watu binafsi, ambavyo vina uwezo wa kubangua korosho jumla ya tani 15,800 za korosho katika mchanganuo ufuatao: *Premier Cashew Industries Limited* tani 10,000, *Mohamed Enterprises* tani 1,000 na *OLAM (T) Ltd.* tani 4,800.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo pamoja na uwezo uliopo wa viwanda hivyo, bado viwanda hivyo vinafanya kazi chini ya uwezo wake. Kwa mfano, katika msimu wa 2002/2003, ambapo uzalishaji wa korosho nchini ulikuwa tani 95,000, Kiwanda cha Kibaha kilibangua korosho tani 380, Kiwanda cha Masasi kilibangua tani 800, Kiwanda cha *Premier Cashew Industries Ltd.* kilibangua tani 5,140, Kiwanda cha *Mohamed Enterprises* kilibangua tani 480, Kiwanda cha *OLAM (T) Ltd.* kilibangua tani 550. Aidha, vikundi vya wabanguaji wadogo wadogo vilibangua tani 60 za korosho na hivyo kufanya jumla ya korosho zilizobanguliwa kufikia tani 7,410, kiasi ambacho ni karibu sawa na asilimia nane tu ya tani 95,000 za korosho ghafi zilizozalishwa katika msimu ule wa 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwezo huo mdogo, wawekezaji wa viwanda vya kubangulia korosho, pamoja na vikundi vya wabanguaji wadogo wadogo, wanakabiliwa pia na tatizo la kukosa mitaji ya kununulia korosho za kutosha na wakati huo huo kuwa na fedha za kuendesha shughuli za ubanguaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hii, nchi yetu bado haina uwezo wa kubangua korosho zote zinazozalishwa hapa nchini. Kwa hiyo, kwa sasa Serikali haitazuia usafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi kwani kuuza korosho ghafi bado kunawapatia wakulima kipato angalau kidogo na hivyo kupiga vita umaskini. Serikali inaendelea kuwashawishi wawekezaji na wamiliki wa viwanda wanaobangua korosho hivi sasa ili waendelee kuwekeza na kubangua korosho kulingana na uwezo wa viwanda vyao. Aidha, Serikali inaendeleza juhudini zilizokwisha anza, za kubinafsisha viwanda vya kubangua korosho, pamoja na kuwahamasisha wabanguaji wadogo wadogo wa korosho kwa kutoa mafunzo juu ya taratibu za uundaji wa vikundi hivyo, ubanguaji korosho, upangaji wa korosho katika madaraja na ufungaji ili kuongeza wingi wa korosho zilizobanguliwa na kukidhi mahitji ya wateja mbalimbali.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha, kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine, tukianza na matangazo ya vikao vya leo ni viwili. Kamati ya Kilimo na Ardhi, Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 11 Julai, 2005 kutakuwa na kikao kuanzia saa 5.00 asubuhi chumba Na. 219. Kamati ya pili, ni Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Mheshimiwa Profesa David Mwakyusa, Makamu Mwenyekiti, anawatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba, leo tarehe 11 Julai, 2005, kikao kitafanyika saa 4.30 katika Ukumbi Namba 231, ghorofa ya pili Mwisho wa matangazo, Katibu endelea na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2005/2006 - Wizara ya Viwanda na Biashara

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, iliyochambua bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Matumizi ya Maendeleo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu ni muhimu sana katika historia ya nchi yetu, kwani Utawala wa Serikali ya Awamu ya Tatu, unahitimisha muhula wake wa dhamana iliyokabidhiwa na Wananchi kuititia Chama Cha Mapinduzi ya kuongoza maendeleo ya uchumi na jamii nzima ya Watanzania, kwa mujibu wa mpangilio wa ahadi, kazi na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Sisi katika Wizara ya Viwanda na Biashara, tunawashukuru na kuwapongeza viongozi wetu chini ya uongozi shupavu wa Rais wetu mpewda, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Makamu wake, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, kwa kudumisha amani nchini na kwa kuongoza Taifa kwa mafanikio makubwa katika kipindi chote cha miaka kumi. Tunaiombea nchi yetu ihitimishe Uchaguzi Mkuu, kwa amani, utulivu na haki, baadaye mwaka huu, ili kudumisha mazingira yenye kutoa fursa kwa kuongeza kasi zaidi ya

ukuaji wa sekta za viwanda na biashara, ambazo ni nguzo muhimu katika kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi wa kisasa wa Taifa letu.

Napenda kutumia nafasi hii pia kuwashukuru wote ambao michango yao imesaidia sana katika kuandaa bajeti ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara. Kwa namna ya pekee, naishukuru Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa mchango na ushauri wao wenye ubunifu na uwazi, wakati wa kujadili Makadirio ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tangu kipindi cha bajeti cha mwaka 2004 hadi sasa, Bunge lako Tukufu na Taifa kwa ujumla, limeondokewa na Wabunge wake hodari ambao wamefariki dunia. Wabunge hao ni Marehemu Mheshimiwa Yetet Sintemule Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, Marehemu Mheshimiwa Capt. Theodos James Kasapira, aliyekuwa Mbunge wa Ulanga Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati, aliyekuwa Mbunge wa Kasulu Mashariki, Marehemu Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, aliyekuwa Mbunge wa Rahaleo, Marehemu Mheshimiwa Abu Towegale Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Rukwa. Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii, kumshukuru Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick T. Sumaye, kwa hotuba yake fasaha, iliyoelezea kwa undani mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu. Napenda pia kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Pesambili Mramba, ambao hotuba zao zimetoa mwelekeo wa uchumi wetu na malengo ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2005/2006, yenye dira na mikakati ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini katika nchi yetu. Aidha, napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wote, walionitangulia kutoa hotuba za Bajeti za Wizara zao humu Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii, kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Mbunge wa Chalinze, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, kwa kuteuliwa na Chama chetu Cha Mapinduzi, kuwa Mgombea wa Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2005. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, kuwa mgombea mwenza na Mheshimiwa Amani Abeid Amani Karume, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuwa mgombea wa Urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2005. Wagombea hawa wote wa CCM nawatakia ushindi wa kishindo mithili ya kimbunga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, Serikali iliandaa na kuanza utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (*Sustainable Industrial Development Policy (SIDP) 1996-2020*). Malengo ya Sera hii yameweka mkazo katika kuendeleza viwanda vya usindikaji wa mazao ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao husika na hivyo kukuza mapato kwa wakulima na mapato ya fedha za

kigeni kwa kuuza bidhaa za viwanda nje ya nchi badala ya bidhaa zisizosindikwa. Pia, uongezaji wa usindikaji mazao nchini unawawezesha wakulima wetu kupata masoko ya ndani ya uhakika zaidi kuliko yale ya nje, ambayo yamekuwa na bei za kubadilika mara kwa mara. Utekelezaji wa Sera hii umezingatia malengo ya Dira ya Taifa (*Vision 2025*), ambayo imeweka bayana kwamba, sekta ya viwanda inatakiwa kuifikisha nchi yetu katika kiwango cha maendeleo ya viwanda ya kati (*Semi-industrialised Country*) ifikapo mwaka 2025. Ili kutekeleza Sera hii, mbinu mbalimbali zimetumika ikiwa ni pamoja na kuandaa Programu Maalum. Serikali, kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (*UNIDO*), ilibuni na kutekeleza awamu mbili za Programu Oanishi ya Kuendeleza Viwanda (*Integrated Industrial Development Programme*).

Kuanzia mwaka 1998 hadi kufikia mwishoni mwa awamu ya pili mwaka 2006, mikakati mbalimbali ambayo imetekeliza na inayoendelea kutekeleza inajumuisha ifuatayo:-

- (a) Kujenga uwezo wa Serikali na Sekta Binafsi katika kuendeleza viwanda na biashara ndogo;
 - (b) Kuboresha mazingira na taratibu za uwekezaji;
 - (c) Kuongeza uwezo wa viwanda wa ushindani katika uchumi wa soko;
 - (d) Kujenga mfumo wa kuhifadhi, kuimarisha na kuendeleza mazingira;
 - (e) Kufanya utafiti wa kina kuhusu sekta za nguo, ngozi na vyakula kwa lengo la kubaini matatizo ya sekta hizi muhimu na kutoa mapendekezo ya kufufua, kuziendeleza na kuziimarisha sekta hizi;
 - (f) Kupunguza upotevu wa mazao ya kilimo baada ya mavuno ikiwa ni pamoja na kuhamasisha na kuhimiza uanzishwaji wa viwanda vya kusindika mazao ya kilimo; na
 - (g) Kufanya utafiti ili kubainisha mtiririko wa thamani (*Value Chain*) ya mazao kwa kuanzia na zao la mhogo, matunda, mbegu za mafuta, mpunga, maharage na korosho.
- Mheshimiwa Spika, Serikali pia iliandaa na kupitisha Sheria ya *Export Processing Zones Act (EPZ)* Na.11 ya mwaka 2002 ya uanzishaji wa Maeneo Maalumu ya Kuzalisha Bidhaa za Kuza Nje, kama hatua mojawapo ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda (*SIDP*). Makampuni matano yamejenga miundombinu ya EPZ, ambayo ni *Millennium Business Park Ltd., NIDA Textile Ltd., Hifadhi EPZ, Mwananchi Gold Co. Ltd. na Gomba Estates Ltd.* Aidha, viwanda sita vimeanzishwa vya

kuzalisha bidhaa za kuuza nchi za nje. Viwanda hivyo ni *Star Apparel Ltd., NIDA Textile Mills Ltd., Reclaimed Appliances Ltd., African Pride Textile Mills, Mwananchi Gold Ltd.* na *Gomba Estate Ltd.* Thamani ya miundombinu hiyo ni Dola za Kimarekani milioni 70. Hadi kufikia mwezi Juni, 2005, viwanda hivyo kwa pamoja vimetoa ajira kwa watu 2,000 na kuuza bidhaa nje zenyenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 10.

Mheshimiwa Spika, chini ya Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda, Serikali ya Awamu ya Tatu iliendelea na utekelezaji wa sera ya ubinafsishaji na urekebishaji wa mashirika na makampuni ya umma kwa lengo la kufufua na kuimarisha uzalishaji katika Sekta ya Viwanda. Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, viwanda vingi vya umma vilipata wawekezaji wapya waliovifanyia ukarabati na kuvifufua ikiwa ni pamoja na vile vilivyokuwa vimesimamisha uzalishaji kwa muda mrefu, kama vile viwanda vya nguo vya *Sunguratex, Mbeyatex, Mutex, Kiltex* (Arusha), *Mwatex, Morogoro Polyester* na Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo (*SPM*). Uzalishaji wa bidhaa viwandani umeendelea vizuri na bidhaa za viwanda vyetu kusambazwa nchini kwa wingi na kuchangia kukidhi mahitaji ya Wananchi.

Kwa sasa bidhaa nyingi za viwanda vyetu zinaonekana katika maduka mbalimbali zikishindana na bidhaa kutoka nje ya nchi, jambo linaloashiria kuimariika kwa Sekta ya Viwanda nchini na mwelekeo mzuri wenye matumaini katika uchumi wa Taifa letu hususan ikilinganishwa na mwanzoni mwa miaka ya 80.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta za Viwanda na Biashara, zoezi la ubinafsishaji linakaribia kukamilika. Baada ya kukamilisha sehemu kubwa ya ubinafsishaji, Mashirika Mama yamefungwa isipokuwa Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*). Mashirika haya mawili yamebakizwa kwa makusudi ili yawe mkono wa Serikali katika kuendeleza miradi mikubwa na midogo ya maendeleo kwa kushirikiana na sekta binafsi, ambayo imepewa kipaumbele katika Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda na kuwezesha ubainishaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Aidha, Mashirika haya yanatarajija kuwa vyombo muhimu katika uwezeshaji Wananchi kiuchumi wakati utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi itakapopata kasi muafaka.

Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, hatua za kuongeza uwezo wa viwanda pia zimefanyika, kwa mfano, upanuzi wa Kiwanda cha *A to Z* cha vyandarua vyenye dawa vinavyouzwa ndani na nje ya nchi na upanuzi wa kiwanda cha chai cha *Wakulima Tea Co.*, ambacho kimeweza kuongeza usindikaji wa chai maradufu. Vilevile, katika kipindi hicho viwanda vipyta vimeanzishwa. Viwanda hivyo ni pamoja na viwanda vya nguo vya *Karibu Textile Mills Ltd., Lakhani Textile Industries Ltd., NIDA Textile Mill Ltd., Star Apparel Ltd.* na *African Pride Textile Mill Ltd.* Vingine ni viwanda vya mafuta ya kula vya *Murzah Oils Ltd., BIDCO Soap and Oil Ltd.* na *Best TIGRA*, viwanda vya kusindika maziwa, kiwanda cha *Mwamba Breweries* kilichoko Mbeya na kiwanda cha mbao cha *TANWAT*, ambacho kimeanzishwa baada ya Serikali kupiga marufuku uuzaji wa magogo nje ya nchi.

Kiwanda kingine ni cha kutengeneza sigara kilichoko Iringa, kiwanda cha kusindika takataka za plastiki (*Recycling Plant*) kilichoanzishwa Mjini Morogoro na

viwanda vya kuyeyusha chuma kutokana na chuma chakavu vikijumuisha *MM Integrated Mill, Iron & Steel Ltd., Steel Master, Simba Steels Ltd., Dar Steel Mill* na *Metro Steel Mills Ltd.* vilivyopo Jijini Dar es Salaam, *Trishala Rolling Mills* na *Hans Nails* vya Arusha, *Nyakato Steel Mills* cha Mwanza na *Unique Steel Rolling Mills Ltd.* cha MJini Tanga. Viwanda vya chuma vimeongezeka zaidi baada ya amri ya Serikali ya kuzuia uuzaji nje (*export*) wa chuma chakavu iliyoanza rasmi tarehe 21 Mei, 2003. Amri hii inaendelea hadi Mei, 2006 ili kuiwezesha Serikali kuandaa mikakati endelevu wa kulishughulikia suala hili la chuma chakavu.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo (*SME Policy*), iliandaliwa na Wizara na kuidhinishwa na Serikali mwezi Februari, 2003 na kuzinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, mwezi Agosti, 2003. Lengo kubwa la sera hiyo ni kuwawezesha Wananchi kushiriki zaidi katika shughuli za kiuchumi kwa kuchochea uanzishwaji wa miradi mipywa wingi na pia kuiimarisha ile iliyopo. Ili kufikia lengo hilo, mikakati kadhaa inatumika ikiwa ni pamoja na kujenga mazingira mazuri ya kisheria; kuboresha upatikanaji wa maeneo ya kufanyia kazi; kuimarisha upatikanaji wa huduma za kuendeleza sekta katika nyanja za teknolojia, masoko, upatikanaji wa taarifa na uendelezaji ujasiriamali; kuboresha upatikanaji wa mitaji na kuimarisha mfumo wa vyombo vya kitaasisi wa kuiendeleza sekta ya viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya uzinduzi wa sera hiyo, mambo ya msingi yafuatayo yamefanyika:-

- (a) Sera imetafsiriwa katika lugha ya Kiswahili na pia maandalizi yanafanyika ya kuchapishwa makala za sera katika lugha rahisi inayotumia picha na michoro (*Popular Version*) ili kutoa ujumbe kwa urahisi na kuwafikia Wananchi wengi zaidi;
- (b) Warsha za kikanda zimefanyika kwa lengo la kuwafahamisha na kuwahamasisha wadau mbalimbali kushiriki katika utekelezaji wa sera. Warsha hizo zimeweka bayana majukumu ya wadau wote katika utekelezaji wa sera; na
- (c) Kuandaa na kunadi kwa wahisani programu na miradi ya kutekeleza sera ambayo mingi imekubalika.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika mikakati ya Serikali ya kutekeleza sera hii, hatua mbalimbali zimechukuliwa ikiwa ni pamoja na:-

- (a) Uanzishwaji wa mfuko wa dhamana wa Maendeleo ya Viwanda na Biashara Ndogo (*SMEs Guarantee Fund*);
- (b) Uendeshaji wa mafunzo ya ujasiriamali;
- (c) Utoaji wa ushauri katika nyanja mbalimbali na huduma za ufundi; na

(d) Kuhamasisha na kuwaelimisha Wananchi wengi zaidi ili kuelewa vizuri umuhimu wa sera hii.

Kutokana na mikakati hiyo, Wananchi wengi hasa wa kipato cha chini, wamehamasika na kuanzisha miradi mingi midogo ikiwemo ya viwanda nya kukamua mafuta ya kula kutokana na mbegu, viwanda nya samani, viwanda nya kusindika matunda, ufumaji wa nguo na ushonaji ambayo imechangia katika juhudzi za kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, Wizara inazo taasisi za huduma za teknolojia ambazo ni muhimu katika kufanya utafiti kwa maendeleo ya viwanda. Taasisi hizo ni pamoja na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (*TIRDO*), Kituo cha Kueneza Teknolojia Rahisi Vijijini (*CAMARTEC*) na Shirika la Ubunifu wa Mitambo (*TEMDO*).

Taasisi hizi katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005 zimetekeleza majukumu yake kwa ufanisi, ingawa katika mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti. *CAMARTEC* ilibuni na kuendeleza teknolojia za nishati mbadala zifuatazo: Majiko sanifu yatumiayo pumba na randa, majiko yatumiayo nishati ya mionzi ya jua, mitambo ya kuchemshia maji itumiayo nishati ya mionzi ya jua na pampu itumiayo nishati ya upepo. Vile vile, kituo kiliendelea kujenga mitambo ya *biogas* sehemu mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi. Mitambo 41 imejengwa Malawi na Rwanda. Hapa nchini imejengwa mitambo 136. Aidha, *CAMARTEC* ilitengeneza na kusambaza majiko sanifu makubwa 83 katika shule za Sekondari 27 nchini Rwanda. Pia, majiko yapatayo 200 yalisambazwa hapa nchini. Vilevile, *CAMARTEC* imetengeneza na kusambaza zaidi ya mashine 1,500 za kukamua mafuta ya mbegu na mazao mbalimbali katika ngazi ya kaya. Mashine hizi zimechochea kilimo cha mbegu za mafuta, upatikanaji wa mafuta ya kula yaliyo safi na salama na ajira kwa Wananchi. Aidha, Kituo kimefanya majoribio na tathmini ya Zana za Kilimo. Mashine na zana zipatazo 20 za aina mbalimbali yakiwemo matrekta saba kutoka China, India, Yugoslavia na Japan, zilifanyiwa majoribio na tathmini. Kutokana na ufanisi wa hali ya juu ya ubora wa bidhaa na huduma zake. *CAMARTEC* mwaka 2004 ilitunukiwa Tuzo ya Ubora ya Karne ya 21 nchini Mexico.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia zilizobuniwa na kuendelezwa na *TEMDO* zililenga katika kuboresha hali ya maisha ya Wananchi walio wengi, pamoja na kuendeleza ujasiriamali na kuongeza ajira. Katika kutimiza azma hii, teknolojia zilizopewa kipaumbele ni za kusindika mazao ya kilimo, kuongeza thamani ya mazao, kupunguza uharibifu baada ya mavuno na uhifadhi wa mazao. Vilevile, *TEMDO* ilibuni teknolojia na chasili za mashine za kukamua mafuta ya alizeti na mawese, asali, kusindika matunda, kuweka dawa kwenye mbegu na nafaka na mashine za kupukuchua mahindi.

Mheshimiwa Spika, huduma za kiuhandisi na mafunzo kwa viwanda vikubwa, nya katika na vidogo, zililenga katika kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa. Viwanda ambavyo vimepata huduma kubwa za kiuhandisi kutoka *TEMDO* vinajumuisha viwanda nya Saruji nya Tanga, Mbeya na Dar es Salaam; viwanda

vya Sukari vya Moshi na Kilombero; kiwanda cha Kimea cha Moshi (*TBL Maltings Co. Ltd.*); viwanda vya nguo vya *Sunflag* na *A to Z* vyote vya Arusha; kiwanda cha kuchambua pamba cha Moshi na viwanda vya Kahawa vya Moshi na Mbozi. Zana za kilimo 200 na mikokoteni 1,000 inayokokotwa na wanyamakazi zilitengenezwa na kusambazwa vijiji.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imeendelea kutoa mchango wake muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, kwa kuongeza ajira na mapato kwa Wananchi wa kawaida. Maendeleo ya sekta hii ni muhimu hasa kwa vile pamoja na kuongeza ajira, inasaidia kutoa msingi wa ujuzi na uzoefu kwa wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo ambao unaweza kuwajenga kuwa wafanyabiashara wakubwa hapo baadae. Katika kuiandaa sekta hii, Serikali iliendelea kuliimarisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*), ili liweze kuandaa mazingira mazuri na kutekeleza majukumu ya kuwasaidia wajasiriamali wadogo na kati kwa lengo la kuwawezesha kufanya shughuli zao kwa ufahamu zaidi na kuongeza tija ya miradi yao. Sera ya Maendeleo ya Viwanda na Biashara Ndogo ya mwaka 2003, imetoa mwanga mzuri kwa kubainisha maeneo muhimu ambayo Serikali itawawezesha walengwa kuimarisha utendaji wao na kuongeza mchango wao katika Pato la Taifa. Utekelezaji wa azma hiyo unaendelea kuimarika hatua kwa hatua; kuimarika huko kutaliwezesha Shirika kutoa huduma kwa ufanisi na kasi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2004, *SIDO* imeendelea kutoa huduma kwa walengwa katika nyanja mbalimbali kama vile teknolojia na ufundi, mafunzo kwa wafanyabiashara, ushauri, masoko, maeneo ya kufanya biashara, fedha na upashaji wa habari. Huduma za kuendeleza teknolojia na ufundi ziliendelea kutolewa kwa kufanya utafiti wa awali ili kuweza kubainisha mahitaji halisi ya kiufundi ya wanaviwanda na wafanyabiashara. Shirika limeimarisha mawasiliano na mahusiano kupitia mtandao wa wadau wanaoshughulikia utoaji wa huduma za teknolojia kama vile *CAMARTEC*, *TIRDO*, *TEMDO*, *TDTC*, *COSTECH* na *TATC* kwa kuweka mikakati ya utekelezaji ya pamoja katika kutafuta, kutengeneza, kuendeleza na kueneza matumizi ya teknolojia kulingana na mahitaji ya sehemu mbalimbali nchini. Kupitia ushirikiano huu, teknolojia tofauti zaidi ya 80 zilibuniwa na matumizi yake kuhamasishwa kwa wajasiriamali kwa kutumia njia ya maonesho, tovuti na vyombo vya habari. Ushirikiano wa kuendeleza na kusambaza teknolojia hizi ni kama ifuatavyo:-

(a) *SIDO* na *TEMDO* wanashirikiana kusambaza teknolojia ya kusindika mawese katika mkoa wa Kigoma na Wilaya za Ulanga na Kyela;

(b) *SIDO* na *COSTECH* wanashirikiana kusambaza tehnolojia ya majiko bora yanayotumia mkaa kidogo. Usambazaji wa teknolojia hii umeanza kwa kuwafundisha mafundi wadogo kwenye Mikoa ya Singida na Dodoma;

(c) *SIDO* na *TIRDO* wanashirikiana kuboresha uzalishaji wa chumvi kwa wazalishaji wadogo na kuwaelimisha namna ya uwekaji madini joto pamoja na ufungashaji mzuri. Utafiti umefanyika katika Mkoa wa Singida; na

(d) *SIDO* na *STAMICO* wanashirikiana katika kuboresha sekta ya wachimbaji wadogo na tayari utafiti umekamilika katika mikoa ya Singida, Dodoma na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza ubunifu wa wajasiriamali, Shirika limetekeleza mradi wa kuwainua wajasiriamali wenye mawazo mapya ya ubunifu. Mradi huu ambao unaitwa Kiatamizi (*Incubator*) umeanzishwa kwa kuanzia katika Mkoa wa Dar es Salaam. Hadi sasa wajasiriamali wanne wameanza kuendeleza ubunifu wao katika miradi ifuatayo:-

(a) Kutengeneza aina ya lishe kutokana na tunda la ubuyu, lishe hiyo inategemewa kuwa na uwezo wa kusaidia mwili kupambana na maradhi;

(b) Mradi wa kutengeneza maziwa kwa kuongeza asali na matunda kwenye *Yogurt*;

(c) Mradi wa kutengeneza Kiatamizi (*Incubator*) inayotumia gesi ya samadi kwa ajili ya matumizi vijiji; na

(d) Mradi wa matumizi mbadala ya zao la mhogo kwa kutengeneza mikate, keki na biskuti.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mafunzo ya ujuzi kwa vijana, Chuo cha Bidhaa za Mianzi kimeanzishwa Mkoani Dar es Salaam na kina wanafunzi wapatao 20, ambao wanajifunza kutengeneza na kuzalisha bidhaa za mianzi. Bidhaa wanazozalisha zimeanza kuingia kwenye soko na zina ubora unaoweza kushindana na bidhaa za aina hiyo kutoka nje. Aidha, elimu ilitolewa kuhusu ubanguaji wa korosho na matumizi ya mashine za kurahisisha kazi hiyo. Vikundi vya wanawake na vijana vilinufaika katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Tanga na Ruvuma. Katika kipindi hicho, jumla ya mashine 284 zimetengenezwa na kuuzwa kwenye maeneo hayo. Ili kuhakikisha teknolojia hii inasambazwa ipasavyo, Shirika limetumia wataalamu wake kuendesha mafunzo ya utumiaji mashine hizi katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Pwani na Tanga. Mahitaji ya mashine hizi yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku. Shirika pia liliendeleza teknolojia ya ukamuaji mafuta ya mawese, alizeti na karanga. Mashine za kukamulia mafuta ziliweza pia kubuniwa, kutengenezwa na kufanyiwa majaribio. Mashine 24 zilitengenezwa katika vituo vya kuendeleza teknolojia vilivyoko Arusha na Mbeya na kuuzwa katika mikoa ya Kigoma na Shinyanga. Aidha, Shirika limeendelea kusambaza teknolojia za usindikaji vyakula, utengenezaji chaki, useketaji wa nguo, utengenezaji uyoga, usagishaji nafaka mbalimbali, ufyatuaji matofali yenyе gharama nafuu pamoja na mashine za kukamua miwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki mashine 1,950 za aina mbalimbali zimetengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali mbalimbali ambao walizitumia kuanzisha miradi ya uzalishaji mali. Mashine hizo ni za kukoboa na kusaga nafaka, kupukuchua mahindi, kutengenezea chaki, kukamua miwa, kupura mtama, kusaga karanga, kukamua mawese, kupasua mbao na magogo na kubangua korosho. Mashine hizi zimetumika kuanzishia miradi ya uzalishaji mali vijiji hasa usindikaji wa mazao.

Kuhusu nyanja ya mafundi wadogo vijijini, mafundi waliendelea kuhudumia kwa kuwapatia mafunzo, zana za kufanya kazi, kuwatafutia masoko ya bidhaa zao na kuwajengea umoja ili waweze kufaidika kwa pamoja na kusaidiana wao kwa wao. Katika eneo hili, *SIDO* inashirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kuboresha kazi na huduma zao. Mafundi hao ni wahanzi, fundi seremala, mafundi vyerehani, wachomeleaji wa chuma na mafundi bomba. Shirika lisilo la Kiserikali lililopo nchini Uingereza liitwalo “*Tools for Self Reliance (TFSR)*” linasaidia programu hii kwa kuleta vitendea kazi kwa vikundi vya mafundi wadogo (*Artisans*) bure isipokuwa wanachangia gharama ya usafirishaji hadi mahali walipo. Toka mwaka 1995 hadi 2004 vifaa vya kufanya kazi vimepokelewa na kusambazwa kwa vikundi vipatavyo 1,554 vyenye wastani wa watu wanne kila kikundi. Ajira mpya iliweza kupatikana kwa watu 10,878. Huduma za viwanda vidogo zimeweza kuwafikia wanavijiji kulingana na mahitaji ya eneo husika. Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi Septemba, 2004, jumla ya miradi mipy 195 ya uzalishaji imeweza kuanzishwa vijijini. Miradi hiyo inahusu utengenezaji sabuni, mashine za kusaga, utengenezaji wa juisi, utengenezaji chaki, useremala, ukamuaji mafuta na useketaji mianzi.

Mheshimiwa Spika, katika kujenga na kuimarisha misingi ya wafanyabiashara mahiri, *SIDO* inaendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali. Mafunzo hayo hulenga kutoa ufahamu wa mazingira ya uzalishaji ama biashara, utayarishaji mipango ya biashara, uwekaji kumbukumbu, ukadiriaji bei, uongozi, utafutaji masoko na usindikaji wa vyakula. Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005 jumla ya kozi 863 zilizoshirikisha wajasiriamali 17,084 ziliandaliwa na kuendeshwa na wakati huo huo kozi 150 maalumu ziliendeshwa kwa ajili ya kutoa ujuzi wa usindikaji wa vyakula na kuhusisha wajasiriamali 2,666. Mafunzo huandaliwa kutoa elimu ya nadharia na vitendo kuendana na mahitaji halisi na mazingira ya walengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za ushauri, Shirika lilitoa huduma za ushauri wa aina mbalimbali kwa jumla ya miradi ya kibiashara 26,610. Walio wengi walihitaji kujua namna au taratibu nzuri za kuanzisha miradi, aina ya teknolojia inayofaa, taratibu za kupata leseni, utafutaji wa masoko na uendeshaji wa miradi ya kibiashara. Ingawa ushauri hutegemea zaidi mwelekeo wa mahitaji halisi ya wajasiriamali, lakini Shirika limeandaa miongozo ya kuzingatiwa ili kulinda viwango vya ushauri unaotolewa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba bidhaa zilizozalishwa zinapata masoko, *SIDO* imekuwa ikiandaa maonyesho ya bidhaa za wazalishaji wadogo kwa kanda mbalimbali. Katika kipindi hiki, *SIDO* iliandaa na kuendesa maonyesho katika Kanda za Magharibi na Kati (Kigoma na Tabora), Kanda ya Ziwa (Mwanza na Mara), Kanda ya Mashariki (Morogoro, Dar es Salaam na Pwani) na Kanda ya Kusini (Lindi). Pia, imewezesha wajasiriamali kushiriki maonesho mengine ya *EOTF, Afro-Arab* na ya *EOTF/NSSF*. Maonesho yote kwa pamoja yaliwawezesha wajasiriamali 2,481 kushiriki kikamilifu katika maonesho hayo. Matokeo yake walifanya mauzo ya bidhaa ya Shilingi 184.1 milioni fedha taslimu na Shilingi 379.9 milioni kwa miadi. Pia, katika kipindi hicho, Shirika liliwezesha wajasiriamali 56 kushiriki maonesho ya Nairobi, Kisumu na

Kampala ambapo walifanya mauzo ya Shilingi 14.5 milioni fedha taslimu na Shilingi 5.0 milioni kwa miadi.

Vilevile, katika juhudini za kuwaandalia mazingira mazuri ya kufanya kazi za viwanda vidogo na biashara ndogo, *SIDO* imeendelea kuwasiliana na Serikali za Mitaa katika mikoa yote ili kukubaliana kutambua umuhimu wa kutenga maeneo na kuhakikisha yanatumiwa kwa shughuli za viwanda vidogo na biashara ndogo. Katika hili tunapenda kukiri kupata ushirikiano na mwitikio mzuri kutoka halmashauri za miji na wilaya zote. Hadi sasa jumla ya maeneo 93 yametengwa na kufanyiwa tathmini na maandalizi ya awali ya kuyaendeleza. Katika kipindi hicho *SIDO* imeendelea kuratibu ujenzi wa soko la Songea mjini, pamoja na soko la wafanyabiashara wadogo la Mchikichini katika Manispaa ya Ilala. Ujenzi wa maeneo haya yote umekamilika kwa awamu kama ilivyopangwa na Serikali ilichangia jumla ya Shilingi 454 milioni. Ujenzi wa soko la Kawe pia unaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* iliendelea na utaratibu wa kuwawezesha wajasiriamali kupata mitaji ya kuanzisha na kuendeleza biashara zao kupitia mifuko mbalimbali ifuatayo: Mfuko wa Mitaji ya Mkoa (*Regional Revolving Fund*), Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wafanyabiashara Wadogo (NEDF), mifuko ya fedha kutoka mashirika mengine kama vile *Small Enterprises Loan Fund (SELF)*, *Tanzania Gatsby Trust Fund (TGTF)* na *National Income Generation Programme (NIGP)*. Katika kipindi cha mwaka 1995 hadi Septemba, 2004, *SIDO* imetua mitaji kwa jumla ya wajasiriamali 21,400 yenye thamani ya Shilingi 10,158 milioni kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza miradi ya aina mbalimbali. Mitaji hiyo imewezesha kuanzisha au na kudumisha ajira zipatazo 60,686.

Mheshimiwa Spika, Serikali mwaka 1994 ilianzisha mfuko wa kuwasaidia wafanyabiashara wadogo kupata mitaji ya kuanzishia au kuendeleza biashara zao kwa masharti nafuu. Hadi kufikia mwezi Septemba 2004, mfuko ulikuwa umetua mitaji kwa jumla ya wahitaji 18,527 yenye thamani ya Shilingi 6,435 milioni kwa ajili ya kuendeleza biashara mbalimbali. Mchango huo uliwezesha upatikanaji wa ajira kwa wananchi 28,340. Bado mahitaji ya mitaji kwa wafanyabiashara wadogo ni makubwa ikilinganishwa na uwezo wa kuwasaidia. Jumla ya maombi ya mitaji yaliyopokelewa hadi kufikia Septemba 2004 ni 77,678 yenye kuhitaji jumla ya Shilingi 29,735 milioni. Mitaji iliyotolewa ni asilimia 24 kwa idadi na asilimia 22 kwa thamani ya jumla ya maombi yote yaliyopokelewa katika kipindi hicho.

Kwa upande wa upashaji habari, hatua za awali za kuanzisha kituo cha habari *SIDO* Makao Makuu zimechukuliwa. Tovuti ya *SIDO* (www.sido.go.tz) na mtandao katika ofisi za Makao Makuu vimetengenezwa na juhudini za kuziunganisha ofisi za mikoa kwenye mtandao zinaendeleza. Nia ya kuanzisha kituo hiki ni kutengeneza mahali na utaratibu mzuri wa kukusanya, kuhifadhi na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo wakati wowote kwa matumizi ya ndani ya Shirika na kwa ajili ya wahitaji wengine nje ya Shirika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ufanikishaji wa malengo ya kuendeleza Sekta ya Viwanda katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, unadhihirishwa na takwimu za

uzalishaji zilizopo. Katika kipindi hicho uzalishaji wa nguo uliongezeka kutoka mita mraba 31.201 milioni mwaka 1995 hadi mita mraba 110.899 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 255.4. Uzalishaji wa saruji uliongezeka kutoka tani 739,000 mwaka 1995 hadi tani 1,281,000 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 73.3. Uzalishaji wa chuma uliongezeka kutoka tani 2,518 mwaka 1995 hadi tani 39,556 mwaka 2004 sawa na ongezeko la asilimia 1,470.9. Uzalishaji wa unga wa ngano uliongezeka kutoka tani 11,612 mwaka 1995 hadi tani 333,548 mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 2,772.4. Uzalishaji wa bia uliongezeka kutoka lita 89,301 milioni mwaka 1995 hadi lita 202,180 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 126.4. Uzalishaji wa sigara uliongezeka kutoka sigara 3,699 milioni mwaka 1995 hadi 4,220 milioni mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 14.1. Viwanda vya bia na sigara vinatoa mchango mkubwa katika mapato ya Serikali kwa njia ya kodi.

Mheshimiwa Spika, kuimarika kwa viwanda na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa kumechangia ukuaji wa sekta kutoka asilimia 1.6 mwaka 1995 hadi asilimia 8.6 mwaka 2004. Aidha, mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 8.2 mwaka 1995 hadi asilimia 8.6 mwaka 2004. Kutokana na kuzorota kwa ufanisi katika viwanda miaka ya themanini na mwanzoni mwa miaka ya tisini, ajira viwandani ilipungua kutoka wafanyakazi 126,052 mwaka 1995 hadi wafanyakazi 61,492 mwaka 2000. Hata hivyo, kutokana na zoezi la ubinafsishaji wa mashirika ya umma, kuanzia mwaka 2001 ajira viwandani imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka na kufikia wafanyakazi 68,045 mwaka 2004. Kwa upande wa uwekezaji, thamani ya miradi ya viwanda iliyopitishwa na Kituo cha Uwekezaji (*TIC*), iliongezeka kutoka Shilingi 71.5 bilioni mwaka 1995 hadi Shilingi 239.6 bilioni mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi mwaka 2003, Tanzania haikuwa na sera mahsusini ya biashara yenye mwelekeo wa kukuza mauzo nje na kuhimili ushindani. Hata hivyo, katika kipindi hicho, Serikali ilikuwa ikichukua hatua mbalimbali za kurekebisha mfumo wa uendeshaji biashara uliokuwepo. Hatua hizo zilihusu ulegezaji wa masharti ya biashara, kwa mfano, ulegezaji wa uingizaji wa bidhaa, usimamizi wa fedha za kigeni na kuondoa mfumo wa kupanga bei.

Mheshimiwa Spika, kama sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya 2025, Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Biashara ambayo ilizinduliwa rasmi mwezi Agosti, 2003. Lengo kubwa la Sera ya Biashara ni kujenga uwezo wa sekta binafsi, asasi na taasisi za umma katika ushindani wa biashara. Aidha, sera hii inabainisha pia nyenzo zitakazotumika katika kupanua na kukuza biashara kwa kuzingatia misingi ya kuongeza tija na ushindani katika sekta za uzalishaji mali pamoja na utoaji huduma.

Utekelezaji wa Sera ya Biashara umeanza kwa kuendesha warsha za kikanda ili kuhamasisha Wananchi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Hatua zingine ni pamoja na kubuni na kutekeleza programu mbalimbali zikiwemo kuanzisha mafunzo maalumu ya kiwango cha Shahada ya Uzamili katika fani ya Uendeshaji wa Biashara ya Kimataifa (*International Trade*) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kuimarisha Ubalozi wa Tanzania ulioko Geneva na Kituo cha Biashara cha London; kubainisha na

kuendeleza mikakati itakayowezesha wazalishaji nchini kupanya katika masoko ya nje pamoja na mbinu za kusaidia sekta binafsi katika kuinua tija na ubora wa uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika juhudzi za kukuza mauzo nje, kumekuwepo na programu za makusudi za kuiwezesha nchi yetu kunufaika na mfumo wa utandawazi chini ya *WTO*. Programu ya kwanza ni ya kukuza uwezo wa kuuza bidhaa nje chini ya *Integrated Framework for Trade Development*. Programu hii imewezesha kuanzishwa kwa mradi wa kuweka Mazingira Wezeshaji ya Kuendeleza Biashara (*Business Environment Strengthening for Tanzania - BEST*). Mradi wa *BEST* unaoteklezwa na Serikali unahu maeneo matano yafuatayo:-

- (a) Kuanzisha kitengo cha kuchambua sheria na kanuni mbalimbali zinazogusa biashara;
- (b) Kuanzisha Mahakama ya Biashara ili kuwezesha kesi za kibiashara kuamuliwa haraka;
- (c) Kuweka mfumo mbadala wa kutoa ufumbuzi wa mashauri ya kibiashara;
- (d) Kubadilisha mtazamo na utendaji wa watumishi wa umma; na
- (e) Kuendeleza sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Programu ya Pili inayoitwa *Joint Integrated Technical Assistance Programme (JITAP)*, inaisaidia Tanzania katika maeneo makuu matatu yafuatayo:-

- (a) Kujenga na kuimarisha uwezo wa Tanzania katika kuelewa masuala ya majadiliano ya biashara ya Kimataifa;
- (b) Kujenga uwezo wa asasi zinazohusika na biashara ya Kimataifa; na
- (c) Kujenga uwezo wa ushindani wa bidhaa zetu katika biashara ya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, ili kujenga mazingira ya kuwezesha nchi yetu kushiriki kikamilifu katika biashara ya Kimataifa, kikanda na ushirikiano baina ya nchi na nchi, Tanzania ni nchi mwanachama inayoshiriki kikamilifu katika *WTO*, *SADC* na *EAC*. Aidha, Serikali imewawezesha wafanyabiashara nchini kushiriki katika maonyesho mbalimbali kitaifa na kimataifa ili waweze kujenga uwezo wao wa kupanya soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuendelea kujenga mazingira ya ushindani wa haki katika soko la dunia, Tanzania ilipata heshima ya kuandaa mkutano wa Mawaziri wa Biashara kutoka nchi maskini, ambapo lilitolewa Tamko la Zanzibar lenye mchango mkubwa katika kuimarisha hoja za kuendeleza maslahi ya nchi maskini katika biashara za kimataifa. Mafanikio ya Mkutano wa Zanzibar yaliweka misingi ya mkutano wa Pili wa Mawaziri wa Biashara wa nchi za *LDCs* uliofanyika Dhaka, Bangladesh, Julai, 2003, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya mkutano wa *WTO* wa Mawaziri wa Biashara uliofanyika Cancun, Mexico, mwezi Septemba 2003. Kutowana na nguvu zilizojengwa na umoja na mshikamano wa nchi za *LDCs* kule Zanzibar, makundi mengine kama kundi la nchi za Afrika na kundi la nchi za *ACP* yaliungana na kundi la nchi za *LDCs* na kuwa *G90* na kutoa msimamo wa pamoja katika mkutano huo wa Cancun mwezi Septemba, 2003. Nguvu hii ndiyo iliwezesha nchi zinazoendelea kuzuia upitishaji wa *agenda* ambazo zingeendeleza na kuimarisha maslahi ya nchi zilizoendelea dhidi ya nchi zinazoendelea na hivyo kuendeleza hali yao ya kuwa pembezoni mwa biashara ya kimataifa (*marginalisation*). Kazi ya kushawishi, kuandaa na kufanikisha Mkutano huo wa Zanzibar umeiletea Tanzania heshima kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika ushirikiano wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), Tanzania ilikuwa na jukumu la kuratibu ushirikiano katika sekta ya Viwanda na Biashara hadi mwaka 2001 wakati mfumo wa uendeshaji shughuli za *SADC* ulipobadilishwa na Idara zote kuhamishiwa kwenye Sekretarieti yake Gabarone, Botswana. Tanzania pia kama Mratibu ilisimamia kikamilifu maandalizi ya Mkataba wa Biashara wa *SADC* (*SADC Trade Protocol*) uliotiwa saini mwaka 1996.

Mkataba huo umewezesha kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la nchi wanachama wa *SADC* na kuzinduliwa rasmi tarehe 1 Septemba, 2000. Vilevile, katika kipindi husika Tanzania iliongoza maandalizi ya sera na mkakati wa maendeleo ya sekta ya viwanda kwa nchi za *SADC*. Kutowana na ushirikiano huo, biashara baina ya nchi za *SADC* imeongezeka toka asilimia tano kabla ya ushirikiano huo hadi kufikia asilimia ishirini na tano ya biashara baina ya nchi hizi na nchi zingine duniani mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulioanzishwa upya kwa kusaini Mkataba wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano wa Nchi *Tatu* (*Permanent Tripartite Commission Agreement*) tarehe 30 Novemba, 1993, uliwezesha kuanzishwa kwa Mkataba wa Jumuiya Novemba, 1999. Mkataba huo umewezesha kubuni Mkakati wa Maendeleo ya Viwanda wa Afrika Mashariki (*EAC Industrial Development Strategy*) na Mfumo wa Biashara (*Trade Regime*), ambao umewezesha kufikia makubaliano ya kuanzisha Umoja wa Forodha (*EAC Customs Union*) ulioanza kutekelezwa tarehe 1 Januari, 2005.

Ushirikiano wa Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki utaondoa vikwazo vya kibiashara viliyyokuwepo awali na hivyo kuwezesha biashara huru baina ya nchi wanachama. Taratibu za kibiashara katika Umoja wa Forodha wa Afrika Mashariki zinahusisha masuala mbalimbali yakiwemo kuondoa vikwazo vya ushuru wa forodha na visivyo vya ushuru wa forodha (*Tariffs and Non-Tariff Barriers to Trade*), vigezo vya

uasili wa bidhaa (*Rules of Origin*) na kuweka wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha kwa bidhaa zitokazo nje ya Jumuiya (*Common External Tariff*).

Mheshimiwa Spika, wigo huo wa pamoja una viwango vitatu kama ifuatavyo:-

(a) Asilimia sifuri kwa bidhaa ambazo ni malighafi, mashine, mitambo, vitendea kazi vya sekta ya kilimo na bidhaa muhimu katika sekta za elimu na kijamii;

(b) Asilimia kumi kwa bidhaa za kiwango cha kati (*intermediate goods*), yaani bidhaa ambazo zimepitia hatua fulani ya matengenezo lakini haijafikia mwisho; na

(c) Asilimia ishirini na tanokwa bidhaa za walaji (*Finished Goods*).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza masharti ya biashara katika nchi wanachama, taratibu zifuatazo zitafuatwa:-

(a) Bidhaa zote zinazotoka Tanzania kwenda Uganda na zinazotoka Uganda kuja Tanzania hazitatozwa ushuru;

(b) Bidhaa kutoka Tanzania na Uganda kwenda Kenya hazitatozwa ushuru;

(c) Baadhi ya bidhaa kutoka Kenya kuja Tanzania na kwenda Uganda zinatozwa ushuru ambaa utakuwa unapunguzwa kila mwaka hadi kufikia sifuri katika kipindi cha miaka mitano kuanzia tarehe 1 Januari, 2005; na

(d) Bidhaa muhimu (*Sensitive Products*) kwa uchumi wa nchi, zitastahili kulindwa dhidi ya ushindani wa nje na hivyo bidhaa hizo zitatozwa ushuru mkubwa kuliko kiwango cha juu cha asilimia 25 ili kuendelea kulinda viwanda vyetu vichanga.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza na kupanua wigo wa biashara baina ya Tanzania na nchi mbalimbali, katika kipindi cha mwaka 1995 hadi 2005, Wizara ya Viwanda na Biashara ikishirikiana na taasisi za Serikali na sekta binafsi hasa za kiuchumi, imetilia mkazo katika kufufua mikataba ya tume za ushirikiano (*Joint Commissions*), ambayo ilikuwa imesimama, kufanya mikutano ya Kimataifa ya kuitangaza Tanzania nchi za nje na kutiliana saini mikataba ya kibiashara na nchi nyingine. Mikataba ya Tume za Ushirikiano ambayo imefufuliwa upya ni baina ya Tanzania na India, Cuba na Namibia. Mikataba ya biashara ambayo imesainiwa ni baina ya Tanzania na nchi za Rwanda, Uturuki na Vietnam. Aidha, mikataba ya biashara na Mauritius, Comoro, Zimbabwe na Misri, imefikia katika hatua ya mwisho ya kutiliana saini. Kutohakana na juhudi hizo, nchi yetu imefanikiwa kuwapata wawekezaji kutoka nchi mbalimbali ambaa wamewekeza katika sekta za viwanda, biashara na sekta nyingine za uchumi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Awamu ya Tatu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Wizara iliendelea kurekebisha na kuweka wazi zaidi taratibu za kupata leseni ya biashara kwa lengo la kuhamasisha uanzishaji wa biashara nyingi zaidi na papo hapo kupunguza gharama za kuanzisha biashara na hivyo kuvutia wawekezaji na kuziba mianya ya rushwa. Sheria Na.25 ya Leseni za Biashara ya 1972, inategemewa kufutwa

na badala yake kuitisha sheria mpya ijulikanayo kama *Business Activities Registration Act, 2005*. Sheria hii inakusudia kurahisisha taratibu za uanzishwaji wa biashara nchini kwa kusajili biashara kwa masharti nafuu. Aidha, biashara zinazotakiwa kutekeleza masharti ya usalama wa nchi, afya ya wanadamu, mimea na wanyama, pamoja na masharti ya mazingira zitatakiwa kutimiza masharti hayo kabla ya kuandikishwa. Biashara zisizohusika na masharti kama hayo zitaandikishwa bila masharti mengine yoyote.

Hata hivyo, kabla sheria hii mpya haijapitishwa Serikali ilikwishafanya mabadiliko kadhaa ya kumpa unafuu mfanyakibashara hasa mdogo kwa kuondoa ulipaji wa ada ya leseni kwa biashara ambayo mzunguko wake haufikii Shilingi 20 milioni kwa mwaka, na ada ya Shilingi 20,000 kwa biashara ambayo mzunguko wake ni Shilingi 20 milioni na zaidi. Hayo pia yalikuwa ni mabadiliko makubwa hasa ikizingatiwa kuwa ada hizo zilikuwa kwa kiwango kuanzia Shilingi 5,000 hadi 20 milioni kwa mwaka. Pia, leseni za udhibiti (*Regulatory Licences*) zilitolewa bila kutozwa ada na Wizara baada ya wahusika kulipa ada kwa vyombo vinavyohusika na udhibiti wa biashara husika. Katika mabadiliko haya, leseni inayotolewa ni kwa kipindi chote cha uhai wa biashara husika. Mikakati hii itaendelea kutekelezwa kwa upeo mkubwa zaidi hapo Sheria mpya ya uandikishaji wa Biashara itakapoanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuleta ufanisi katika shughuli za Serikali, wakala mbili zilianzishwa chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Wakala hao ni *Business Registrations and Licensing Agency (BRELA)* na Wakala wa Mizani na Vipimo (*WMA*). BRELA iliendelea na majukumu yake ya usajili wa makampuni, leseni za viwanda na shughuli za kusimamia sheria za makampuni, majina ya biashara, alama za biashara, hatazo na sheria ya leseni ya viwanda. BRELA baada ya kuzinduliwa kwake mwaka 1999, iliangalia upya taratibu mbalimbali zilizokuwa zinatumika katika kutoa huduma zake na kugundua kuwa kulikuwepo na taratibu zisizokuwa za kisheria na zilizokuwa zinazuka tu kiholela katika kusimamia utekelezaji wa sheria ambazo Wakala inazisimamia. Baada ya kuondoa taratibu zilizokuwa sio za kisheria huduma mbalimbali za BRELA zilianza kupatikana kwa urahisi.

Usajili wa kampuni kwa mfano, ulikuwa hauna muda maalum ambapo mwombaji angeweza kusajiliwa kampuni yake. Baada ya mabadiliko huduma hiyo sasa inapatikana kati ya siku tatu na tano tu kutoka maombi yanapopokelewa. Vivyo hivyo, kwa majina ya biashara, sasa huduma hiyo hupatikana kati ya siku moja hadi tatu toka maombi yanapopokelewa. Aidha, BRELA ilichukua mikakati mbalimbali ya kutoa elimu kwa wananchi na kuwahuisha kwa njia mbalimbali ili wawe washiriki katika kuweka mipango ya kuboresha huduma wanayopata kutoka BRELA.

Kuanzia mwaka 2000 hadi 2005, Wakala huu ulisajili makampuni 15,999 na majina ya biashara 26,507. Kuhusu hatazo, alama za biashara na alama za huduma zinazotakiwa kulindwa kisheria hapa nchini yapo maombi ya aina tatu: maombi yanayopitia katika shirika la kimataifa la *World Intellectual Property Organisation (WIPO)*, Shirika la *African Regional Intellectual Property Organisation (ARIPO)* na maombi ya hapa nchini. Aidha, katika kipindi hicho, maombi ya hatazo 873

yalipokelewa na Wakala kupitia *WIPO*, 4,054 kupitia *ARIPO* na maombi 90 kutoka hapa nchini. Kuhusu alama za biashara na za huduma kulikuwa na maombi 6,269 ya ndani ya nchi, 4,336 kati ya hayo yalisajiliwa na mengine 95 yalisajiliwa kupitia *ARIPO*.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Vipimo unaendelea na jukumu lake la kuhakikisha haki na usawa katika biashara na sehemu nyingine ambazo matumizi ya vipimo ni muhimu katika kuboresha maisha ya binadamu, kufanya ukaguzi ili kuhakikisha kwamba vipimo vyote vinavyotumika katika biashara ni sahihi kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo Na. 20 ya mwaka 1982, pamoja na kanuni za sheria hiyo. Kazi hizi hufanywa na Maafisa Vipimo ambao wamepata elimu na utaalamu kutoka Chuo cha Elimu ya Biashara Dar es Salaam na Vyuo/Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi. Mpaka hivi sasa tunazo ofisi za vipimo katika Mikoa yote 24 Tanzania Bara. Hii inajumuisha Wilaya nne: Kibaha, Ilala, Temeke na Kinondoni ambazo zimepewa hadhi ya Kimkoa kiutendaji sawa na mikoa mingine. Pamoja na majukumu hayo, Wakala huu unalo jukumu la kusimamia na kueneza matumizi ya Vipimo vya Metriki katika sekta zote za uzalishaji, maendeleo ya huduma mbalimbali za jamii na kutoa elimu na ushauri wa namna bora ya matumizi ya vipimo vya metriki.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kwenda sambamba na maendeleo ya teknolojia ya vipimo pamoja na kuleta uwiano wa vipimo duniani, Tanzania ni mwanachama hai wa Shirika la Kimataifa la Vipimo vinavyotumika katika nyanja zote (*The International Organization of Legal Metrology - OIML*), ambalo Makao Makuu yake yako Paris, Ufaransa. Shirika hili kwa namna moja au nyingine linasaidia kuleta uwiano wa taratibu na sheria zinazotawala vipimo duniani.

Mheshimiwa Spika, Wakala umeendelea kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kuhakikisha kuwepo kwa haki na usawa katika biashara kwa lengo zima la kumlinda mnunuzi/mlaji (*Consumer Protection*) na muuzaji. Ili kufanikisha haki na usawa, Wakala unahakikisha kuwa mnunuzi amepata kiasi cha bidhaa alicholipia na kwa upande mwingine muuzaji katoa bidhaa kulingana na kiasi cha fedha alizolipwa;

(b) Kuwaelimisha wananchi na taasisi mbalimbali kuhusu haki zao na matumizi bora ya Vipimo. Jukumu hili linatekelezwa kwa njia ya matangazo katika vyombo vya habari, kama vile luninga, redio na magazeti. Vile vile, Wakala umeshiriki katika maonyesho ya biashara, kama vile Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ya mwaka 2005;

(c) Kuhakikisha usahihi na matumizi bora ya Vipimo katika maeneo mengine muhimu katika maisha ya mwananchi mbali na biashara kama vile afya, usalama na utunzaji wa mazingira yake anamoishi;

(d) Kuwachukulia hatua za kisheria wale wote wanaokiuka Sheria na taratibu za matumizi sahihi ya vipimo. Ofisi za vipimo ni kitovu (*Focal Point*) cha kupokea malalamiko ya kibiashara;

- (e) Kutoa ushauri kuhusu masuala yote yanayohusu vipimo; na
- (f) Kutoa mapendekezo kuhusu sheria mpya na marekebisho ya sheria za zamani ili kukidhi na kuzingatia mabadiliko katika mfumo wa sasa wa biashara, uchumi pamoja na ugunduzi katika nyanja za Sayansi na Teknolojia zinazofanyika sehemu mbalimbali duniani.

Mheshimiwa Spika, ili kukuza na kulinda haki za watanzi, waigizaji, wanamuziki, watengenezaji wa kanda na vituo vya utangazaji, kimeanzishwa Chama chaHakimiliki Tanzania (*Copyright Society of Tanzania - COSOTA*). Chama hiki, ambacho ni asasi isiyo ya kibiashara na ya pekee ya kisheria iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 46 cha Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999, kilanza rasmi shughuli zake tarehe 24 Oktoba, 2001. Hadi kufikia Juni 15, 2005, Chama kilisajili jumla ya wanachama 784 ikijumuisha wanamuziki 475, waigizaji 69, watanzi 93, wachapishaji 13 na vikundi vya sanaa 134. Hadi tarehe hiyo jumla ya kazi 4,113 zilisajiliwa zikijumuisha kazi 3,756 za muziki, maigizo 98 na kazi za maandishi 259.

Mheshimiwa Spika, *COSOTA* Kimataifa ni mwanachama Na. 223 wa Muungano wa Kimataifa wa Vyama vya Waandishi na Watunzi (*International Confederation of Societies of Authors and Composers - CISAC*) kuanzia tarehe 15 Desemba, 2002. Uanachama huu umeiwezesha *COSOTA* kuingia mikataba ya kuwakilishana kazi na vyama 11 vya nchi za nje vinavyohusika na Hakimiliki na Hakishiriki. Vyama hivyo ni: *Music Copyright Society of Kenya (MCSK)* cha Kenya, *Uganda Performing Rights Society (UPRS)* cha Uganda, *Copyright Society of Malawi (COSOMA)* cha Malawi, *Societe Nationale Editeurs Compositeurs et Autior (SONECA)* cha Jamhuri ya Congo, *Zambia Music Copyright Protection Society (ZAMCOPS)* cha Zambia, *Zimbabwe Music Reprographic Rights Association (ZIMRA)* cha Zimbabwe, *South African Reprographic Rights Association (SAMRO)* cha Afrika ya Kusini, *Copyright Organisation of Trinidad and Tobago (COTT)* cha Trinidad na Tobago, *American Mechanical Rights Association (AMRA)* cha Marekani, *Mozambican Authors Society (SOMAS)* cha Msumbiji na *Uruguayan Authors Society (AGADU)* cha Uruguay. *COSOTA* imetuma mapendekezo ya Mikataba ya aina hiyo kwa *Copy Rights Society of Ghana (COSGA)* cha Ghana, *Performing Rights Society (PRS)* cha Uingereza na nchi nyingine.

Aidha, *COSOTA* katika kipindi cha mwaka 2004/2005, iliendesha semina za uhamasishaji katika mikoa saba ambayo ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Mtwara na Morogoro. Chama hiki kimetafsiri Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na. 7 ya mwaka 1999 katika lugha ya Kiswahili. Chama kimeandaa Kanuni za kutoa leseni za kutumia na kutangaza kazi za hakimiliki kibiashara (*Copyright Licensing of Public Performances and Broadcasting Regulations*) za mwaka 2003, ambazo zimeanza kutumika. Kanuni za kupiga vita uharamia wa Hakimiliki (*Copyright and Neighbouring Rights, Production and Distribution of Sound and Audio Visual Recordings Regulations*) za mwaka 2005 na kanuni za kusajili wanachama na kazi zao

(Copyright and Neighbouring Rights, Registration of Members and Their Works) Regulations za mwaka 2005 zinakaribia kukamilika ili zichapishwe katika Gazeti la Serikali. Tangu Aprili, 2004 hadi Juni, 2005, COSOTA imekusanya jumla ya Shilingi 5,688,000 za Mirabaha (Royalties) kutoka kwa watumiaji wa kazi za muziki kibashara katika mahoteli na nyumba za burudani.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na azma yake ya kuimarisha mwenendo wa uchumi wa soko ili kuweka misingi ya kuendesha biashara ya haki na usawa na kuwapa watu wote fursa ya kushiriki katika shughuli za uchumi wa Taifa letu. Serikali ilitunga Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003, ambayo iliifuta sheria ya ushindani ya mwaka 1994 ili kuendana na wakati na kukidhi matakwa ya kimataifa juu ya sheria za ushindani. Serikali iliteua timu ndogo ya wataalamu kujifunza na kuanzisha utekelezaji wa Sheria hii ili kuwa na muda wa kujenga utaalamu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha tangu 1995, Ofisi ya Kamishna wa Tume ya Ushindani, iliweza kufanya maamuzi mbalimbali baada ya kupitia upya Sheria ya awali ya Biashara ya Haki na Kuifanyia marekebisho stahiki. Maandalizi yako kwenye hatua ya uteuzi wa wajumbe wa Tume ya Ushindani na kuunda Baraza lake pamoja na Baraza la Ushauri la Walaji. Aidha, kazi ya kuunda chombo cha ushauri cha watumiaji/wadau imekamilika kwa kuzingatia Sheria ya Ushindani ya mwaka 2003. Chombo hiki kimetengewa muda wa miaka mitatu ili kijijengee uwezo wa utendaji. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Wizara itatangaza na kuhamasisha zaidi shughuli za Tume ya Ushindani na Baraza la Ushindani pamoja na Baraza la Ushauri la Walaji ili wafanyabiashara na watumiaji/wadau wa bidhaa na huduma mbalimbali waweze kuelewa maudhui yake na jinsi wanavyoweza kulindwa na kufaidika na Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka kumi iliyopita, Halmashauri ya Biashara ya Nje iliendelea kutekeleza malengo yake ya kukuza mauzo na kuongeza Pato la Taifa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuishauri jumuiya ya wafanyabiashara kuhusu biashara ya Kimataifa; kutoa habari za kibashara kama vile bei za bidhaa kwenye soko la nje; masharti ya uuzaji; kupanga, kuratibu na kusimamia ushiriki wa Tanzania kwenye maonyesho ya biashara ndani na nje ya nchi yetu. Ili kufanikisha malengo yake, Halmashauri ya Biashara ya Nje ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

(a) Kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Biashara (*International Trade Centre - ITC*) Geneva, chini ya mpango wa JITAP, Halmashauri iliandaa mikakati ya kukuza mauzo ya nje kwa baadhi ya bidhaa ambazo Tanzania ina uwezo wa kuzizalisha. Bidhaa hizo ni ngozi iliyosindikwa na bidhaa zake, mboga, matunda na uyoga, samaki na bidhaa zake, viungo, nguo na vitambaa;

(b) Kuongeza ushiriki wa Tanzania kwenye maonyesho ya kimataifa kwa lengo la kuzitangaza bidhaa za Tanzania. Kwa kipindi hiki cha miaka kumi, Tanzania ilishiriki zaidi ya maonesho 60 katika nchi mbalimbali. Aidha, Tanzania ilishiriki kwenye maonesho maalumu ya EXPO yafuatayo: EXPO 98 Kigali, EXPO 98 Lisbon, EXPO 99 China, EXPO 2000 Hanover (Ujeruman), EXPO 2003 Ujeruman na mwaka huu AICHI EXPO 2005 nchini Japan. Tanzania ilitumia maonyesho yote haya

kuzitangaza bidhaa na utamaduni wake pamoja na kukuza mahusiano na nchi wenyeji wa maonyesho;

(c) Halmashauri ya Biashara ya Nje ilitoa mafunzo mbalimbali kwa wafanyabiashara wadogo (*SMEs*) ili kuwapa mbinu mbali mbali za kuuza bidhaa nje ya nchi. Zaidi ya Makampuni madogo 30 yalinufaika na mafunzo hayo ambayo yaliendeshwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuendeleza Biashara ya Kimataifa (*Centre for International Business Development Services - CIBDS*) na kuhisaniwa na *INWENT* ya Ujerumani;

(d) Vilevile, Halmashauri ya Biashara ya Nje kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi kwa kupitia taasisi yake ya kuendeleza uagizaji wa bidhaa kutoka nchi zinazoendelea (*Centre for the Promotion of Imports from Developing Countries - CBI*) imetoa mafunzo kwa wakufunzi ambaa baada ya kufuzu watatoa mafunzo kwa wauzaji bidhaa nje ya nchi. Mpango huu ulianza mwaka 2004 na utaendelea hadi 2007 ukiwa na lengo la kupata wataalamu 30 watakaotoa mafunzo kwa wafanyabiashara 3,000. Mpango huu unaotekelawa kwa pamoja katika nchi za Afrika Mashariki, mafunzo yalitolewa na yanaendelea kutolewa kwa Waambata wa Biashara katika Balozi zetu ili waweze kuziwakilisha nchi zetu vyema. Waambata wa Biashara 10 wa Tanzania wameshapata mafunzo. Lengo ni kuwapa mafunzo Waambata 30;

(e) Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (*Dar es Salaam International Trade Fair*), yameendelea kuboreshwa na kuwa na sura ya kimataifa zaidi. Baada ya kutimiza viwango vya Kimataifa maonesho haya yalisajiliwa na kuwa mwanachama namba 164 wa Umoja wa Maonesho ya Biashara ya Kimataifa (*Union of International Trade Fairs - UFI*) mnamo mwezi Oktoba 1996;

(f) Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliboreshw na kuongeza idadi ya ushiriki wa makampuni ya ndani na nje. Kwa mwaka 1997 makampuni ya ndani yaliyoshiriki yalikaribia 584 na kuongezeka hadi kufikia 1,780 mwaka 2004. Makampuni ya nje pia yaliongezeku kutoka 156 hadi 365 kwa kipindi hicho. Vile vile, kulikuwa na ongezeko la ushiriki wa nchi za kigeni kutoka 19 hadi 28 katika kipindi hicho. Aidha, maonyesho yamekuwa chachu kwa ushiriki wa vikundi vya wanawake kupitia Mfuko wa Udhmini wa Fursa Sawa kwa Wote (*EOTF*) unaoongozwa na Mheshimiwa Mama Anna Mkapa. Washiriki kutoka mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar wametumia fursa hii kuongeza ubora wa bidhaa zao pamoja na kuzitangaza; na

(g) Kuhusu kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania, bidhaa na masoko yafuatayo yalihusika kikamilifu: madini ya vito katika masoko ya Thailand, Japan na Hong Kong, mbaa na bidhaa zake katika nchi za Oman, Abu Dhabi na Sharjah, samaki wa chakula katika masoko ya nchi za China, Japan, Hong Kong na Ureno, asali na nta katika soko la nchi za Ulaya, mboga na matunda katika nchi za Ulaya, Abu Dhabi, Sharjah na Dubai na samaki wa mapambo katika soko la nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ilipata heshima ya kuandaa maonyesho ya Sita ya Biashara yanayozijumuisha Nchi za Kiafrika na Kiarabu (*Afro Arab Trade Fair*),

yanayoandaliwa kila baada ya miaka miwili kati ya nchi wanachama. Maonesho hayo ya Sita yalifanyika kwa mara ya kwanza Desemba, 2003 nchini Tanzania kwa ufanisi mkubwa na kuliletea sifa kubwa Taifa letu. Serikali iliipa Halmashauri ya Biashara ya Nje jukumu la kuratibu maonyesho hayo, kazi ambayo Halmashauri ilifanya kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki Halmashauri ya Biashara ya Nje ilifanikiwa kujenga na kuhamia kwenye ofisi zake zilizoko kwenye uwanja wa Mwalimu Julius K. Nyerere na kuondokana na adha ya kupanga. Aidha, Shirika limeweza kurejesha huduma na vifaa vyake hasa baada ya kupata ajali ya moto katika jengo la *NASACO* la zamani. Shirika lilijenga ukumbi mpya wa kisasa wa maonyesho wenyewe ukubwa wa mita za mraba 2,600. Ukumbi huu umeongeza ubora wa uwanja na chanzo cha mapato kwa Shirika. Kadhalika Shirika lilibadili jina la Uwanja wa Maonesho na kuitwa *Mwalimu J. K. Nyerere Trade Fair Grounds*, kwa ajili ya kumuenzi Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Shirika pia lilibadili jina la Ukumbi wa *PTA* na kuwa Ukumbi wa Sheikh Abeid Amani Karume, kwa kumuenzi Hayati Sheikh Abeid Aman Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Vile vile, *BET* kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Biashara *ITC*, chini ya mpango wa *JITAP*, ilitayarisha vitabu viwili vya kutoa maelekezo muhimu kwa wafanyabiashara vikijumuisha *How to Approach Banks* na *Trade Secrets*. Vitabu hivi vinatoa maelezo ya kina ya namna ya kufanya biashara na namna ya kuwasiliana na vyombo vya fedha kwa ajili ya biashara.

Mheshimiwa Spika, *BET* imefanikiwa kuwakutanisha wafanyabiashara na wanunuzi katika mazungumzo ya kibiashara. Makampuni mbalimbali yanayozalisha bidhaa za dharura kama vile, mahema, mablanketi, magodoro, vyombo vya ndani, vyandarua na chakula kwa ajili ya wakimbizi au waathirika wa mafuriko, yalikutanishwa na taasisi za kimataifa kama vile *UNICEF*, *FAO* na *World Food Programme*, ambazo hununua bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Lengo la mkutano huo ni kutangaza makampuni ya Tanzania kwenye mashirika hayo ili yaweze kununua bidhaa hizo hapa nchini badala ya kuziagiza kutoka nje.

Katika kipindi hicho, Serikali ya Canada iliandaa mpango maalumu wa kukuza mauzo yetu nchini Canada na kupunguza pengo la biashara kati ya Tanzania na Canada. Kwa kuanzia bidhaa za sanaa za mkono za Tanzania zilipewa kipaumbele. Ujumbe wa Serikali ya Canada uliitembelea Tanzania ili kujiona wenye hali ya bidhaa hizi ili maandalizi ya msafara wa wanunuzi kutoka Canada uandaliwe. Shirika liliteliwa kuwa mratibu wa mpango huu. Aidha, chini ya mpango huo wa *PACT*, mafunzo ya kusanifu na kutengeneza vifungashio (*Packing Materials*), yalitolewa kwa makampuni yanayotengeneza vifungashio hivyo, lengo likiwa ni kuwapa mbinu bora za kuzalisha vifungashio vyenye hadhi ya Kimataifa. Vilevile, mafunzo ya kuongeza ubora wa bidhaa za mboga, matunda na viungo yalitolewa Tanzania Bara na Zanzibar na wataalamu wa biashara chini ya Kituo cha Biashara cha Kimataifa, Geneva, Uswisi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi iliongezeka kutoka Dola za Kimarekani 682.9 milioni mwaka 1995 hadi 1,334.90 milioni mwaka 2004. Sekta ya Biashara ilikua kutoka asilimia 3.1 mwaka 1995 hadi asilimia 8.0 mwaka 2004. Aidha, mchango wa Sekta ya Biashara kwa Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 15.7 mwaka 1995 hadi asilimia 17.0 mwaka 2004.

Mafanikio Makubwa Katika Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2000, katika Sekta ya Viwanda, Wizara ilielekezwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 kutekeleza mambo yafuatayo:-

- (a) Ufufuaji wa viwanda vilivyopo nchini hassa vya nguo, ngozi, kanvasi, usindikaji wa mazao ya kilimo, kufufua na kuimarisha miundombinu na kadhalika;
- (b) Usindikaji wa mazao ya kilimo, mbao na madawa kwa kuwakaribisha wawekezaji wazalendo na wa kutoka nje;
- (c) Kufufua na kuimarisha viwanda na miundombinu;
- (d) Kuimarisha viwanda na miundombinu ya utengenezaji wa vifaa na mitambo ya chuma kwa kushirikisha wawekezaji;
- (e) Kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji wa makaa ya mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga kwa lengo la kuipatia nchi yetu msingi wa viwanda mama (*Basic Industry*);
- (f) Kubuni mpango wa kuwaandaa mabingwa katika fani mbalimbali za sayansi na teknolojia ya viwanda humu nchini na ng'ambo; na
- (g) Kutoa kipaumbele kwa kuweka mtandao bora wa vituo vya taasisi za utafiti nchini pamoja na kuviwezesha kuyafikisha matokeo ya utafiti kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM katika Sekta ya Viwanda, yamekuwa na mafanikio makubwa. Viwanda na mashirika yaliyobinafsishwa mengi yalipata wawekezaji makini, walioweza kufanya ukarabati wa mitambo na majengo au kuagiza na kusimika mitambo mipya; mambo haya yameweza kufufuliwa kwa viwanda vingi. Viwanda hivyo ni pamoja na vya nguo, vinywaji, saruji na chuma. Aidha, viwanda vipyta vya *Trishala Rolling Mill* na *Hans Nail Manufacturers* vya Arusha, *Sita Steel Rolling Mill*, *Steel Master*, *Simba Steel Rolling* na *Dar Steel Mill* vyote vya Dar es Salaam vimeanzishwa. Viwanda hivi vimeanzishwa ikiwa ni matokeo ya uamuzi wa Serikali wa kuzuia uuzaji nje wa chuma chakavu, jambo ambalo liliviwezesha viwanda hivyo kupata malighafi ya kutosha.

Viwanda vya nguo vilivyofufuliwa ni pamoja na kiwanda cha *Namera Group Ltd.* kilichokuwa *Sunguratex* cha Dar es Salaam, *New Kilimanjaro Textile* kilichokuwa *Kiltex* kilichoko Arusha, *New Mwatex* iliyokuwa *Mwatex* na *New Mutex* kilichokuwa *Mutex* cha Musoma. Viwanda vingine vilivyobinafsishwa na ambavyo vilifanyiwa ukarabati wa mitambo na majengo ni pamoja na Kiwanda cha Karatasi cha Mgololo ambacho sasa

kinajulikana kama *Mufindi Paper Mills Ltd*, *Morogoro Polyester*, ambacho kwa sasa kinaitwa *21st Century Textile Mills*, *Tabora Textile*, *Tegry Plastic*, *Tanzania Pharmaceutical Industries*, Arusha na Kiwanda cha Zana za Kilimo cha *UFI*, Ubungo, Dar es Salaam, ambacho kimepata mwekezaji mpya atakayetengeneza mabomba hasa kwa ajili ya mradi wa maji wa Ziwa Victoria, Kahama na Shinyanga. Vingine ni viwanda vya usindikaji vyakula, vinywaji, vifaa vya ujenzi na vya chuma. Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu na hivyo kuvutia wawekezaji kuanzisha viwanda vipyta mbalimbali vikiwemo vya usindikaji wa mazao ya kilimo, mbao na madawa. Kwa mfano, vimeanzishwa viwanda vya kusindika matunda, usagishaji wa nafaka, mbao na samani na viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula. Aidha, mafunzo ya usindikaji wa vyakula na mboga yaliendelea kutolewa kwenye mikoa yote.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Maendeleo ya Taifa (*NDC*), limepewa jukumu la kuendeleza Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma kwa ajili ya kuzalisha umeme na Mradi wa Chuma cha Liganga. Kuhusu uwekezaji katika Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga, Mkataba wa uwekezaji kati ya *NDC* na Kampuni ya *Siemens* ulitiwa saini mwezi Julai 2001 ili kufanya upembuzi yakinifu wa miradi husika. Kutokana na upembuzi huo, Shirika la *NDC* limeweza kuingiza miradi ya Makaa ya Mawe na Chuma cha Liganga katika mpango wa *NEPAD*. Aidha, *NDC* ni chombo muhimu katika kuendeleza shughuli za Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara na ule wa Kati. Mradi wa Barabara ya Mtwara - Songea - *Mbamba Bay* umefikia hatua ya usanifu.

Katika kutekeleza agizo la Ilani ya Uchaguzi la kuliimarisha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (*SIDO*), Serikali katika kipindi hiki cha mwaka 2000 hadi 2005 ilitoa Shilingi bilioni moja kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi, yakiwemo magari na kompyuta. Fedha hizo zilitumika kununua magari 21 ambayo yalipelekwa kwenye ofisi za mikoa ili kuimarisha shughuli za Shirika. Aidha, kompyuta 30 zilinunuliwa kwa ajili ya kuboresha shughuli za Shirika. Hatua hizi zimeipa nguvu *SIDO* kuweza kufikisha huduma zake kwa walengwa wengi zaidi na kwa ufanisi ikijumuisha utoaji wa mafunzo kwa wajasiriamali 14,345 katika nyanja mbalimbali za ujuzi wa kuzalisha bidhaa zinazohitajika katika masoko ya hapa nchini na yale ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa *National Entrepreneurship Development Fund (NEDF)*, ulioanzishwa na Serikali umeendelea kusimamiwa na *SIDO* kwa kutoa mikopo kwa Wananchi ili kuwawezesha kuanzisha shughuli za kiuchumi na hivyo kuongeza kipato chao katika juhudhi za kuondoa umaskini wa kipato na kuinua ubora wa maisha. Katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2005 jumla ya mikopo iliyoolewa na *SIDO* ilikuwa yenye thamani ya Shilingi bilioni 4 kwa wajasiriamali 10,871 kutoka katika mikoa mbalimbali. Katika mikopo hiyo, wajasiriamali Wanawake 5,236 walipata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 ikiwa ni asilimia 48 ya mikopo yote iliyoolewa. Aidha, mchanganuo wa mgawanyo wa mikopo hiyo kisekta ulikuwa kwa wajasiriamali 7,618 wa Sekta ya Biashara, 844 wa Sekta ya Viwanda na wengine 1,330 wa Sekta za Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Spika, Katika Sekta ya Biashara, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ilielekeza yafuatayo:-

- (a) Kuhimiza Serikali kuimarisha upatikanaji wa bidhaa nyingi na bora kutoka sekta za ndani na nje ya nchi yetu kwa lengo la kukidhi mahitaji ya Wananchi wetu;
- (b) Kuimarisha mwenendo wa soko la ndani ili kuwepo na uendeshaji wa biashara ya haki na usawa;
- (c) Kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa nyingi na bora;
- (d) Kuzuia nchi yetu kugeuzwa dampo la bidhaa hafifu/duni kutoka nje;
- (e) Kuendelea kuimarisha ushirikiano wa kimataifa wa nchi za Afrika Mashariki na nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuwavutia wawekezaji; na
- (f) Kuhimiza Serikali zake kuendelea kukamilisha mipango ya uanzishwaji wa Maeneo Maalumu ya Kuzalisha Bidhaa za Kuza Nje (*EPZ*) ili utekelezaji wake uanze katika kipindi hiki cha Ilani.

Mheshimiwa Spika, nimeshaelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu kuhusu Sera ya Taifa ya Biashara ilioanzishwa mwaka 2003. Lengo la sera hiyo ni kujenga uwezo wa ushindani katika biashara kwa kuzingatia misingi ya kuongeza tija katika sekta za uzalishaji mali na utoaji huduma. Mahitaji ya bidhaa kwa Taifa yametimizwa kwa kuhimiza uzalishaji bidhaa nyingi na bora nchini na pia kuagiza kutoka nje ili kuziba pengo. Vile vile, Bunge lako limehuisha Sheria ya *Merchandise Marks Act Cap 519* ya mwaka 1963 ili kukabiliana na uingizaji na usambazaji wa bidhaa hafifu nchini (*counterfeit*). Sheria hii tayari imeshatangazwa katika gazeti la Serikali na itaanza kutumika hivi karibuni. Nimeamua Tume ya Ushindani ndiyo taasisi mwafaka ya usimamizi na utekelezaji wa Sheria hii na wakaguzi wa bidhaa duni/hafifu watateuliwa hivi karibuni kama hatua madhubuti ya kulikabili tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokwishesem, Serikali imefanya marekebisho makubwa katika mfumo wa utoaji wa leseni za biashara ili kuweka mazingira wezeshaji kwa biashara kuanzishwa na kukua. Aidha, muswada wa sheria mpya ya kuandikisha biashara umeandaliwa kwa lengo la kuondoa kero kwa wafanyabiashara pamoja na kuwezesha sekta isiyo rasmi kuingia katika sekta rasmi. Natumaini Bunge hili litaupitisha Muswada huu ili kukamilisha mageuzi haya katika mfumo wa utoaji leseni za biashara nchini.

Mheshimiwa Spika, Ushiriki wa Tanzania umeimarishwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC*) na Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), kwa lengo la kupanua soko la bidhaa zetu na kuwavutia wawekezaji. Mbinu mojawapo ya utekelezaji wa malengo haya ni pamoja na kuandaa mazingira na kuwawezesha kuza bidhaa nje zenye viwango vinavyokubalika kimataifa. Mafanikio yaliyopatikana ni

pamoja na marekebisho ya Sheria ya Vipimo namba 20 ya 1982 ili kuendana na mikataba inayohusu vipimo katika *SADC* na *EAC*. Aidha, katika *SADC* chini ya *SADC Cooperation in Legal metrology (SADCMEL)*, sheria za vipimo zimehuishwa kulingana na sheria za Shirika la Vipimo Duniani katika maeneo ya bidhaa zilizofungashwa viwandani, uhakiki wa vipimo na mikakati ya utekelezaji. Vilevile, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, vigezo vya Vituo Bora (*Centres of Excellence*), mathalani vile vya Chuo cha Biashara (*CBE*), zimewasilishwa katika kikao cha Baraza la Mawaziri la *EAC*.

Mkataba wa uanzishaji wa Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ulioanza kutumika tarehe 1 Januari, 2005 umekwishardhiwa na Bunge letu. Kwa upande wa mafanikio katika uanzishaji wa Mkakati Maalum wa Uzalishaji kwa Mauzo Nje (*EPZ*), kama nilivyokwisha yaeleza hapo awali, tunaendelea kujifunza kutokana na uzoefu tuliofata katika miaka ya mwanzo tangu tuanze utekelezaji wake. Aidha, Serikali inaendelea kujizatiti kwa kufanya marekebisho ya Sheria yenyewe ya *EPZ* ili kuondoa utata kwa lengo la kuimarisha utekelezaji wake pamoja na kufanikisha miundombinu ya *EPZ* ili mkakati huo uendelee kuwavutia wawekezaji zaidi.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2004/2005, katika Sekta ya Viwanda kwa mwaka 2004/2005, mkazo uliwekwa katika kuendelea kuhamasisha uwekezaji kwenye sekta za kipaumbele, yaani sekta ndogo za nguo, ngozi na usindikaji wa mazao ya kilimo na chakula. Mipango husika ni pamoja na:-

- (a) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ndogo ya ngozi na viwanda vya ngozi kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo;
- (b) Kuendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Viwanda Awamu ya Pili (*Integrated Industrial Development Programme-Phase II*), kwa kushirikiana na *UNIDO*, inayolenga katika kuimarisha usindikaji wa mazao ya kilimo na chakula;
- (c) Kuendelea na zoezi la ukusanyaji wa takwimu za viwanda kuwezesha uanzishwaji wa Benki Mahsusni ya Takwimu ya Sekta (*Sectoral Data Bank*);
- (d) Kutekeleza maamuzi yatakayofikiwa na Serikali baada ya kupokea taarifa za sekta ndogo ya viwanda vya mkonge na hali ya biashara ya chuma chakavu;
- (e) Kufuutilia utayarishaji wa sheria mpya za Taasisi za Huduma za Viwanda (*Industrial Support Organisations - ISO*), kama itabidi ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao mapya ya utafiti na maendeleo na uzalishaji kibashara (*Commercialisation*);
- (f) Kufuutilia uwekezaji katika Maeneo ya ukanda za Maendeleo (*Development Corridors*), hususan wa Mtware na wa Kati ikiwa ni pamoja na miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga;

(g) Kuendelea kuhamasisha uanzishwaji wa maeneo ya *EPZ* na uwekezaji ndani ya maeneo hayo;

(h) Kuendelea kutekeleza Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ya mwaka 2003; na

(i) Kufanya utafiti katika maeneo mengine yenyewe matatizo yanayokwamisha maendeleo ya viwanda kwa kushirikiana na wadau husika.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali, wakati nilipokuwa natoa taarifa ya mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000, utekelezaji wa malengo kadhaa ulifanikiwa kwa viwango vikubwa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Utekelezaji wa malengo yanayohusu Awamu ya Pili ya Mpango wa Kuendeleza Viwanda (*Integrated Industrial Development Programme-Phase II*);

(b) Kufuutilia uwekezaji katika maeneo ya *Mtwara Corridor*;

(c) Makaa ya Mawe na Chuma cha Liganga; na

(d) Uendelezaji wa *EPZ* na utekelezaji wa Sera ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

Utekelezaji wa mkakati wa kuimarisha sekta ndogo ya ngozi na viwanda vya ngozi, ulienda kwa kasi ndogo kutokana na kusubiri kukamilika kwa utaratibu wa uandaaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Ngozi (*Leather Development Fund*), ambayo yamo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Spika, tathmini kuhusu biashara ya chuma chakavu ilifanyika kama ilivyotarajiwa. Madhumuni ya tathmini ni kuiwezesha Serikali kuandaa utaratibu wa kudumu kuhusu matumizi ya chuma chakavu. Utafiti umekamilika na Serikali ikaamua kwamba, iandaliwe sera itakayosaidia kuwepo kwa utaratibu wa kudumu wa biashara ya chuma chakavu. Aidha, tathmini hiyo imewezesha kufahamika kiwango cha uzalishaji, kiasi kilichopo, mahitaji ya ndani kwa sasa na baadaye, na takwimu za mwenendo wa mauzo ya chuma chakavu nje.

Vilevile, Wizara ilitumia wataalamu washauri wa *TISCO* kufanya tathmini ya sekta ya viwanda vya mkonge hususan viwanda vya magunia ili kujua sababu za sekta hii kukosa maendeleo ya kuridhisha katika uzalishaji na soko la magunia ya mkonge. Majadiliano yanaendelea na wadau kwa lengo la kubainisha matatizo ya viwanda vyenye na yale ya kisera ili kukubaliana juu ya ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, katika mwaka 2004/2005 taasisi za utafiti na huduma zinazosaidia katika maendeleo ya viwanda ziliendelea na shughuli za utafiti kwa lengo la kuboresha uzalishaji viwandani na katika sekta nyingine za uchumi. Taasisi hizo ni *TIRDO*, *TEMDO* na *CAMARTEC*. Taasisi hizi kwa pamoja

zimechangia katika maendeleo ya viwanda kwa kubuni teknolojia za kusaidia ama katika upatikanaji wa malighafi kwa viwanda au kuwezesha wananchi kupata teknolojia zinazohitajika katika uanzishaji wa viwanda, hususan viwanda vidogo. Mashirika ya NDC, SIDO na TBS halikadhalika yaliendelea kutoa huduma muhimu zinazohitajika katika uendelezaji wa viwanda nchini ikiwa ni pamoja na kutafuta wabia watakaoshirikiana na Watanzania katika uwekezaji kwenye miradi mikubwa (*Mtvara Corridor and Central Corridor*); kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vidogo na kuweka viwango kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, CAMARTEC imeendelea kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kubuni na kuandaa zana za kilimo na teknolojia zinazofaa kwa wakulima vijijini, kufanya majoribio ya zana za kilimo na kutoa ushauri wa kitaalamu, kusambaza teknolojia husika kwa walengwa na kuhamasisha wajasiriamali mbalimbali kwa kuwapa mafunzo ya kutengeneza na kueneza teknolojia. Katika kipindi hicho, CAMARTEC ilitilia mkazo katika utafiti, uundaji na uenezi wa teknolojia ya zana za kilimo na nishati mbadala. Kituo kiliunda sampuli mbalimbali za teknolojia ambazo zimethibitishwa kutumika. Aidha, kituo kiliendelea kupokea mahitaji ya zana mbalimbali na kutengeneza zana husika.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2004 hadi 2005, TIRDO iliendelea kutoa mafunzo katika nyanja za uchomeaji vyuma, kuzalisha bidhaa bora za mbao, uzalishaji uyoga na kuwapa ushauri wajasiriamali wa namna ya kuboresha bidhaa za usindikaji. Mafunzo ya uchomeaji vyuma yamelenga kwenye kuunga chuma cha pua, alumina na chuma chepesi (*Mild Steel*). Kuhusu uyoga, Shirika limewatemebelea na kutoa ushauri wa kitaalamu wa kilimo cha uyoga kwa vikundi vilivyofundishwa, hususan katika mikoa ya Pwani, Arusha, Dar es Salaam na Iringa. Katika kipindi hiki watu 22 walifundishwa kulima uyoga, wakiwemo wanawake 14 kutoka Dar es Salaam na Pwani.

Aidha, Shirika limetilia mkazo usambazaji wa teknolojia ya ulimaji wa uyoga wenyewe viini vinavyowezesha kusaidia kinga ya mwili. Pia, Shirika limeendelea na utafiti wa utumiaji mwani kama vimeng'anya vyta kuzalishia uyoga kwa lengo la kuongeza madini joto ili kuondoa tatizo la tezi ya shingo (*goiter*) kwa walaji. Kwa upande wa usindikaji matunda, Kikundi cha Wanawake watano kutoka Kibaha mkoani Pwani walifundishwa usindikaji matunda na nyanya za kopo, wameanza kusindika kwa kutumia vifaa vyta Shirika. Kuhusu mradi wa utafiti unaochunguza sumu iitwayo *Ochratoxin A*, itokanayo na aina fulani za ukungu (*fungus*) kwenye mbegu za kahawa, Shirika limeweza kuchanganua aina ya bakiteria waliopo na kuangalia jinsi wanavyoweza kutumika kuzuia ukungu katika mbegu za kahawa (*Biocontrol Method*).

Mheshimiwa Spika, TIRDO pia wametoa mafunzo kwa wajasiriamali 15 wanaotengeneza chaki ili kuboresha uzalishaji. Aidha, Shirika limeanza kufanya utafiti wa namna ya ukaushaji mzuri wa chaki kwa kutumia nishati ya mionzi ya juu. Vilevile, Shirika limeendesa semina kwa wazalishaji wa bidhaa zinazouzwa nchi za nje, hususan samaki, kahawa, korosho na chai kwa madhumuni ya kuwaelimisha wahusika umuhimu wa kuweka kumbukumbu katika kila hatua ya uzalishaji, utengenezaji hadi usafirishaji ili kukidhi matakwa ya walaji huko mazao yanakokwenda. Mradi kwa sasa uko kwenye hatua ya ushirikishaji wadau wa mazao hayo katika kuandaa kumbukumbu pale ambapo

hazipo au kuziimarisha pale ambapo zilikuwepo lakini zina upungufu. Vile vile, Shirika limeanza mpango wa kuinua hadhi ya maabara zake ili ziweze kufanya utafiti na upimaji utakaotambuliwa Kimataifa (*Accreditation*).

Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea kupima na kutoa ushauri kwa wenye viwanda kuhusu uchafuzi wa mazingira unaotokana na ama moshi, vumbi au maji machafu yatokanayo na uzalishaji viwandani. Aidha, Shirika pia limepima na kutoa ushauri kwa wenye viwanda kuhusu athari za mingurumo ya mitambo (*Sound Levels*) kwa wafanyakazi. Makampuni zaidi ya matano yamepata huduma hizi. Shirika pia limeweza kutathmini matumizi ya nishati viwandani na kwenye majengo ya Serikali, hususan Wizara ya Fedha, Nishati na Madini, Elimu na Utamaduni na Wizara ya Ujenzi. Nia ni kupunguza matumizi ya nishati na kuongeza tija kwenye uzalishaji na utoaji huduma. Katika kutekeleza mradi wa kupima ubora wa vifaa vya chuma na zege bila kuviharibu, Shirika liliweza kupata msaada kutoka Shirika la Umoja wa Kimataifa linaloshughulikia nishati ya nyuklia (*International Atomic Energy Agency*) wa kuimarisha maabara ya uthibiti wa vyuma na vifaa vya ujenzi. Maabara hii imeweza kukagua matanki ya mafuta yapatayo 21 kwa kutumia *non destructive methods*.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa taka rejea (*Plastics and Paper Recycling*) ulizinduliwa rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Frederick Sumaye, tarehe 7 Aprili, 2005 na hivyo kuanza rasmi shughuli za uzungushaji taka rejea hasa za plastiki. Shirika kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hasa *UNIDO*, *SIDO* na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam, limeanza utaratibu wa ukusanyaji wa taka rejea mitaani na kuzipeleka kwenye mitambo kwa ajili ya uzungushaji. Mtambo huu una uwezo wa kurejeresta kiasi cha tani 50 za plastiki za aina mbalimbali kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* ilitoa mafunzo ya kuimarisha uwezo wa wajasiriamali kuzifanyia matengenezo mashine na mitambo ya viwanda vyao. Mafunzo yalitolewa kwa walengwa mbalimbali hasa katika maeneo ya uendeshaji na utunzaji wa mitambo inayoendeshwa kwa dizeli; ukamuaji na uchujaji wa mafuta ya kula; ubanguaji wa korosho na usindikaji wa vyakula kwa ujumla. Katika kuendeleza wahanzi, Shirika lilitoa mafunzo kwa wahanzi 412 kutoka mikoa 18 na kutoa zana za kufanyia kazi kwa vikundi 123 katika maeneo mbalimbali. Huduma za mafunzo na ushauri zilitolewa kwa wajasiriamali; ambapo jumla ya kozi 73 zilitolewa kwa ajili ya wawakilishi wa miradi ya uzalishaji na biashara 1,126.

Mheshimiwa Spika, Shirika kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa limeainisha na kuwezesha kutengwa maeneo mapya 92 kwa ajili ya matumizi ya viwanda na biashara ndogo. Aidha, ujenzi wa majengo ya wafanyabiashara wadogo yalijengwa maeneo ya Kawe (Kinondoni) na Rangi Tatu (Temeke). Kwa upande wa huduma za fedha Shirika lilitoa ushauri kwa wahitaji mbalimbali, kwa kuwaonyesha namna ya kuandaa miradi yao kwa lengo la kutimiza matakwa ya vyombo vya fedha. Aidha, Shirika liliendelea kusimamia mifuko ya mitaji iliyoko na kuhakikisha mitaji inatolewa na kutumika kwa ufanisi. Jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi 770.6 milioni ilitolewa kwa miradi 1,756 na kutoa ajira mpya kwa watu 5,268.

Mheshimiwa Spika, *SIDO* iliandaa na kuwawezesha wafanyabiashara kushiriki katika maonyesho ya bidhaa zao katika maeneo mbalimbali nchini. Shirika liliwezesha baadhi ya wajasiriamali kushiriki katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (*DITF*). Hii inawapa fursa ya kujefunza kutoka kwa wazalishaji wengine, kuwapa hali ya kujiamini na kujenga msingi wa kuendelea kufanya biashara. Jumla ya wajasiriamali 1,178 wa bidhaa na huduma mbalimbali walishiriki kutangaza bidhaa zao. Mauzo ya bidhaa mbalimbali zenyе thamani ya Shilingi 115.3 milioni yalifanyika na kupokea miadi (*commitment*) ya thamani ya Shilingi 228.5 milioni. Vilevile, *SIDO* ilihamasisha wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo kuanzisha vyama vyaya ushirika, ambapo jumla ya vyama 33 vilianzishwa na kupewa huduma kama vile kutayarisha Katiba, kuweka taratibu nzuri na zilizo rasmi za uongozi, taratibu za kuanzisha huduma za kuweka na kukopa na uendeshaji wa vyama hivyo. Huduma hizo zimesaidia kuongeza kasi ya uanzishaji wa miradi ya uzalishaji hasa viwanda vidogo vijijini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, matatizo ya miundombinu, hususan umeme, mafuta ya kuendeshea mitambo na gharama za usafirishaji kutokana na ongezeko kubwa la bei ya petroli ni mambo yaliyochangia katika kuathiri uzalishaji viwandani. Tatizo jingine ni mitaji midogo ya kufanya kazi kutokana na riba kubwa za mabenki, mitambo mibovu katika baadhi ya viwanda na miundombinu haffifu. Matatizo haya kwa ujumla yamechangia kwa kiasi kikubwa katika baadhi ya viwanda kushindwa kutumia uwezo wake kikamilifu na kuzalisha bidhaa kwa gharama kubwa na hivyo kushindwa kuhimili ushindani katika soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, hatua zimechukuliwa kuimarisha miundombinu hasa barabara, mawasiliano (simu, barua pepe na tovuti), urekebishaji wa mfumo wa kodi na ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na kuhimiza uzalishaji wa bidhaa bora katika viwanda vyetu. Katika kukabiliana na tatizo la gharama za umeme, viwanda vichache vimeanza kutumia gesi ya Songas. Tatizo la bei kubwa ya petroli bado ni kitendawili, halijapata ufumbuzi. Suala la nishati nafuu kwa matumizi ya viwanda kwa ujumla na hasa vile vyaya *EPZ*, lazima lipatiwe ufumbuzi wa haraka kama kweli tunataka kutekeleza dhamira ya kuifanya Sekta ya Viwanda kuwa Sekta Kiongozi katika mchango wake katika Pato la Taifa na upatikanaji wa ajira kwa kasi na uwingi unaotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, mikakati mbali mbali ilitekelezwa na Wizara katika sekta ya biashara iliyosaidia uchumi wetu kuweza kuhimili ushindani wa kimataifa pamoja na kunufaika kutokana na mfumo wa biashara ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na mikakati ya:-

(a) Kuendelea kutekeleza programu ya *Joint Integrated Technical Assistance (JITAP)* na programu ya *Integrated Framework (IF)*, kwa lengo la kujenga uwezo wa Taifa katika kushiriki kwa manufaa zaidi katika majadiliano yanayofanyika sasa na kuongeza uwezo wa ushindani wa bidhaa zetu katika soko la kimataifa;

(b) Kuendeleza ushirikiano na asasi za kimataifa hasa *WTO*, *ITC*, *UNCTAD* na *UNIDO* kwa lengo la kudumisha mafanikio yaliyopatikana katika *JITAP* na *IF* katika awamu ya kwanza ili kutufikisha katika hali ya kujitegemea;

- (c) Kushughulikia matatizo yanayosababisha tushindwe kunufaika na fursa za masoko ya nje, hususan upande wa vikwazo vya uzalishaji (*Supply Side Constraints*);
- (d) Kuendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003; na
- (e) Kushiriki katika vikao vya *SADC* na *EAC* kwa lengo la kuimarisha ushirikiano wa kiuchumi kikanda.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla karibu malengo yote ya mwaka jana yalitekelezwa katika viwango tofauti vya ufanisi kama nilivyoeleza hapo awali, nilipokuwa naeleeza mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tatu na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2000.

Mheshimiwa Spika, wakati nawasilisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2004/2005, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa tarehe 14 Aprili, 2004, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, alitia saini kuidhinisha Sheria Na. 374 ya mwaka 2004 ya *Anti-Dumping and Countervailing Measures*, ili ianze kutumika baada ya kupitishwa na kikao cha Bunge hili cha tarehe 9 Februari, 2004. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Sheria hiyo ilitangazwa rasmi kupitia Tangazo la Serikali Na. 354 la tarehe 17 Septemba, 2004. Wizara yangu, ikishirikiana na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba, imeandaa Rasimu ya Kanuni (*Anti-Dumping and Countervailing Measures Regulations*) ili kuiwezesha sheria kufanya kazi. Rasimu hiyo imepelekwa Geneva, Makao Makuu ya *WTO*, kwa ushauri wa kitaalamu ili kuhakikisha kuwa, utekelezaji wa Sheria hii na Kanuni zake, hazipingani na kanuni za shirika la *WTO*, ambazo zinahusu pia nchi yetu kama mwanachama.

Wizara inaendelea na taratibu za kujenga uwezo wa ndani wa kutekeleza Sheria hii. Taratibu hizo ni pamoja na kuunda Sekretarieti ya Kitaifa itakayohusika na uchunguzi wa awali kuhakiki usahihi na ushahidi wa misingi ya malalamiko ya bidhaa zinazouzwa chini ya bei ya kawaida (*Normal Value*), yaani *dumping* katika masoko yetu. Aidha, utaratibu unaandalowiwa wa kuipa Sekretarieti hiyo fursa ya kujifunza kutokana na uzoefu wa nchi zilizofanikiwa katika utekelezaji wa sheria kama hii.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Biashara cha London (*LTC*) kiliendelea kuelekeza juhudi zake katika kutangaza biashara, kuhamasisha uwekezaji, utalii na ushirikiano na kuhimiza diplomasia ya kiuchumi (*Economic Diplomacy*). Kituo kiliweza kuiwakilisha Tanzania katika mikutano mbalimbali, semina na warsha zilizoandalowiwa na Mashirika ya Kimataifa kama vile *Commonwealth Agricultural Bureaux International (CABI)* na *International Sugar Organisation (ISO)*, *International Coffee Organisation (ICO)*, *Commonwealth Business Council (CBC)*, *London Sisal Association (LSA)* na Mashirika mengine kama *British Tanzania Society*, *Tanzania UK Business Group* na *African Diaspora*. Aidha, Kituo kilipokea na kushughulikia maulizo kuhusu bidhaa mbalimbali zikiwemo nguo, samaki, kazi za mikono na madini. Katika kutangaza biashara, Kituo kimeweka tovuti yake ambayo itawezesha kutangaza taarifa mbalimbali za uwekezaji na biashara ili kuwafikia watu wengi kirahisi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Biashara ya Nje (*BET*), imeendeleza na kuboresha Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (*DITF*). Aidha, Halmashauri imeendelea kuhamasisha wafanyabiashara wa Tanzania kushiriki maonyesho ya biashara katika nchi mbalimbali. *BET* chini ya wahisani mbalimbali kama Canada kupitia Programu ya *PACT*, imeendesha mafunzo mbalimbali kwa wafanyabiashara wadogo kama vile njia bora za ufungashaji wa bidhaa katika sekta ndogo za *horticulture* na kadhalika, kwa ajili ya masoko ya nje. Pia, Shirika limeendesha mafunzo mbalimbali kuhusu ujuzi wa biashara na kuendeleza masoko na kutoa taarifa. Ili kuimarisha uwezo wa *BET*, Serikali inaifanya uchambuzi sheria iliyoanzisha *BET* kwa lengo la kutunga sheria mpya itakayoipa uwezo zaidi Halmashauri hiyo kukuza biashara ya nje kwa kuzingatia mazingira ya soko.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliari Bunge lako Tukufu kuwa, hatua za awali za kuichambua sheria hiyo zimekwishafanyika na taarifa ya kitaalamu itakayoelekeza mabadiliko hayo itatoka hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira, Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*), kinaandaa mkakati wa kupanua mitaala yake kwa kuongeza programu zaidi kama vile uanzishaji wa kozi za utalii, mafunzo ya kompyuta na hasa kuweka mtandao wa mawasiliano kwa kutumia teknolojia ya kompyuta. Chuo kimetoa mafunzo hayo kwa wakufunzi ili nao waweze kuendesha mafunzo hayo kwa walengwa. Mwaka 2004/2005, Chuo kilikuwa na wanafunzi 3,082, kati ya hao wanafunzi wa kike walikuwa 1,349 yaani sawa na asilimia 43.7 ya wanafunzi wote.

Pamoja na jitihada za Wizara kufanya vizuri katika nyanja za Kimataifa, bado kuna vikwazo vinavyozuia Tanzania kufanya vizuri zaidi. Kwa mfano, upungufu wa watumishi, ufinyu wa bajeti na uwezo mdogo wa kitaalamu katika Ubalozi wetu wa Geneva, ukilinganisha na majukumu yake makubwa ya kuratibu shughuli na mikutano mbalimbali ya biashara ya Kimataifa yanayohusu asasi 16 za Kimataifa zilizopo Geneva, matatizo mengine ni:-

- (a) Uwezo mdogo wa watendaji katika Serikali, asasi za umma na sekta binafsi katika kuilewa na kutoa majibu kwa masuala yanayotakiwa kushughulikiwa katika majadiliano;
- (b) Uchanga wa sekta binafsi unasababisha masuala yao kutojulikana na hivyo kutowakilishwa kikamilifu Serikalini hata pale Serikali inapo jitahidi kulinda maslahi yao katika majadiliano;
- (c) Uwezo mdogo wa asasi zinazosaidia kuendeleza biashara kama vile *TBS*, *BET* na *CBE*;
- (d) Uelewa mdogo wa jamii katika masuala ya matakwa ya soko la Kimataifa;

- (e) Sheria zetu za biashara hazijalenga kulinda maslahi na haki za walaji katika mfumo wa uchumi wa soko;
- (f) Ukosefu wa miundombinu ya kiuchumi (*Financial Services*), inayoweza kutoa mikopo ya fedha kwa riba nafuu na urasimu kidogo; na
- (g) Uelewa mdogo na hivyo kushindwa kuchangamkia fursa mbalimbali za upendeleo katika masoko na biashara, kama vile *EBA* ya Jumuiya ya Ulaya, *AGOA* ya Marekani, *PACT* ya Canada, *GSP* ya Japan na ile ya China.

Mheshimiwa Spika, Wizara iliendelea na zoezi la kuimarisha uwezo wake katika utendaji kazi kwa kuajiri wataalamu wa kada na ngazi mbalimbali kulingana na muundo ulioihinishwa. Katika kuimarisha ufanisi wa kazi wizarani, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imeendelea kuinua viwango vyta elimu kwa watumishi. Kwa kutumia mpango maalum wa *Performance Improvement Fund (PIF)*, mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na elimu ya majadiliano ya Kimataifa ya biashara hasa kuhusiana na mikataba ya biashara ya kimataifa na kikanda (*Trade Negotiation Skills*) na uwezo wa kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, matumizi ya kompyuta, uhasibu na utawala. Aidha, Wizara iliendesha warsha za utawala bora na vita dhidi ya rushwa na janga la UKIMWI kwa watumishi kwani ni tishio la nguvu kazi yetu na taifa kwa ujumla. Ili kukidhi mahitaji ya sera ya utumishi wa umma, Wizara imeweza kuwapeleka masomoni watumishi waliokwama kimuundo kwa kukosa sifa ili kuweza kuwakwamua hadi ifikapo 2007.

Mheshimiwa Spika, mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2005/2006, utazingatia maeneo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Mpango wa MKUKUTA umegawanywa katika mafungu makuu matatu; Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa Kipato; Kuboresha hali ya maisha na afya; na Utawala Bora.

Mpango huo unalenga kuwaongeza uwezo wanaviwanda na wafanyabiashara wadogo ushiriki wao katika juhudzi za kuongeza kipato na kukuza uchumi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha uanzishaji wa viwanda vidogo vijijini hasa vyta kusindika mazao ya kilimo na misitu. Aidha, msisitizo utawekwa katika kutoa huduma za kiufundi, kuendeleza ujasiriamali, masoko, mawasiliano na huduma za kifedha kwa ajili ya mitaji. Vilevile, Serikali imanzisha Mfuko wa Dhamana ambao unalenga kuwakwamua wazalishaji na wafanyabiashara wadogo kwa kuwaondolea kikwazo cha kukosa dhamana hasa mali zisizohamishika kutumika kama dhamana ya mikopo wanayoomba kutoka kwenye taasisi za fedha.

Mheshimiwa Spika, Wizara itashirikiana na taasisi zilizoko chini yake na zingine zinazojishughulisha na uendelezaji wa sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo katika kuwaendeleza wajasiriamali kwa lengo la kutekeleza programu ya MKUKUTA. Taasisi hizo ni pamoja na *SIDO*, *CAMARTEC*, *TEMDO*, *TIRDO*, *TBS*, *BET*, *CBE*, *NDC*, Kituo cha Ujasiriamali cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Asasi za Sekta Binafsi na *NGOs*. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana kwa karibu na wenye viwanda na biashara ili

kujuu matatizo yao na kuyatafutia ufumbuzi. Wizara pia, itaendelea kutekeleza na kubuni sera na mikakati ya kuendeleza Sekta za Viwanda na Biashara ili kudumisha mafanikio yaliopatikana kwa lengo la kukuza mchango wa sekta hizi katika maendeleo ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mazingira wezeshaji kwa wafanyabiashara, Wizara itachukua hatua zifuatazo kuhusiana na Sheria mpya ya uandikishaji wa biashara nchini:-

(a) Kuhamasisha wadau wote wanaohusika na utekelezaji wa Sheria hii ili waielewe. Wahusika watakuwa waheshimiwa madiwani, viongozi wa wilaya, viongozi wa mikoa na watendaji katika ngazi za wilaya na mikoa, pamoja na vyombo vya wafanyabiashara na wawakilishi wa sekta binafsi kama vile *TCCIA, CTI, TPSF* na *TNBC*;

(b) Kuanza utekelezaji wa uandikishaji wa biashara kwa taratibu zilizorahisishwa badala ya utaratibu wa zamani wa utoaji wa leseni za biashara;

(c) Kufuatilia uelewa wa Sheria mpya kwa kulinganisha hali ya utekelezaji na matakwa ya Sheria yenyewe; na

(d) Kufanya uchambuzi wa jinsi Sheria hiyo ilivyopokelewa na wadau mbalimbali, hususan wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuondoa kero katika Sekta ya Biashara, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na wadau wengine, inaendelea na zoezi la kuwianisha sheria mbalimbali za udhibiti wa biashara na kubainisha vikwazo kwa lengo la kurekebisha vikwazo hivyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika mwaka wa fedha 2005/2006, itaendelea kuwapatia mafunzo watumishi na kuweka mazingira mazuri ya kazi na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali kulingana na mahitaji ya muundo wa Wizara. Aidha, watumishi wanne wa Wizara na wengine toka Idara na Wizara nyingine za Serikali, Sekta Binafsi na Asasi nyingine, wapatao ishirini na moja, watapatiwa Mafunzo ya Shahada ya Uzamili wa Biashara ya Kimataifa kwa kushirikiana na *DANIDA*.

Vile vile, Wizara imeshakamilisha Mkataba wa huduma kwa wateja na unatarajiwa kuzinduliwa rasmi katika mwaka 2005/2006, kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Ukamilishaji wa zoezi la kuboresha utendaji kazi wa masjala ili kuimarisha mawasiliano ndani ya Wizara, unaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuzishukuru nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa, ambayo yamekuwa yakitoa misaada iliyioongezea uwezo Wizara wa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na tija zaidi. Napenda kuzishukuru nchi za Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Japan, Marekani, Sweden, Uhlanzi, Uingereza, Ujeruman na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara.

Aidha, napenda kuyashukuru mashirika ya *SIDA*, *UNIDO*, *DANIDA*, *DFID*, *GTZ*, *NORAD*, *WTO*, *UNCTAD*, *OECD*, *USAID*, *UNDP*, *OPEC Fund*, *JICA*, *WIPO*, *ARIPO* na *ITC*. Nazishukuru pia Taasisi za Kimataifa za Benki ya Dunia, Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) na *Commonwealth Fund for Technical Cooperation*, kwa misaada na michango yao ya fedha na utaalamu katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja hii ni matokeo ya kazi nzuri na ushirikiano wa karibu, nilioupata kutoka kwa wenzangu katika Wizara, mashirika, asasi, taasisi na makampuni yaliyo chini ya Wizara. Naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mbunge wa Kawe, Katibu Mkuu, Bwana Wilfred L. Nyachia na watumishi wote wa Wizara, Mashirika, Makampuni na Taasisi zilizo chini ya Wizara, kwa michango yao katika kufanikisha kazi za Wizara na kwa kuhusika kwa

namna moja au nyingine na maandalizi ya Bajeti ninayoiwasilisha leo. Nazishukuru pia Jumuiya na Taasisi za Sekta Binafsi, ikiwemo Jumuiya ya Wenye Viwanda (*CTI*), Jumuiya ya Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo (*TCCIA*) na *Tanzania Private Sector Foundation (TPSF)*.

Aidha, nazishukuru taasisi zinazoshughulikia utafiti, hasa Kituo cha Utafiti wa Masuala ya Uchumi na Jamii (*ESRF*), Idara ya Utafiti wa Uchumi (*ERB*) na Kitivo cha Biashara na Menejimenti cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na Chuo Kikuu cha Mzumbe, kwa michango yao ya mawazo wakati wa mikutano, warsha, semina na makongamano mbalimbali, kuhusu Sekta za Viwanda na Biashara hapa nchini. Ushirikiano huu ni muhimu katika kuendeleza na kuimarisha Sekta za Viwanda na Biashara kwa maendeleo ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2005/2006, Wizara inaomba Shilingi 1,626,000,000.00 kwa ajili ya shughuli za miradi ya maendeleo ya viwanda na biashara. Kati ya fedha hizi, Shilingi 300,000,000.00 ni fedha za ndani ambazo zitatumika katika shughuli za maendeleo katika taasisi zilizo chini ya Wizara na Shilingi 1,326,000,000.00 ni fedha za nje kutoka kwa wahisani ambazo zitatumika kulipia tafiti za kitaalamu na vifaa kwa miradi mbalimbali itakayotekelawa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo na majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika kipindi cha mwaka 2005/2006, ninaomba Shilingi 14,774,569,400.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizi, kiasi cha Shilingi 5,448,202,200.00 ni matumizi ya Wizara yenyewe yakijumuisha mishahara na matumizi mengine na Shilingi 9,326,367,200.00 ni ruzuku kwa ajili ya mishahara na shughuli za kuondoa umaskini zinazofanywa na mashirika ya umma yanayosimamiwa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali, ambayo yanatoa takwimu zitakazowawezesha Waheshimiwa Wabunge, kutafakari vizuri zaidi maendeleo na utendaji katika Sekta za Viwanda na Biashara. Ninaomba takwimu hizi zichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naafiki

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO - (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa mwaka 2005/2006, kwa mujibu wa Kanuni Namba 81 (1) ya kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, kabla sijafanya hivyo, naomba kutoa salamu za rambi rambi kwa niaba ya Kamati, kwa familia na ndugu wa Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyefariki tarehe 2 Juni, 2005 na kuzikwa kijijini kwake Utengule, Wilayani Kilombero na pia Marehemu Mheshimiwa Margaret James Bwana, aliyefariki tarehe 23 Juni, 2005 na kuzikwa Jijini Dar es Salaam. Wote walikuwa Wajumbe wenzetu katika Kamati hii. Wakati wa uhai wao, walitoa michango mikubwa na maoni mazuri sana yaliyosaidia kuboresha utendaji kazi wa Kamati yetu, Mwenyezi Mungu, aziweke roho zao mahali pema peponi, *Amin*.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha zoezi la kuchambua Bajeti ya Wizara kuhusu fungu la 44, Kamati ilizingatia vipengele vifuatavyo: Dira ya Wizara kwa kulinganisha na Dira ya Taifa kuhusu mchango wa Sekta ya Viwanda; majukumu ya Wizara; Taarifa kuhsu utekelezaji wa malengo ya mwaka 2004/2005; Taarifa ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya mwaka 2004/2005; Maelezo kuhsu Mapato na Matumizi ya kawaida, pamoja na fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2004/2005; maelezo ya Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2005/2006 na kupitia utekelezaji wa majukumu ya Wizara na ushauri uliotolewa wakati wa kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwamwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuweza kuiongezea Wizara hii fedha katika Bajeti ya mwaka 2005/2006, kwa karibu mara mbili ikilinganishwa mwaka 2004/2005 na hivyo, kutekeleza ushauri ambao tumekuwa tukiutoa mara kwa mara. Kamati imefurahia kuona kwamba, Sekta ya Viwanda na ya Biashara, zimepewa umuhimu katika Bajeti hii na kwamba, zinachangia kwa ufanisi zaidi katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA). Kamati inatoa wito kwa wakulima na wafugaji, kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo ili yatosheleze mahitaji ya viwanda nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara hii ni mengi, lakini jukumu la msingi zaidi ni lile la kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha kuongezeka na kuanzishwa kwa viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa, yaani viwanda mama. Pia kuhamasisha na kuwezesha upatikanaji wa masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini. Pia kwa kupitia Taasisi zake, Wizara inafanya tafiti mbalimbali kuhusu viwanda na ubora wa bidhaa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu hayo, Wizara pamoja na Taasisi zake, inaomba fedha chini ya vifungu 44 kama ifuatavyo: Matumizi ya Kawaida ya shilingi bilioni 14,774,569,400 na Matumizi ya Maendeleo shilingi bilioni 16,400,569,400.

Mheshimiwa Spika, Kamati inakubaliana na maombi hayo ya fedha na kutarajia kuwa, Wizara itatekeleza malengo waliyowekewa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nafasi ya Taasisi za Utafiti ni kwa kufanya tafiti nydingi na ambazo hapana budi zigharamiwe ndipo tutakapoweza kuwa na maendeleo ya viwanda na uboreshaji wa bidhaa na vifunganishio vyake. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kugharamia utafiti maana si rahisi kwa wahisani kugharamia utafiti ambao shabaha zake ni kujenga mazingira ya kujitegemea kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kanda za mchakato wa mauzo nje (*Export Processing Zones*), Tanzania imezungukwa na nchi jirani nane ambazo ni Msumbiji, Malawi, Zambia, Congo, Burundi, Rwanda, Uganda na Kenya. Hivyo, lipo soko kubwa na bidhaa zinazozalishwa hapa nchini zinaweza kuuzwa kwa urahisi kama zinakuwa na ubora utakaostahili ushindani. Kwa hiyo, Serikali iimarishe maeneo ya EPZ, kwa kuboresha miundombinu na kuhamasisha wawekezaji wengi kuwekeza katika maeneo hayo.

Aidha, Kamati inashauri Serikali kuanzisha Mamlaka Maalum ya kuhamasisha na kusimamia uwezeshaji wa kanda za mchakato wa mauzo nje. Ushauri huu unatokana na kuelewa kuwa, jukumu hili linahitaji ushirikiano wa vyombo vingine vinavyohusika na miundombinu ya uzalishaji, hivyo haliwezi kutekelezwa kama kazi ya kawaida (*Routine Function*), chini ya Shirika la Wizara au Wizara.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), litazamwe upya. Sheria ya kuunda Shirika la Maendeleo la Taifa, imepitwa na wakati na hivyo ni vema sheria hii ikatazamwa upya ili majukumu yake yaainishwe kwa uwazi na nafasi yake katika maendeleo ya Taifa yaye na mlango unaokubalika katika uchumi wa soko. Sambamba na hili, Shirika hili ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa, lipewe nyenzo ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, *Mtwara Development Corridor* inahusu shughuli nydingi mbalimbali. Aidha, mradi huu au mkakati huu wa maendeleo ni wa ushirikiano na nchi za Msumbiji, Malawi, Zambia na Tanzania. Kamati inashauri kuwa iiundwe Mamlaka Maalum ya *Mtwara Development Corridor* na iwe na bajeti yake ili iweze kutekeleza

majukumu yake ipasavyo. Mamlaka hiyo ingeweza kuitwa *Mtwara Development Corridor Commission*.

Mheshimiwa Spika, jitihada zetu za kuingia katika masoko ya nje hazitafanikiwa iwapo Tanzania hatutajitangaza vya kutosha. Kujitangaza huko kutahusu kushiriki kwenye maonesho ya kibiashara katika nchi mbalimbali duniani, pamoja na kuandaa vipeperushi na matangazo katika vyombo vya habari. Kamati inashauri kuwa, fedha za kutosha zitengwe kwa ajili ya shughuli ya kutangaza bidhaa za viwanda vilivyopo hapa nchini. Kazi hii iwe chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa kushirikiana na Wizara ya Ushirika na Masoko, Vyama vya Biashara na wenye viwanda.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko mengi mionganoni mwa wawekezaji kuhusu mwingiliano na kukosekana kwa chombo cha kuratibu shughuli za viwanda zinazoendeshwa na sekta mbalimbali. Kamati inapendekeza kwamba, Wizara ya Viwanda na Biashara, ipewe jukumu la kuratibu viwanda vilivyo katika sekta zote ili kuwe na udhibiti makini na ubora wa bidhaa zote zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, moja ya majukumu makuu ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni kuhamasisha na kuvutia wawekezaji katika viwanda. Hivyo, wawekezaji kutoka sehemu mbalimbali duniani, wanakwenda Wizarani hapo ili kuonana na Waziri au Maafisa wake, mahali ilipo Ofisi ya Viwanda na Biashara, hapana hadhi inayofanana na jukumu hilo kubwa. Kwa hiyo, Kamati inashauri kuwa, Wizara itafute ofisi mahali pengine penye mazingira ya kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo la Ubungo ilipojengwa *EPZ Millennium Business Park*, lilitengwa kwa ajili ya kukuza mauzo ya bidhaa chini ya EPZ na kwa kuwa jukumu kuu la Serikali ni kuweka miundombinu muhimu kuwezesha EPZ zianzishwe. Kamati inashauri kuwa, Serikali iendeleze majadiliano na mwekezaji huyu kwa nia ya kununua eneo hilo na kuboresha miundombinu inayotakiwa katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria ya Ushindani, ni kweli kabisa kuwa kwa sasa kinachoendelea kwenye uchumi wa Tanzania ni soko huria au uchumi wa soko. Soko lisilo na utaratibu na soko la namna hii, haliwezi kuwasaidia hivyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iharakishe kukamilisha kuundwa Tume na Baraza la Ushindani ili Taasisi hizi ziweze kusimamia utekelezaji wa sheria ya ushindani katika mazingira ya uchumi wa soko ipasavyo. Aidha, Tume ya Ushindani iandae mpango wa elimu kwa wadau wote wazalishaji, wasambazaji, wauzaji na walaji, ili waelewe kwa kina, maudhui ya Sheria hii ya ushindani katika uchumi wa soko ambao hapana budi uongozwe na kudhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru tena kwa nafasi hii uliyonipa ili nitoe maoni na ushauri wa Kamati yangu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu Waziri, Mheshimiwa Rita Mlaki, Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Wilfred Nyachia na watumishi wote wa Wizara hiyo, kwa

kuandaa vizuri vitabu vyao vya Bajeti na kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati wote tulipofanya kazi na Wizara hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi hii nzuri ya Kamati isingewezekana bila mchango mzuri wa Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, napenda kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Sumri Mohamed, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Nazir Mustapha Karamagi, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Marehemu Mheshimiwa Margareth James Bwana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka, ambaye aliwezesha Kamati hii kufanya kazi zake vizuri sana. Aidha, namshukuru Ndugu Aggrey Nzowa, Katibu wa Kamati, kwa kuihudumia Kamati kwa ufanisi mkubwa muda wote alipokuwa anahudumia Bajeti ya Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Kabla sijamwita Msemaji wa Upinzani, niwataje waliojiandikisha kuchangia kwa mdomo ili wasiende Mtera ni Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo na Mheshimiwa Mwanne Mcemba, wajiandae kwa kuitwa. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, atoe maoni ya Kambi hiyo. (*Makofi*)

MHE. ADELASTELA E. MKILINDI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuchukua nafasi hii, kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5) (b) (c) na 81(1), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuungana na wenzangu, kutoa rambirambi zetu za dhati kabisa, kwa familia za Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyejewa Mbunge wa Kilombero na Marehemu Mheshimiwa Magareth Bwana, aliyejewa Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuondekewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu, awalaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Naibu wake, Mheshimiwa Rita Mlaki, pamoja na watumishi wote walioshiriki kufanya kazi hii ya kuandaa bajeti ya Wizara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kiasi cha jumla ya shilingi 1,626,000,000/=, kwa ajili ya shughuli za maendekeo ambazo Wizara imeomba katika kipindi cha bajeti ya 2005/2006 na kiasi cha shilingi 14,774,569,000/= kwa matumizi ya kawaida, ni kidogo mno ukilinganisha na majukumu ambayo Wizara hii inapaswa kuyatekeleza. Haitoshi kwa Serikali kuendelea kuimba tu kuhusu umuhimu wa sekta ya Biashara na Viwanda katika kukuza Pato la Taifa bila ya kutoa nyenzo na uwezo wa kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama Taifa letu lina nia kweli ya kuendelea, Kilimo na Viwanda ndizo sekta za kuleta mabadiliko na hususan *vision* ya Taifa ya 2025 ya kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, tulitegemea Wizara hii ingewezeshwa kwa sehemu kubwa kutekeleza majukumu yake ambayo kwa ujumla wake ni kuunda Sera ya Viwanda na Biashara, kuanzisha viwanda mbalimbali na kuviuza kwa wawekezaji binafsi. Hili ni wazo jema japo *PSRC* imeshindwa kulitekeleza kama ilivyokuwa katika azma yake kuwa itauza viwanda na kujenga vipyta ambavyo itaviendesha na hatimaye kuviuza kwa watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, tusiwe na tegemeo la kuja kuanzishiwa viwanda mbalimbali na wageni. Ni jukumu la Serikali kubuni aina ya viwanda kufuatana na mazingira yetu. Tuvijenge na hatimaye tuviuze kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaona hili linawezekana, hasa kukiwa na nia ndani ya Serikali kuendeleza viwanda. Tunashauri Wizara hii itengewe fedha za kutosha ili kuendeleza sekta ya viwanda na kuviuza kwa *private sector*. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumesaidia shughuli nyingine kukua na hivyo kutoa ajira kwa watu wetu, pia Serikali itafaidika na kodi.

Mheshimiwa Spika, Sekta hii ya Viwanda na Biashara ni muhimu sana katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu, kitu ambacho hakina ubishi wowote ule. Mapato mengi kwa njia ya kodi mbalimbali hupatikana kutokana na sekta hii ya viwanda.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa sekta ya bidhaa za viwandani kwa mwaka 2004, ulibakia uleule wa kiwango cha mwaka 2003, wa asilimia 8.6 na mchango wake katika Pato la Taifa kwa mwaka 2004 ni asilimia 8.8. Kwa maana nyingine, tunaweza kuielezea kuwa hii inatokana na mikakati ya Serikali ya kutokutoa unaofuu unaohitajika ili kuilinda sekta hii ya viwanda kwa malighafi ipatikanayo nje ya nchi. Kitu kinachozidisha ughali wa uzalishaji bidhaa na ughali wa bidhaa kwenye soko, hivyo husababisha kukosa soko la ndani na nje kutokana na ushindani wa bei kwenye soko huria.

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya *TRA* ya Idara ya Kodi ya Mapato ya kuanzia miaka ya 1999 mpaka 2004, inayoonesha kiasi cha kodi ambacho kimeshindikana kukusanywa, sababu kubwa ikiwa ni makampuni kutojulikana ofisi zao zilipo (*Physical Addresses*), kwa mtazamo wetu sisi Kambi ya Upinzani kwa hili, Wizara na Mamlaka za kutoa leseni za biashara zinatakiwa ziwajibike.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa kumbukumbu wa makampuni yaliyo hai kwenye biashara ni muhimu, kwani tunaamini Wizara ndio mlezi wa makampuni. Hivyo, ukaribu wa Serikali (Wizara), kwa wenge makampuni kuelewa nini matatizo na mafanikio waliyonayo, ndio njia ya kuongeza Pato la Taifa toka sekta hii ya viwanda na vile vile kuongeza ajira katika sekta iliyo rasmi.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha utendaji wa kuleta tija katika sekta binafsi, Serikali na wabia toka nje ya nchi, imeanzisha Mfuko unaojulikana kama *Chief Executive Officers Scholarship Fund*. Ni mpango wa miaka mitano utakaogharimu dola milioni 6.3.

Mheshimiwa Spika, kwanza tunashukuru kwa Serikali kugundua kuwa udhaifu wetu kwa miaka mingi umekuwa kwenye uongozi na sio kwenye umaskini wa nchi katika kuongoza mashirika yetu. Tunaamini Watanzania wamesoma na sifa wanazo lakini wanakosa mbinu za kubadili mashirika yanayopata hasara ili yawe mashirika yenye kuleta faida (*to-transform loss making institution into profit making ones*), kwani ni ukweli uliowazi kuwa, kama mpango ungekuwepo toka zamani kusingekuwa na haja ya kuleta watu kama *Net Group Solution* hapa kwa ajili ya kuendesha *TANESCO* tu. Wapo Watanzania wangapi wenye uwezo na sifa kuliko watu wa *Net Group Solution*?

Hebu tuiangalie *CRDB* wakati iko chini ya Uongozi wa Mtanzania kwa asilimia mia ilikuwa inaelekea kufa. Sasa tunaona uongozi uliopo kwa kushirikiana na wa-Danish, *CRDB* ilivyofanikiwa. Wafanyakazi wengi ndani ya *CRDB* ni Watanzania. Hivyo, fursa ya kuona wenzetu wanafanya nini ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atoe ufanuzi ni watendaji wakuu wa makampuni na mashirika yenye sifa zipi wanaingizwa kwenye mpango huo? Mpaka sasa ni wakurugenzi wangapi wameshanufaika na mfuko huo? Ni wabia toka nchi gani ambao wameshakubali kuchangia mfuko huo?

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa makusudi kabisa ilianzisha mpango wa *Export Processing Zones (EPZ)*, ili kuviwezesha viwanda kuzalisha bidhaa kwa ajili kuuzwa kwenye soko la mpango maalum wa Marekani wa kusaidia maendeleo ya nchi za Afrika (*AGOA*). Kambi ya Upinzani, inamtaka Waziri, alieleze Bunge na Wananchi kwa ujumla, ni kwa nini wafanyakazi wafanyaokazi katika viwanda hivi wamekuwa na migogoro ya mara kwa mara na waajiri na sababu kubwa ikiwa ni maslahi yao na mazingira yasiyordhisha ya kazi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tukiambiwa na Waziri mwenye dhamana ya Uwekezaji kuwa, ubinafsishaji na uwekezaji katika viwanda umeongeza ajira. Hapa bado tuna matatizo, kwani tunavyoolewa ajira sio ya kwenda asubuhi kazini na jioni

kurudi au kuingia *night shift!* Ajira ni kuwa na uhakika wa kipato kitakachosaidia kuinua familia ya mwajiriwa. Kwa hali halisi ya viwanda vyetu vya nguo ambavyo vimo kwenye EPZ, ukweli ni kuwa, Watanzania wanawafanya kazi wageni, kwani mshahara wa shilingi 45,000/= kwa mwezi kwa maisha ya Dar es Salaam ni uuaji. Tunaiomba Serikali, iangalie viwango vya mishahara kati ya Watanzania na wageni katika viwanda hivyo, ajira na ujira lazima vifanane. Mtumishi alipwe ujira kufuatana na sheria ya nchi. Wawekezaji wengi wanalipa viwango vya chini na mara nyingi watumishi hawa huajiriwa kama vibarua, ni wachache ambaو wana ajira ya kudumu, hivyo, unakuta mfanyakazi anafanya kazi kwa miaka mingi kama kibarua na kukosa haki zake kama angeajiriwa kwa masharti ya kudumu. Kibarua halipwi NSSF, akipata ajali ya kazi halipwi fidia na kadhalika. Huku ni kumdhalilisha Mtanzania kwa lengo la kuwanufaisha wawekezaji. Tunaamini wawekezaji hawa huko wanakotoka wanazijua sheria, kwa nini wazikiuke nasi tukae kimya?

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Biashara inayojumuisha uuzaji wa jumla na reja reja, mahotelni na utalii, ilikua kutoka asilimia 6.5 mwaka 2003 hadi asilimia 8 mwaka 2004. Ukuaji huu ni kutokana na ongezeko la watalii nchini.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kabisa kuwa, Tanzania ina wafanyabiashara wengi, wenyen moyo na ari ya kufanya biashara, tatizo kubwa ni kujua aina gani ya biashara ifanyike, ambayo itakuwa endelevu kwao na kwa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie ushauri tuliooutoa katika hotuba yetu ya mwaka 2004, kuhusu mtazamo wa Watanzania kwenye biashara. Itabidi tukubaliane kuwa, Watanzania huko nyuma hatukuzwa kwenye maadili na hulka ya kibashara, hivi sasa tumeingia na inatulazimu kushindana kwenye Jumuiya za watu ambaو wao ni wafanyabiashara wa miaka mingi, wamelelewa na kukulia kwenye biashara. Wanachama waliomo kwenye ushirikiano wa Jumuiya ya nchi za Afrika ya Mashariki, utakuta viongozi wake na Watendaji Wakuu Serikalini, wote ni wafanyabiashara. Hapa ndipo wanapotuzidi kete na kuchukua nafasi kubwa zaidi kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi. (*Makof*)

Hapa kwetu watendaji wengi Serikalini hawana *background* ya biashara, wengi ni wakiritimba kitu kinachosababisha ukwamishaji wa kutoa maamuzi ya haraka kwenye masuala yahusuyo biashara. Mfano, wenzetu wa Uganda, soko la *AGOA* wamelitumia vizuri sana na wengi limewanufaisha, kwa nini Tanzania bado wafanyabiashara wetu hawajanufaika nalo ingawa nchi yetu ina bidhaa nyingi za kuuza kuliko wenzetu. Katika biashara wa kwanza kulikamata soko ndio wanaonufaika zaidi, hivyo, *timing* kwenye maamuzi ni muhimu sana, vinginevyo Tanzania itaendelea kupewa sifa kubwa ya kuwa mabingwa wa kutengeneza sera nyingi nzuri zisizokuwa na misingi ya utekelezaji. Kwa kuongezea hapo, naomba niungane na Mheshimiwa Leonard Derefa, kwenye mchango wake alioutoa kwenye semina moja hapa Bungeni kuwa, sasa ni wakati wa kuwa na watendaji wenyen *Business Acumen* ili kuweza kufanya biashara. Alikuwa anaongelea *TAZARA* inavyokosa mizigo ya kusafirisha baina ya Tanzania na Zambia.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Biashara (*Tanzania National Business Council*), pamoja na kazi ya kuwa kiungo kati ya Sekta binafsi na Serikali, bado tunadhani kazi yake inatakiwa kuwa ni ya kubadili mtazamo wa biashara kwa Watanzania, kwa maana ya kutoa ushauri wa aina ya biashara na jinsi ya kufanya hiyo biashara kwa wafanyabiashara kutegemea sehemu waliyopo (*feasibility studies on business before taking off*). Hii itasaidia kuondoa msongamano kati ya wale wenye mitaji mikubwa, ya kati na midogo, kugombea aina moja ya biashara, kwa mfano, biashara ya Daladala, biashara ya kuza *computer*, biashara ya simu za mkononi, biashara ya *salon* na nguo.

Mheshimiwa Spika, kwa mtaji huu bila ya kufanya juhudzi za lazima kuubadilisha mtazamao huu wa wafanyabiashara toka *short term* kwenda *long term investment*, nchi yetu itaendelea kupiga hatua za kusimama pale pale wakati wenzetu wanakwenda mbele. Kwa Tanzania mianya ya biashara bado ni mingi na wenye mitaji wapo lakini wanakosa wafanye nini badala yake wanakimbilia biashara ya uchuuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na mpango wa kurekebisha mashirika ya umma, ni viwanda vingi vimeuzwa kwa asilimia 100 na vingine kwa ubia na Serikali. Kutokana na hilo, Watanzania walitegemea ufanisi mkubwa ikiwa ni pamoja na ajira ya kuongeza tija kwa Watanzania. Badala yake tumeshuhudia viwanda vilivyouzwa, vinafanya biashara tofauti na ile iliyokuwa inafanya na viwanda hivyo kabla ya kuuzwa. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri, atueleze inakuwaje aliyenunua kiwanda anashindwa kutimiza masharti yaliyomo kwenye Mkataba wa ununuza na mpaka sasa Serikali imekwisha rudisha viwanda vingapi kwenye himaya yake baada ya wanunuza kushindwa kutimiza masharti? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya fedha na bima, mali na huduma za kibiashara, takwimu zinaonesha kuwa na ongezeko la asilimia 0.1 mwaka 2004 katika sekta hii kwa kulinganisha na mwaka 2003 iliyokuwa asilimia 4.4, lilitokana na sekta ndogo ya fedha na bima. Tafsiri hii itokanayo na fedha na bima inatokana na kuwa na viwango vikubwa vya riba vinavyotozwa kwa wakopaji na vilevile viwango vidogo vya riba vitolewavyo kwa wanaoweka fedha zao kwenye mabenki. Kwa kukumbushia maneno ya Waziri wa Fedha aliyyatoa humu Bungeni kuwa, Mabenki yana mabilioni ya pesa zinazongoja kukopeshwa kwa Watanzania. Tunachojiliza ni mfanyakibashara gani atakayeweza kulipa mkopo wenye riba kubwa? Si hilo tu, bali mfumo wa mahesabu unaotumiwa na mabenki kupata riba bado unachanganya watu wengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema haya, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza katika kuchangia kwa siku ya leo. Kwanza na mimi kama mwenzangu, nitoe pole za rambirambi kwa aliyejewa Mjumbe mwenzetu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, aliyejewa Mbunge wa Viti Maalum, kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, aliyejewa Mbunge wetu wa Jimbo la Rahaleo na pia kwa familia ya Marehemu

Mheshimiwa Abu Kiwanga, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero, Mungu awalaze mahali pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Spika, mimi kama wenzangu, napenda pia kushirikiana na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuwa mteule wa Chama chetu Tawala. Pamoja na Mheshimiwa Abeid Amani Karume na Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, wote kwa kuwa wateule wa Chama chetu Tawala, Chama cha Mapinduzi na ninaamini watashinda kwa ushindi mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, shukrani zangu ziende kwa wananchi wa Jimbo la Mlandege kwa muda wote huo ambao wamekuwa na mimi tukishirikiana katika kutekeleza Ilani yetu ya Uchaguzi wa Chama chetu cha Mapinduzi, kubwa kabisa, kwa ujenzi wa Shule ya Makadala ambayo tayari imefunguliwa na watoto au wanafunzi wa kiume na wa kike wanasoma hapo.

Mheshimiwa Spika, napenda tena nichukue nafasi hii kuwaomba wananchi wa Jimbo la Rahaleo wanipokee rasmi kwa sababu Jimbo letu la Mlandege limechangamshwa na Jimbo la Rahaleo. Kwa hiyo, nakwenda kuomba nafasi ya Ubunge katika Jimbo la Rahaleo. Naamini watanipokea kama walivyonipokea wananchi wa Jimbo la Mlandege. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza wanawake wote ambao wamegombea Udiwani na wamepata kura za maoni, nawapongeza sana na hasa kwa Jimbo la Mlandege, Ndugu Salma Msellel ambaye amepita kwa kura kura nyingi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye hoja ya Wizara ya Biashara na Viwanda kwa siku ya leo. Nachukua nafasi hii kumpongeza rasmi Waziri - Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Naibu Waziri - Mheshimiwa Rita L. Mlaki na Katibu Mkuu - Ndugu Nyachia kwa hoja yao waliyoileta hapa na sote tumeona mengi yaliyokuwemo humu ni mambo mazuri ambayo yamefanyika katika kipindi cha mwaka mmoja. Kwa hiyo, ni mafanikio ya Wizara yetu ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, naanza kwanza kwa kupongeza maonesho ya kibiashara ya 29 ya Sabasaba ambayo yamefanyika katika Uwanja wa *Mwalimu J.K. Nyerere Trade Fair Ground* na ni maonesho mazuri sana na tunashukuru kwamba safari hii kulikuwa na mabadiliko hasa kuwfurahisha wananchi kwa kuwa Milango iliongezwa, kwa hiyo, msongamano wa wananchi kwenda kwenye maonesho haukuwepo. Kwa hiyo, tunashukuru sana na wananchi wengi wameweza kushiriki kwa raha zao.

Pia, bidhaa nyingi tumeziona za ubora ambazo zimetoka humu humu kwetu na pia nchi za nje. Huduma za mafunzo kutoka Taasisi mbalimbali na asasi yalikuwepo pale.

Mheshimiwa Spika, mimi nilifurahishwa sana na hali hii ya kwamba kuna mafunzo ambayo yanaoneshwaa katika maonesho yetu. Natoa mfano kwenye Shirika la *TPDC*. Hapa tunazungumzia namna ya utekelezaji wa MKUKUTA na namna mipango

ya kuondoa umaskini, sasa tulivyoingia kule ndani ya *TPDC* tumeona kwamba Shirika hili la *TPDC* limetuonyesha matokeo ya utafiti wao wa mafuta kama yapo Tanzania. Mimi naona hii ni hatua kubwa sana na nzuri kwa wananchi wote kufahamu na wakawa wanaonesha kabisa kisayansi mafuta yameonekana kwenye miamba na pia katika bahari.

Mheshimiwa Spika, hili limenifurahisha kwa sababu na sisi Pemba tunda-ua zimeonekana alama za mafuta. Kwa hiyo, kwa Visiwani kwetu matatizo ya umaskini tunajua iko siku tutayamaliza.

Mheshimiwa Spika, pia nilipongeze Shirika la *SIDO*, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo Vidogo. Shirika la *SIDO* limefanya vizuri sana na Mheshimiwa Waziri ukisoma hiki kitabu cha leo, nusu ya kitabu hiki ni mafanikio ya Shirika la *SIDO* kwa sehemu mbalimbali, kwenye kutoa huduma za ufundi, kwenye mafunzo ya wafanyabiashara wadogo wadogo, ukuzaji wa masoko na pia teknolojia na upatikanaji wa mitaji pia na mikopo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kilio changu kikubwa hapa ni kwamba: Je, Zanzibar kuna tatiizo gani hatuanzishi Tawi la *SIDO*? Ukisoma hotuba hii utaona kila sehemu inaonyesha, kwa mfano ukurasa wa 14, wananchi wengi hasa wa kipato cha chini wamehamasika na kuanzisha miradi mingi midogo midogo ikiwemo viwanda vya kukamua mafuta ya kula kutokana na Mbegu, viwanda vya samani, viwanda vya kusindika matunda, ufumaji wa nguo na ushonaji. Sasa haya yote na Zanzibar sisi tunayahitaji.

Mheshimiwa Spika, hapa Mheshimiwa Waziri pia amezungumza kwamba kuna tamko la Zanzibar katika Mkutano ule mkubwa tunatajwa. Ukiangalia Mheshimiwa Waziri anaelezea kwamba: "Tamko la Zanzibar lenye mchango mkubwa katika kuimarisha hoja za kuendeleza maslahi ya nchi maskini katika biashara za Kimataifa." Lakini hii *SIDO*, Shirika la viwanda vidogo vidogo au miradi midogomidogo kuwashamasisha wananchi wetu Zanzibar hatuna Kituo au Tawi. Ukiangalia pia katika ukurasa wa 26 Mheshimiwa Waziri ametuelezea kwamba kuna Vituo vingi kama 93 ambavyo *SIDO* imeanzisha. Sasa naomba basi, ongezeni viwili, kimoja Unguja na kingine Pemba viwe angalau 95 kwa sababu tumeshaona kwamba *SIDO* ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka hapa Mheshimiwa Rais Mkapa alizungumzia sana mambo ya *SIDO* na akatuomba wananchi wa Tanzania tuthamini vitu vinavyotengenezwa *locally* na usemi ule wa kusema *Think Globally but buy Locally*, sasa Wazanzibar tukanunue wapi na sisi ndiyo tunataka hii *locally*?

Mheshimiwa Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili kwa sababu Zanzibar tayari tunazo *NGOs* kama vile Tanzania *Gatsp Trust* ambao wanafanya sana (kazi za mikono). Tungewaterumia NGO hao na tungeanza na wana- Mikono halafu tukaanzisha hili Shirika la *SIDO*. Kwa hiyo, hili lilikuwa ombi kwa Waziri na Menejimenti yake afikirie tu kuongeza Vituo viwili tu, Unguja kimoja na Pemba kimoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nimelifurahia katika Wizara hii, iko ukurasa wa 96 ambao Mheshimiwa Waziri hapa ameellezea kwamba Wizara itaendelea kushirikiana karibu na wenyewe Viwanda na Biashara ili kujua matatizo yao na kuyatafutia ufumbuzi. Hii ni muhimu sana kwamba Wizara sasa ifanye *workshop* kubwa tu katika Mashirika yake madogo madogo pamoja na wadau wenyewe kwa sababu tunataka kushiriki kwa wingi zaidi katika masoko haya ya Kimataifa na wakikaa pamoja ndiyo watajua namna ya kuyatatua matatizo na kero za biashara.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Ndugu Reginald Mengi kwa kipindi chake kizuri kwenye *ITV* ambacho kilikuwa kinahusu *CTI* na wadau ni mdahalo wa wafanyabiashara ndogo ndogo, wameweza kutoa mawazo yao na kutoa matatizo yao. Kwa hiyo, hili mimi naliona zuri sana na ninaamini litatekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nimeliona kama ni muhimu katika Wizara hii, ni kwamba waweze kuhamza haraka katika ile Ofisi. Sasa hivi mafanikio yote mazuri, wawekezaji wanakuja, nchi za nje zote zinakuja na Ofisi yao pale hairidhishi kutokana na majukumu makubwa wanayoyafanya na kukutana na watu mbalimbali. Kwa hiyo, naomba kama wazo hili lilikuwepo, basi haraka liweze kufanikishwa.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo napenda kuchangia ni kuhusu Tume. Mimi kama wenzangu walivyosema, tunaomba Serikali iharakishe kukamilisha kuundwa kwa Tume na Baraza la Ushindani ili liweze kusimamia Sheria ya Ushindani. Tume hii hii tutaiomba iandae mipango ya kuweza kuelimisha wadau, wazalishaji, wasambazaji na pia sisi walaji. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kutukumbuka walaji. Malalamiko na matatizo yetu yote hapa tutaweza kuzungumza katika sehemu yetu hii au Baraza letu la Walaji.

Kwa hiyo, mimi nilikuwa nahimiza tu kwamba Tume haraka haraka iundwe maana yake najua kwamba matayarisho yako tayari, lakini ianze kazi kwa sababu sasa hivi tunasema tunataka kubadilika mawazo yetu tuwe na utamaduni wa kibiashara ili tupate uchumi wa soko, siyo soko huria.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nafikiri hii Tume ni chombo muhimu sana tuache yote tuanze na hii Tume. Pia, hii Tume iweze kusimamia sheria zetu za biashara iweze kutusaidia katika kuondoa kero katika Sekta za Biashara.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kuiombea hii Wizara iongezewe fedha kwa sababu safari hii imeongezwa fedha kazi yake kubwa imeonekana na mafanikio tumeyaona. Lakini kuna tatizo kubwa ambalo ninaliona linakwamisha kwa wazalishaji wetu ambao wanataka kupeleka bidhaa zetu nje, nalo ni tatizo la *packaging*. Hii *packaging* kwa sababu ukiuza biashara zako ni lazima uzifunge vizuri, zipendeze, mtu akisoma aelewe tunatangaza nini.

Kwa hiyo, naomba haya Mashirika yaliyokuwa chini ya Wizara kama *TIRDO*, *TBS* yaangalie ni namna gani tunaweza kutatua tatizo la *packaging* kwa sababu sasa hivi

ni biashara ya ushindani na kama kushindana bidhaa itachukuliwa vizuri ile iliyofungwa vizuri, hapa hakuna uzalendo. Kwa hiyo, mimi nafikiri *packaging* tujitahidi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo. Mimi ningeomba sana Serikali itusaidie tuondokane na tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza *SIDO* kwa kupitia Wizara hii kwa kutoa mikopo kwa ajili ya wajariamali hasa wanawake. Tena tumeambiwa wanawake 5,236 wamepata mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.7. Hili ni jambo kubwa sana kwa sisi akina mama na ikiwa kila kipindi wanawake wengi hawa wanapata mikopo kwa sababu wanarudisha, mimi ningeomba tu kwamba *SIDO* sasa iongeze hii mikopo kwa akina mama wengi.

Tumeona juzi kwenye maonesho, akina mama wanatengeneza *wine* nzuri tu kutoka Kibaha na wakasema kwamba kama soko kubwa wanalo, lakini hawana mitaji na mikopo. Wale akina mama tayari wanatengeneza *wine*, wengine wanasantika vyakula vyao, mfano *yogurt*, *cheese* na vitu vidogo vidogo vingi tu. Mimi nafikiri tumwombe Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Basil Mramba, aombe mabenki yapunguze riba tupate mikopo mingi ili akina mama na wao waweze kushiriki kiuchumi, kwa sababu, kisiasa tumeshafuzu tuko mbali sana na karibuni tutapata hiyo asilimia 30 ya wanawake. Tutakuwa wengi humu Bungeni. Tunataka tuwe wengi pia kwenye kushiriki katika kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nitoe maoni yangu kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Kwa vile hii ni mara yangu ya pili kuongea, nilikwisha toa rambirambi zangu kwa yote yaliyotupata kutokana na wenzetu huko nyuma, lakini kuna moja hili la Mheshimiwa Margareth Bwana ambalo limejitokeza hivi karibuni. Kwa kweli imetusikitisha, lakini ndiyo maamuzi ya Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, inanibidi nitoe rambirambi kwa Wanarukwa, Ndugu na Jamaa wa karibu kuhusiana na kifo cha ndugu yetu Margareth Bwana.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze sana Waziri wa Viwanda na Biashara kwa hotuba yake, imekuwa wazi, imekuwa mahiri kabisa, imeeleweka, kwa hiyo, ninampongeze sana. Pia, nimpongeze Naibu Waziri Ndugu yetu Rita Mlaki kwa kushirikiana na Waziri kutoa hotuba nzuri, Katibu Mkuu pia Makamishna wote wa Wizara na Watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Nawashukuru sana kwa hotuba ilivyokuwa nzuri na sote tumeielewa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri, kuna machache ambayo ningependa niyazungumzie kama tu kupata mwelekeo wa shughuli hizi tunakwenda nazo namna gani. Sasa tuna mipango mingi ya kutaka kujikwamua kiuchumi, mipango ya kuondoa umaskini na mipango ya kuboresha uchumi wetu ukue uweze kutusaidia tufaidike

Watanzania tuishi maisha mazuri. Tuna mawazo mbalimbali ambayo yamejitokeza hapa kwa mfano mawazo ambayo tunayatekeleza sasa ya *EPZ*, namna ya kushughulika na utaratibu huo, kuitekeleza *EPZ* na namna *EPZ* inavyoweza kutusaidia tuweze kuondokana na umaskini na Taifa liendelee.

Nashukuru juhudi za Ubungo, zinaonekana na sehemu nyingine pia, lakini nilikuwa nategemea labda katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri angezungumzia suala kwamba atafika Mwanza ili tufanye shughuli hii, Kituo kimoja cha *EPZ* kijitokeze Mwanza. Dar es Salaam tumefanya vya kutosha sasa Mwanza lini tutafika?

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hayo, nina imani kwamba kwa mwelekeo huu na jinsi Wizara inavyotekeleza mipango yake siku moja tutafanya juhudi hizo na tutafanya kazi hiyo Mwanza. Kuna sehemu ya kiwanda cha Vioo ambayo iko eneo la Mkuyuni kule Nyegezi, nilidhania kwamba sasa Wizara ingeweza kuwa angalau imeweka mipango kwa sababu kuna swali moja niliuliza Bungeni na nilijibiwa pia na ninashukuru kwamba Naibu Waziri alikuja Mwanza, tukaenda mpaka eneo hilo, lakini ikaonekana kwamba eneo linaweza likatumika kwa *EPZ*. Sasa labda Waziri ataniambia anapanga nini kwa ajili ya Mwanza ili iweze kujitokeza na tutumie eneo hilo tuweze kuwa na *EPZ* sehemu ya Mwanza.

Lakini kingine ambacho ningependa kuliongelea katika maeleo ya Waziri, niweze tu kupata msimamo wa Wizara kuhusiana na mpango mpya wa *Special Economic Zones* ambao sasa ndiyo mtindo mpya, tumeanza kuuingia kwa ajili ya kuendeleza Taifa na kuondoa umaskini. Katika mpango huu, mimi nina imani kabisa kwamba Wizara ina nafasi kubwa ya kufanya shughuli pale katika huu utaratibu mpya wa *Special Economic Zones*.

Sasa katika hotuba ya Waziri sikusikia amezungumzia nini, lakini hapa nina imani kabisa kwamba Wizara inapaswa ndiyo iwe mhimili mkubwa wa Sera ya Viwanda katika eneo hilo, iwe mhimili mkubwa wa taratibu za masoko katika eneo hilo na iwe mhimili wa mipango yote ya kibiashara. Sasa kama sera na mipango hii imeanza, lini sasa Wizara itapanga mipango hii na itajiingizaje kwa sababu ina nafasi kubwa na inapaswa ifanye kazi pamoja na Taifa ili kwamba tufaidike na huo mpango mzima uweze kutuletea mafanikio Tanzania.

Jumamosi tulikuwa na Semina hapa, Semina ambayo imetupanua mawazo sana Wabunge. Suala la *Mini Tiger in Tanzania* namna gani tufanye mipango yetu kwenda mbele na ninashukuru sana kwamba tumeamua kuiga mfano wa Asia kwa sababu Asia *actually* sasa hivi ndiko mahali ambako tutajifunza mambo hayo, ni watu wanashughulikia taratibu za kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Hawa ndiyo wanatekeleza mipango hii, inaonekana wazi, huko ndiko tunaweza tukajifunza mengi na ninashukuru kwamba Serikali imeamua kufanya hivyo na nina imani kwamba na sisi pia katika mipango hii Wizara iwe na nafasi yake ya wazi kabisa katika kutekeleza mipango hii na utekelezaji mpya wa kuondoa umaskini.

Lakini kingine ambacho ningependa kukisemea kwenye hilo, ni kwamba katika mipango yote hii ya ziara kutembelea maeneo mbalimbali, kupeleka watu wetu kujifunza kwa wenzetu kuonatufanye nini sisi huku Tanzania, tunakwenda nchi mbalimbali kama Amerika, Uingereza, Ulaya na Asia, pia sasa tumeanza kwenda. Sasa ningeomba kwamba Wizara labda ingesimamia huu mpango kuieleza Serikali kwamba tunapokuwa na ziara hizi, *private sector* zihuishwe sana katika mipango hii.

Kama Rais anakwenda kutembea Asia, basi aende na wafanyabiashara wengi kwa sababu hawa ndiyo watakwenda kujifunza na kuona wakirudi huko watakuja kutekeleza mambo hayo. Ningeomba Wizara isimamie hilo na iliingize ndani ya Serikali kwamba tunapokuwa na ziara hizi, safari za namna hiyo basi, *private sector* ningeomba sana ihusishwe na iende ili iweze ikajaribu kujifunza.

Mheshimiwa Spika, kuna mfano tu ningeusema kwamba nilitembelea China kwa mpango huu wa kujifunza. Wizara ya Mipango ilifanya mpango mzuri na mipango yake ndiyo inaanza kujitokeza ndiyo *Mini Tiger* hizi zinajitokeza. Lakini nilichoona, China kuna mengi, watu wetu wanawenza kujifunza wakienda huko ambavyo wangejifunza wakienda Amerika. Kwa mfano, wakienda kumwangalia mkulima wa Amerika, wao ni wakulima wa aina yake. Ni tofauti na sisi hapa, unakuta mkulima anajitegemea kivifa mpaka Watumishi Watendaji wakubwa kama Bwana Shamba na Wataalam mbalimbali lakini kwa utaratibu wa China wanakuwa na *Communities*, wanam-share yule mtaalam, wana-share vile vitendea kazi na wanalima mashamba madogo madogo.

Kwa hiyo, sisi tukienda kujifunza kilimo kule China, tutaelewa mengi na wakulima wetu wakitoka kule watakuja wafanye mambo. Watatoka na elimu ya kutosha kule na wakija nyumbani lazima wataanza *ku-practice* waliyoyaona kule, wanawenza wakatusaidia sana. Kwa hiyo, kwenye hili mimi ningeomba sana Wizara pamoja na Wizara ya Mipango washirikiane, tunapokwenda kutafuta elimu hii ya kujifunza kwa kuona na vitendo ningeomba tuelekee Asia zaidi.

Mheshimiwa Spika, kingine, ningeomba tu nishukuru sana Serikali kupitia Wizara hii kuhusiana na kuifufua *MWATEX*. *MWATEX* sasa inafanya kazi na Waziri nimemualika kwenda kututembelea Mwanza kwa ajili ya jambo hili. Alimtuma Naibu Waziri na tulizunguka naye mpaka *MWATEX* na tuliangalia kazi iliyopo pale. Lakini ningependa pia afike kule kwa sababu unapokuwa pale na kuona mambo *on sight* unajifunza mambo mengi sana, ukirudi unaweza ukawasaidia wale wawekezaji ambao wanaiendesa *MWATEX* sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hilo, mimi ningeomba tu niiieleze Serikali kwamba kuna wafanyakazi wa *MWATEX* iliyofungwa ambao wanadai mafao yao, taratibu zake hazijaelezwa wala kuwekwa wazi mpaka sasa. Kabla ya ubinafsishaji na kabla ya kutaifisha *MWATEX*, *MWATEX* ilikuwa mali ya Vyama vyya Ushirika waliokuwa wanamiliki *MWATEX*, ni wakulima walikuwa wameshirikiana na mfanyabiashara mwagine ambaye kwa makubaliano ya kibiashara walikuwa wanaendesa shughuli zao sawasawa.

Lakini baadaye, Serikali ilijiingiza pale ikataifisha *MWATEX*. Sasa mimi nilijiuliza maswali kwamba hivi Serikali inataifisha kwa kumpa nani? Inawanyang'anya wakulima, inataifisha sijui inampa nani! Lakini pamoja na hilo lililofanyika, basi *MWATEX* haikuendelea tena, ilisimama. Baada ya kusimama, kuna mambo pale yalijitokeza mengi ambayo naamini Serikali inabidi ijifunge mkanda iyakamilishe yote kwa vile ilijiingiza pale.

Labda kama Serikali isingetaifisha, labda wakulima wangeendesha *MWATEX* mpaka leo. Utaratibu wa kawaida wa kuamua na kumaliza taratibu nzima ya kufilisi Shirika ni kwamba Serikali ilipeleka *MWATEX* isimamiwe na *LART*, bahati mbaya *LART* haikuja na mawazo mapya na ilikuwa inang'ang'ania tu kudai madeni na *MWATEX* ilikuwa imekaa muda mrefu bila kufanya kazi, lakini bahati nzuri baada ya majadiliano marefu na Waziri namshukuru sana Waziri, tulishirikiana sana kwenye hili.

Pia, namshukuru sana Waziri wa Fedha, tulishirikiana sana kwenye hili akaamua kuyaondoa madeni yote *MWATEX*, ndiyo hilo lililojitokeza. Sasa kwa nyuma huko mpaka sasa *LART* haijalipa wafanyakazi walioondoka *MWATEX*, madai yao kama wafanyakazi bado yako hai pale, lakini kwa vile Serikali ilijiingiza pale ni vizuri sasa kwa kuwa iliamua kuvua nguo, basi ioge maji. Siyo kuvua nguo halafu unaogopa kuoga maji. Kwa hiyo kwa kuwa walijiingiza, ni vizuri wakamilishe. Hao watumishi wana haki kabisa ya kudai haki zao na tutawasimamia, tutawatetea mpaka wapewe haki zao kama tulivyofanya kwa Watumishi wa Shirika la Reli kuitia *East African Community*.

Mheshimiwa Spika, nasema na ninaiomba Serikali iliangularie hili kwa makini na nipaye majibu, hawa watu watalipwa lini? Wanalia wako wengi na mali zote wanazo wao walikuwanazo Serikali kwa utaratibu wake kabisa. Sasa sio vizuri na sioni kama ni busara kuendelea kubaki na kuwapa mgongo hawa watumishi ambao walifanya kazi yao kwa utaratibu uliokuwepo kwa wakati ule. Kwa nini, sasa wasilipwe? Mimi naomba na ninasema kwamba hawa wana haki kabisa ya kulipwa ili kwamba sasa suala la *MWATEX* liishe na shughuli ziendelee vizuri na kila mmoja aridhike.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia tu naomba sana kwa heshima kubwa nimshukuru sana Waziri wa Fedha kwa sababu naweza nisipate tena nafasi ya kuzungumza kwa juhudzi zake nyingi alizozifanya kuhusiana na *MWATEX*, lakini pia kwa mambo mengi ambayo sasa ameyafanya Mwanza. Palikuwa na jengo la *Revenue Office* ambalo lilikuwa gofu, tulizungumza naye hapa Bungeni sasa amelikamilisha na limekuwa tayari. Kilichobaki tu ni Maofisa wa *TRA* sasa warudi kwenye jengo lile ili waache nafasi kwetu sisi wengine tuweze kupata nafasi za *offices* katika maeneo mengine.

Pili, amejitahidi sana kwa kushirikiana na Mashirika yake ya fedha *PPF* na *NSSF*, wanajenga sasa majengo Mwanza ya Kisasa, yatakuwa marefu, mazuri na majengo ambayo nina imani yatakuwa yanaipamba Mwanza na yatatusaidia sana kutupatia nafasi kwa ajili ya kutumia na kiofisi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache naunga mkono hoja ila nasisitiza sana Watumishi wa *MWATEX* walipwe haki zao. Ahsante sana. (*Makofii*)

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Lakini awali ya yote nami nianze kwa kutoa pole kwa msiba uliotokea wa Mbunge mwenzetu Margaret Bwana. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Lakini binafsi, nimshukuru Mheshimiwa Waziri mwenyewe na Naibu wake kwa kuainisha yaliyomo haya kwa kutamka Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Yote yaliyomo humu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie mambo matatu. La kwanza, nitazungumzia bei ya vitu; la pili, nitazungumzia ubora wa bidhaa zetu na tatu, nitazungumzia viwanda vyetu.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la bei. Mimi ni mtoto wa mkulima na asilimia 70 ya Watanzania kama siyo asilimia 80 wanalima kwa kutumia jembe la mkono. Sasa kwa bahati nzuri au mbaya, Mheshimiwa Waziri hili analijua kabisa kwamba asilimia 80 ya Watanzania wanalima kwa jembe la mkono. Lakini kwenye hotuba yake, bahati mbaya hakuzungumzia suala la jembe la mkono pamoja na viwanda vyake.

Lakini jembe la mkono kwa sasa huko Vijijini linauzwa kwa Sh.2,000/= kwa jembe moja. Ni ghali kweli kweli kwa mkulima mdogo aliyeko Sumve, Ksimba, Magu na Mkoa mzima wa Mwanza. Lakini pia jembe la kukokotwa na ng'ombe, maksai kwa sisi wakulima wa Mkoa wa Mwanza linauzwa Sh.65,000/= mpaka Sh. 70,000/. Ni ghali kweli kweli kwetu.

Mheshimiwa Spika, lakini nikija kwenye saruji, kwa upande wa Mkoa wa Mwanza hasa katika Wilaya ya Ksimba, Mfuko mmoja wa sementi unauzwa kwa Sh.12,000/= mpaka Sh.13,000/. Lakini pia mabati yanauzwa kwa Sh.12,000/= mpaka Sh.13,000/= kwa bati moja. Tunazungumzia ujenzi wa nyumba bora na tunazungumza kwamba bei ya saruji ipungue, lakini ukitazama kama unataka kujenga nyumba bora, mfuko wa sementi ni Sh.12,000/= au Sh. 13,000/. Sasa tuna mpango wa MMEM na MMES, *TASAF*, kwa hali ya bei kama hii nafikiri haitusaidii kujenga Shule zetu vizuri na haitusaidii kuboresha makazi yetu vizuri.

Mheshimiwa Spika, lingine ni bei ya sukari. Kule Vijijini, sukari inayotengenezwa na viwanda vyetu, kilo moja ni Sh.800/= mpaka Sh.1,000/. Sasa wananchi wengi wanaikimbia sukari, wanatumia ukwaju. Ni mzuri, lakini imefikia kipindi sasa sukari ingekuwa kama vile anasa kwa wananchi wetu! Kwa sababu mzee

wa viwanda na Mheshimiwa Waziri ndiyo mwenye viwanda, hebu hili nalo alitazame vizuri. Si vizuri sana wananchi kutumia ukwaju wakati wote.

Mheshimiwa Spika, lakini nimeyasema haya ya jembe la mkono na jembe la kukokotwa na ng'ombe kwa makusudi kabisa kwamba wananchi wa Jimbo langu la Sumve na Jimbo la Kwimba kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni, Mheshimiwa Bujiku Sakila, ni kwamba bidhaa hizi sasa kwetu imekuwa kama kero. Kwa nini? Nafikiri ndugu zetu wa *TBS* wapo, ndiyo maana nikasema nitazungumzia ubora. Majembe ya mkono haya na plau hizi havina ubora tena. Siyo chapa jogoo ile ya zamani wala siyo chapa mamba ile ya zamani.

Mheshimiwa Spika, nililetewa mifano ya majembe matano mapya wameyatuma siku moja yakajikunja na mengine yakavunjika kwenye ardhi ya kawaida kabisa na majembe hayo nililetewa na mzee mmoja anaitwa Mzee Nswagi, majembe matano mapya chapa jogoo na chapa mamba. Sasa wenzetu wa *TBS* nafikiri ni vizuri zaidi wangetazama vizuri hayo majembe, tunaambiwa yanatoka China.

Ni vizuri zaidi wakatazama ule ubora kwa sababu kwa kawaida zamani mkulima wa Mwanza anaponunua jembe moja, analitumia kwa msimu mzima, ndiyo linakwisha. Lakini leo imekuwa ni biashara ya kwamba ananunua jembe leo kesho linavunjika, keshokutwa anakwenda kununua lingine kwa Sh.2,000/= . Sasa kwa msimu mzima anaweza kujikuta amenunua majembe matatu au manne. Ningombaa sana *TBS* itazame majembe hayo.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, kwenye zile ndimi za plau, hizo hazina ubora. Tena mkulima akilimia ekari moja, unakuta huo ulimi wa plau umekwisha na lakini siyo kwisha tu, bali utakuta umevunjika. Sasa unajiliza; je, hapo kuna ubora? ubora unakuwa haupo. Kwa hiyo, nawaomba watu wa *TBS* wajaribu kuangalia ili kuwasaidia wakulima wetu wasipate taabu kuhusu jembe la mkono na hayo majembe ya kukokotwa na ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie lingine kuhusu suala la viwanda. Katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, amezungumzia kiwanda cha *UFI*, lakini hapa anasema, naomba ninukuu: "Viwanda vingine vilivyobinafsishwa ambavyo vinafanyiwa ukarabati ni pamoja na kiwanda cha zana za kilimo cha *UFI* Ubungo Dar es Salaam ambacho kimepata mwekezaji mpya atakayetengeneza mabomba hasa kwa ajili ya mradi wa maji wa Ziwa Victoria."

Mheshimiwa Spika, sasa kiwanda hiki mahsusni kabisa kilikuwa kwa ajili ya kutengeneza zana za kilimo majembe. Hatukatai kuhusu mabomba, lakini kile kiwanda kilikuwa mahsusni kwa ajili ya kutengeneza majembe na yalikuwa bora zaidi kuliko haya yanayotoka nje. Sasa leo kile kiwanda kimekuwa ni cha kutengeneza mabomba siyo majembe tena. Sasa mradi mmoja tu, sijui mradi ukiisha. maana ule mradi hauwezi kuendelea kwa miaka 80. Ukiisha ule mradi wa kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria kuja Kahama Shinyanga, wayafanya nini? Waanze kutengeneza mabomba ya kwenda wapi? Sijui!

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama tunabinafsisha viwanda, wale wawekezaji wanaokuja, basi tuwaambie jamani kiwanda hiki kilikuwa kinatengeneza majembe ya mkono na majembe ya kukokotwa na ng'ombe, basi ni vizuri yakatengenezwa majembe ya kukokotwa na ng'ombe kuliko hivi sasa kiwanda kinabadilishwa kinakuwa cha kutengeneza mabomba.

Mheshimiwa Spika, nitoe ombi kwa sababu muda unakimbia, kwamba kwa sababu Serikali ilishasema inatoa ruzuku kwenye zana za pembejeo na zana za kilimo, naomba Mheshimiwa Waziri ikiwezekana kupunguza bei za majembe ya mkono pamoja na majembe ya kukokotwa na ng'ombe, sio vibaya sana Serikali ikapunguza bei iliyopo angalau basi kwa jembe moja la mkono liuzwe kwa Sh.500/=, iwe kama ni ruzuku kwa wananchi wa Tanzania. Kwa sababu asilimia 80 ya wananchi wanatumia jembe la mkono, lakini sasa bei ni mkubwa mno Sh.2,000 kwa jembe moja.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimwombe Mheshimiwa Waziri, hili jembe la kukokotwa na ng'ombe kwa sababu matrekta hayapo, wananchi wa Jimbo la Sumve na Kwimba wanatumia majembe ya kukokotwa na ng'ombe, naomba basi na yenewe yapunguzwe bei kutoka hizo Sh.65,000/= mpaka Sh.70,000/= ziwe angalau Sh.30,000/= kwa jembe moja la kukokotwa na ng'ombe. Hii itasaidia sana kuinua kilimo cha kutumia wanyamakazi.

Mwisho, Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa sababu bidhaa nyingi zinazoingia sasa hazina ubora, unaweza ukaenda ukauziwa redio imeandikwa *Phillips*, lakini ukiitazama vizuri siyo *Phillips*, unaweza ukatazama saa imeandikwa Sanyo ukiitazama vizuri siyo Sanyo na kadhalika. Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba Tanzania isiwe sehemu ya kutupia vifaa za nje. Sasa vinaingia vitu vya namna hii. Kuna wakati unaweza kusema ni bei rahisi, lakini unanunua saa ya Sh. 2,000/= lakini ukitoka hapa kwenda kwa Spika saa inakuwa imesimama.

Wengine kwa kweli hawafahamu kwa sababu wanaambiwa saa hii ni nzuri na wanaamini kwamba hiyo saa ni nzuri kweli. Sasa tukiendelea na mtindo huu, Tanzania itakuwa ni sehemu ya kutupia bidhaa mbovu zinazotoka nchi za nje. Hili Mheshimiwa Waziri naomba sana Serikali iwe makini, ilitazame ili kusudi Watanzania wanaonunua zile bidhaa wafaidi waone ule uthamani wa fedha yao lakini vilevile wafaidi kile kitu ambacho wanunua. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja. (*Makofi*)

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo ni muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu. Kwanza, lazima ni-*declare* kwamba pamoja na kuwa Mbunge, mimi ni mfanyakishara na nitalenga biashara na naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Watanzania, tumekuwa na mipango mingi sana ya kufikiria tutakuza uchumi, tuweke viwanda vingi tunajaribu kusema vitawenza kufanya kazi. Mimi nataka kutoa mfanano mmoja nilipokuwa nafanya biashara, sasa mimi ni Mbunge. Niliwahi kwenda India nikasema, nataka kiwanda. Wana *data Bank* ambayo wanakuonyesha kila sehemu ya nchi ni wapi penye sehemu unaweza kujenga kiwanda na wamekwishafanya *feasibility study* na wanakwambia itaku-cost kiasi gani na watakutafutia na fedha za kuweza kuanza. Mtindo huo hapa kwetu hakuna. Ndiyo maana yake hata juzi nilipokuwa namsikiliza yule Mjapani aliyekuwa anatufanyia Semina hapa hakulisema hilo katika zile *tiger countries* ambazo ndiyo uchumi umefumuka na umesambaa katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, lazima sisi wenyewe tuwe *tumesha-identify areas* ambazo tumeshazifanya utafiti, hata Mtanzania akitaka, tumeambiwa mabenki yetu yana fedha nyingi sana, anakwenda pale anaambiwa hii biashara nenda pale Mwanza kuna biashara fulani au nenda Shinyanga kuna biashara fulani, kitu kinachotakiwa pale wameshakuandikia kila kitu. Hiyo ingekuwa kazi ya kwanza ya wataalamu wetu kwa mtu yejote na Mtanzania anayetaka kufanya biashara anakwenda pale kwenye Wizara anapewa kitabu na anajua anataka kwenda kufanya biashara gani na mpango wa fedha wanakufanya.

Lakini hiyo hapa kwenye nchi yetu hatufanyi na ndiyo sababu tunazidi kuwaagiza wageni wao ndiyo wanakuja kutuelekeza tukaweke wapi kiwanda wakati hata sisi hatujui. Wakati mwengine bei za kutengeneza kile kiwanda sisi hatujazifanya utafiti, unakuta wanakuja na bei mara mia moja ambayo inazidisha deni la Taifa na tunazidi kutumbukia kuwa maskini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, siyo dhambi matajiri kujenga katika nchi hii. Kama tungekuwa na Reginald Mengi kila Mkoa au katika kila Wilaya nina hakika matatizo ya ajira yangekwisha katika nchi hii. Lakini ukiritimba au kwa falsafa yake ya kusema kuwa tunasambaza fedha kwa nchi nzima, unamkopesha mtu milioni 50 unasema ataanza nazo biashara, atafanya biashara gani na Shilingi milioni 50? Shilingi milioni 50 nitafanya nazo nini? Haziwezi kufanya chochote! Ni kheri kumjenga mtu mmoja katika Mkoa akaweza kuanzisha biashara kubwa na akaweza ku-create employment kwa watu zaidi ya 2,000 na pale ndipo maendeleo yanakuja. Tutake tusitake, lakini huo ndiyo ukweli!

Hata kule America walikuwa na *Act* ambayo walipitisha ambayo wanassema *I think, Affirmative Action Policy* ambayo ni makusudi kabisa kwa kuwainua watu weusi wawe na wao matajiri kama Wazungu walivyo na siyo dhambi hapa kwetu Tanzania kuwainua matajiri wachache wakawa wakubwa wakawa ndiyo wanapunguza umaskini katika nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa la biashara ni mtaji, yaani fedha. Mheshimiwa Waziri wa Fedha alisema katika nchi hii mabenki yetu yana fedha nyingi sana za kufanya kazi, lakini wanaotaka kukopa hakuna. Sasa hebu niambie Mtanzania wa kawaiida anayetaka kukopa fedha Benki atazipataje?

Natoa mfano huu kwa sababu mimi *personally nime-experience*, naitoa wazi kwa sababu kama Philemon Ndesamburo, Mbunge, mfanyakishara ninayejulikana *nina-investment* nydingi katika nchi yetu. Nakwenda CRDB nataka kukopa Shilingi milioni 50 inachukua miezi sita halafu mwishoni naambiwa wewe ni Mpinzani, hizi fedha unataka kukopa za kwenda kufanya kampeni. Hayo ni matusi na kwa kweli *I really need an apology for that*. Kwa sababu alinitukana! Shilingi milioni 50 ni kitu gani na inachukua miezi sita! Mimi ni mfanyakishara, nasema kweli nilitoka hapa wiki juzi palikuwa na *property London, real property* inauzwa *one million pound*.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda nikamwita *Manager* akaja nyumbani kwangu asubuhi, saa sita *survey* ikapelekwa saa 10.00 akaniambia *your loan is approved*. Hapa kwetu miezi sita hata kile ulichokuwa unataka kufanya unakuta kimeshachukuliwa na wengine. Sasa hii ni *sabotage* au ni kitu gani? Kitu ambacho nataka kuuliza Serikali ni mambo yale ambayo wafanyakishara wa kawaida wanayaona na wanapata taabu na wanashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine hata nchi ya Uganda imekataa. Kuna mali zinaingia katika nchi yetu *especially* za magari, unakwenda dukani unaambiwa hii ni *genuine* na hii ni *non-genuine*. Hivi tunaingiza mali hizi hapa *non-genuine* unafunga *bearing* gari linakwenda kilometra 20 inakufa na tunasema kweli tunajenga nchi. Kwa nini tunaachia vitu vya namna hiyo? Hata Uganda wame-*ban* vitu vya namna hiyo! Kwa nini Mheshimiwa Waziri tusi-*ban* vitu vya namna hiyo? Kwa nini kama mtu ana *macedesi* aiagize *spare* kutoka Ujerumani kama una gari ya Japan, agiza zile *spare* kutoka Japan, utapata *genuine part* na tuta- *save a lot of foreign exchange* ambayo kwa sasa tunatupatupa bila sababu?

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Kwanza iliweka misingi mizuri sana ya kuweka viwanda katika nchi hii. Tulianza vizuri sana, lakini hapa katikati tukaja tukavuruga vuruga. Lakini sasa ninachosema ni kwamba bado kuna viwanda vingi na magodown mengi ambayo bado yanafaa katika kuanzisha viwanda na yamekaa tupu yanaliwa na mchwa. Tunaiomba Wizara ikayafanyie *study* magodown hayo. Natoa mfano kama pale Moshi, yapo magodown zaidi ya 10 na Mheshimiwa Waziri anajua hiyo. Tunao vijana wazuri wenye kujua kufanya kazi. Sasa hivi masofa ya viti yanatoka Dubai, lakini tuna mbaopapa hapa nchini, tuna vijana wanaweza kufanya kazi nzuri sana. Badala ya ku-*promote* watu wetu hapa nchini tuna *promote* watu wa nje, ni aibu!

Mheshimiwa Spika, *magodown* yale yapo na tunasema mikopo ipo, kwa nini Serikali isisaidie wale wenye ujuzi? Tuna watu wenye ujuzi! Tusijidanganye tukasema Watanzania ni mbumbumbu! Ni watu wenye akili za ajabu, wanaweza kufanya mambo ambayo huwezi kuamini. Kwa nini tusiwasaidie hao tukawajenga wakaweza kufanya kazi hizi na kuunda vitu hivi ambavyo tunaviagiza nje bila sababu ya kutosha na tuka-*create employment?* *The all problem* ni ku-*create employment* katika nchi hii ili vijana wote wapate kazi. Watu wakishapata kazi watapata kula, matatizo yatakwisha, hakuna ugomvi na mambo yatakwenda vizuri. Haya mambo yanatia uchungu sana.

Mheshimiwa Spika, unakwenda katika hizi Benki zetu ambazo ndiyo *institution* ambazo ndizo tunazitumainia kutoa fedha, Mameneja wamekuwa ni ma-boss wanakaa ndani. Lakini katika nchi za nje yule mwenye pesa ndiyo *boss* wanatoka Maofisini wanakuafuata wewe Ofisini kwako. Sijaona *Bank Manager* wa hapa anayekwenda kumtafuta mteja kumwambia wewe una fedha tukufanyie nini?

Mheshimiwa Spika, naweza kuisifia Benki moja tu, nadhani *Standard Charter*. Ni Benki yenyе watu wanaoweza kwenda kuwafuata wateja na kuwauliza tufanyie nini na fedha zako. Au ukitaka hata *overdraft* kwao haichukui mwezi. Lakini wenzetu *NBC*, mimi nilikuwa nafanya biashara nao, lakini sasa nimesema potelea mbali nawaambia kweli miezi mitatu baada ya kuona hao watu hawafanyi kazi yangu vizuri, nikasema funga akaunti yangu *personally* mpaka leo miezi mitatu hawajanipa fedha yangu. Nikawaambia hata na ile akaunti mama ya kampuni yangu nafunga. Nitafunga nitakwenda kwa watu ambao wanataka kufanya biashara, kwa sababu Meneja wa Benki kazi yake ni kwenda kutafuta wateja nje.

Mheshimiwa Spika, nikienda Benki Meneja wa Benki siyo *boss* wangu, mimi ni *boss* wake na waelewe hivyo na wafanye kazi wakijua hivyo, sisi ndiyo ma-boss! Unamkuta meneja Ofisini anakaa tu, unaingia anakuangalia. Unaniangalia nini? Mimi *boss*! Maana yake kuna *competition* ya Benki hapa nchini! Halafu wengine ni wahuni, unakwenda unakopa fedha katika Benki anawekea *condition*, huwezi kufungua akaunti kwenye Benki nyingine.

Nchi hii ni soko huria, hebu Mheshimiwa Waziri wa Fedha awapelekee *circular* waache huo ujinga. Unamwambia mtu asifungue akaunti kwenye Benki nyingine, unaning'ang'ania mimi tu, halafu ninayotaka hunipi! Haya ndiyo mambo yaliyoko hapa Tanzania jamani na ndiyo kitu kinacholeta umaskini katika nchi yetu, lakini fedha tunaambiwa zimejaa Benki.

Mheshimiwa Spika, nani aende? Philemon Ndesamburo nakatazwa kukopa Shilingi milioni 50, nani aende akakope apewe? Au kwa kuwa mimi ni Mpinzani? Maana alinijibu akaniambia wewe Mpinzani unakopa fedha za kampeni. Ala, Shilingi milioni 50 za kampeni! Mimi nitakopa za nini wakati watu wa Moshi wanantaka wenywewe. (*Makofu/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, halafu nina fedha Shilingi milioni 160 wamechanga CCM, nikawaambia wale wanataka tena nyingine za nini? Wamekwishapanua midomo hivi hivi wanangojea kula zile fedha. *Alhamdullilah*, mimi nashukuru Mungu wamekwishanifanyia kampeni wamemaliza, kazi imekwisha. Tunataka tuwe wastaarabu, tunataka tuendelee.

Kama ni mfanyabiashara ujivunie uwe mfanyabiashara kama Mwamerika alivyo anafanya biashara na ukitaka kukaa kwa raha wanasema "kama wewe mwanaume oa mwanamke wa Kijapani kwa sababu ukirudi saa saba usiku hatakuuliza. Weka mpishi wa Kichina atakupikia hata majani utakula utafurahi. Nunua gari ya Benzi ya Kijerumanii

kwa sababu hata ukipata ajali hutakufa. Halafu jenga nyumba kubwa ya Kimarekani sasa hapo mwisho wa maisha. Mambo sasa safi. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumalizia hapo. Naunga mkono hoja hii. (*Makofi/Kicheko*)

MHE. MWANNE J. MCHEMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niwapongeze Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa, Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mama Rita Mlaki kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Pia, nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii, Ndugu Nyachia na watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kazi ambayo imeleta mwelekeo mzuri wa hotuba iliyopo mbele yetu.

Nianze kwa kuunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Awali ya yote nianze kwa kuchangia suala zima la kuhusu *SIDO* ingawaje litakuwa kama linajirudia, lakini kwa mtazamo tofauti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuliona Shirika la *SIDO* kwamba ni kiungo kikubwa na ni kiungo cha MKUKUTA. *SIDO* imeanza kuijua MKUKUTA mapema kabla ya haijaanza kusambaa kwa sababu *SIDO* inafanya kazi nzuri sana Mijini tu. Hapo sasa inafanya kazi nzuri sana Mijini na inatoa mikopo mizuri sana Mijini. Ningombaa ili iweze kusomeka vizuri na iweze kueleweka vizuri, *SIDO* ifike hata Vijijini. Kwa sababu *SIDO* ni mkombozi wa wananchi wa Tanzania wa kipato cha chini wanawake na wanaume *SIDO* inawakopesha

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na kuwakopesha huko. Mikopo inayotolewa ni midogo sana. Kila unapouliza, wanakwambia ufinyu wa bajeti. Sasa kama ni ufinyu wa bajeti, ni vizuri Mheshimiwa Waziri akakubaliana na mimi kwamba ashirikiane na Waziri wa Fedha ili lile wazo na utafiti wanaofanya kwa ajili ya kuanzisha Benki ya kuwakomboa wafanyabiashara wadogo wadogo sasa ipitie *SIDO*. Ningombaa sasa ipitie *SIDO* kwa sababu *SIDO* tayari wana uzoefu na wana wataalamu waliobobe. Nimpongeze sana Meneja Mradi wa *SIDO* wa Mkoa wa Tabora, naye pia amefanya kazi nzuri sana kwa Mkoa wa Tabora kiasi ambacho mpaka sasa kwa kweli ningekuwa na uwezo wa kumpa fedha ningempa mimi mwenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kweli mtazamo huo wa kuwakopesha wananchi laki moja, laki mbili au laki tano imepitwa na wakati. Tunao pia wafanyabiashara wakubwa ambao wanahitaji mkopo zaidi ya Shilingi milioni moja, hawapati kwa sababu hawawezi kwenda kukopa Shilingi laki tano wakati mahitaji yake ni milioni moja au mbili. Ningombaa bado kusisitiza Wizara hii iangalie namna ya kutenga fungu maalum kwenye bajeti hii, kupunguza sehemu nyingine kuongeza *SIDO* ili iweze kufanya kazi nzuri iliyokuwa imetarajiwaa.

Mheshimiwa Spika, pia niipongeze *SIDO* kwa kuandaa maonyesho ya Kanda. Walianza na Mkoa wa Tabora, wakafanya vizuri sana yale maonyesho ambayo yalikuwa yameongozwa na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Akinamama na akinababa walijitokeza. Lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba maonyesho hayo yanakwenda kwa Kanda na kama katika Kanda kuna umbali wa kusafirisha zile bidhaa, wengi wanakwama kwa sababu hawapati faida.

Ningeomba pia, kama kuna uwezekano wa haya maonyesho, basi Wizara ingetusaidia pia angalau kutenga fungu maalum la kuwasaidia hawa akinamama na akinababa kuhusu usafirishaji wa bidhaa zao. Gharama zake ni kubwa sana kiasi ambacho wanaoshiriki haya maonyeshi ni wachache. Kama ndiyo hivyo basi, hawa wanaoshiriki haya maonyesho wakopeshwe fedha nyingi kama alivyokiri mwenyewe Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake kwamba mikopo inarejeshwa ambayo wanakopa kwa asilimia kubwa. Kwa hiyo basi, ili wasivunjike moyo, ni vyema wakaangaliwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la elimu inayotolewa na *SIDO* kuhusu usindikaji wa matunda na mazao mbalimbali. Namshukuru pia Waziri kwenye hotuba yake amekiri kwamba Watanzania asilimia kubwa wamekuwa na elimu ya kusindika matunda hayo ya asili na pia mengine ya kawaida. Tatizo lililojitekeza ambalo ni gumu ni elimu kuhusu *TBS*. Wananchi hawa wanaosindika matunda haya wao wanajua tu kwamba amefundishwa kupaki yale matunda, amefundishwa kupaki chakula na matokeo yake mtu anajua kwamba akitoka pale ni moja kwa moja anakwenda kutembeza ile biashara.

Sasa kwa wakati huu ni vizuri elimu hizi zikaenda sambamba. Waziri ashirikiane na kitengo cha *TBS* ili wajue jinsi gani ya kuwasaidia hawa akinamama ambao wamezamisha mtaji wao kwenye zile biashara ambazo tayari wao wanajua kwamba ziko sokoni. Lakini wanapopeleka nje ya eneo lao inaonekana kwamba hazina kiwango cha *TBS*. Kwa hiyo, hakuna ile nembo. Sasa tunawasaidiae?

Mheshimiwa Spika, mtaji wameshauzamisha mle, soko halipo na matatizo ya *TBS* ni makubwa. Ningeshauri Serikali iangalie jinsi gani *TBS* inaweza kuwa na matawi kwenye maeneo husika ambayo asilimia kubwa ya akinamama wanafanya kazi ya kusindika hayo mazao, kwa sababu yanakuwa ni matunda ya aina nyingi, atatoa aina moja ya chakula anapeleka *TBS* inakaguliwa, kesho anabuni tena kusindika matunda mengine anapeleka *TBS* nayo ni Makao Makuu. Kwa hiyo, naomba hili Serikali iangalie jinsi gani ya kuwasaidia hawa akinamama ambao tayari wameshakuwa na elimu waliyopewa na *SIDO* kuhusu kusindika hizo bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, pia *SIDO* hiyo hiyo, kwa sababu mimi nataka nizungumzie suala zima la *SIDO*. Kuna maonyesho yanayofanywa kwenye Uwanja wa Saba Saba hivi sasa Uwanja wa Hayati Baba wa Taifa. Ni kitu cha ubunifu kwa Mtanzania. Ubunifu huo mimi mwenyewe nimekwenda nimeona kuna ubunifu wa mashine ya kufyatulia matofali ambayo amebuni mtaalamu mmoja Mtanzania ambaye haina vikorombwezo vingi kiasi ambacho hata mtu wa chini anaweza kununua na ikafanya kazi. Ni vyema

badala ya kumwacha yeche akahangaika kutafuta soko, Wizara hii imsaidie kutafuta soko kwenye maeneo ya ujenzi mbalimbali hususan *NSSF* ambako kila Mkoa wanakwenda wanajenga majengo yao ili hawa watu kipaji chao kiweze kuendelea.

Lingine ambalo nimeliona la ubunifu ni mashine ya kutotolea vifaranga ambavyo imetengenezwa na vijana wadogo sana pale *SIDO*. Hawa vijana wamebuni mashine zile. Ni vyema tena Wizara ikasaidiana pamoja na kwamba imejitoa kwenye masuala ya masoko na masuala mengine, lakini bado ni dhima ya elimu waliyoipata. Ubunifu wao ili waweze kupata masoko kwa kutumia hao hao *SIDO* chini ya Wizara mama ambayo watakuwa wametangaza na wawasadie wale vijana kutoa kwenye matangazo ya aina mbalimbali kwa mfano TV hata redio ili haya masoko yao yaweze kueleweka Tanzania nzima.

Pia, kuna mashine ambayo ilionyeshwa Tabora kwenye Maonyesho ya Wiki ya Ushirika na Masoko ambayo ilitengenezwa na *CARITAS*. Mashine hii ni kama friji ya kienyeji. Hizo friji za kienyeji jinsi alivyotengeneza yule kijana mbunifu, inagandisha kabisa kuliko friji za kawaida. Sasa Wizara ya Viwanda na Biashara inawasaidiaje watu kama hao wenye vipaji maalum ili elimu yao iweze kutumika hapa nchini?

Mheshimiwa Spika, lingine naomba niwapongeze hususan Wakala wa *BRELA*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ukurasa 45 amezungumzia kwamba wanafanya kazi kati ya siku tatu na tano. Mimi nakiri kwamba wanafanya kazi nzuri chini ya uongozi wake wa Ndugu Mahingira. Ni kweli wamefanya kazi nzuri ambayo wafanyakazi wengi na wafanyabiashara wamekiri kufaidika na Wakala huyu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba pia kama kuna uwezekano, ningeishauri Serikali au Wizara hii itusaidie pia kupeleka hata Mikoani. Kuwe na matawi Mikoani ili waweze kufanya kazi nzuri kuliko kila mfanyabiashara kwenda mahali hapo. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niende haraka haraka. Suala lingine ni haya matatizo ya viwanda. Ugomvi na migogoro inayokuwepo kwenye viwanda ambavyo vimefufuliwa, Wawekezaji watatukimbia. Ni vyema Wizara hii ikasaidia kuyatatua yale matatizo. Juji wamegoma; sasa mwekezaji mwengine wa nje ya nchi akiona, atakuja! Kwa hiyo, uwekezaji utakuwa na mushkeli kidogo. Naomba haya masuala madogo madogo yaliyotokea *Shoprite* yaangaliwe, yaliyotokea Kiwanda cha Nguo yaangaliwe ni matatizo ambayo yanaweza kuathiri uwekezaji wetu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kiwanda kinachotengeneza khanga, samahani nimekisahau. Kuna Kiwanda ambacho kinatengeneza khanga sio kwa kutumia pamba ya Tanzania, inatumia malighafi ambayo inajua yenewe. Khanga hizo zinaitwa “Tereza”. Mama wa Kijiji akivaa inadondoka, ukiishika bahati mbaya nimekisahau nilitaka kuja kuionyesha *sample*. Ni khanga ambazo Mheshimiwa Waziri naomba mziangalie. Akinamama wanapata taabu sana na hizi khanga. Kama ni mtandio iitwe mtandio, lakini isiiwtwe khanga wakati ni mtandio.

Naomba *TBS* iangalie kuna tatizo gani kati ya hicho kiwanda. Akinamama hatujui kujifunga hizo khanga zinazotereza. Wao wanaita mali ya “Tereza”, “Tereza” yuko wapi? Kuna “Tereza” hapa? Kwa hiyo, tuangalie ni jinsi gani Serikali itaangalia hicho kiwanda kuhusu hizo khanga za kuteleza. Mheshimiwa Waziri nitakupa baadaye kwa sababu mimi ninayo uone kama unaweza kujifunga.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niombe kwa hayo niliyoyaomba na nimwombe Mheshimiwa Waziri ayafuatilie pamoja na Wataalamu wake. Kwa heshima na taadhima, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe na kukushukuru. Uliniita kwa bahati mbaya nilikuwa na ugeni hapo nje nilikwenda kuperuzi kidogo hotuba ya mwaka jana ili nisirudie leo. Kwa sababu kuna tabia ya mdudu mmoja anaitwa furuiri kule nyumbani, kama mvua inanyesha inatokea vidudu fulani vinazunguka hapo hapo tu, sasa nisionekane mimi nazunguka pale pale.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameonyesha nidhamu moja ya kubadilisha msimamo, mwelekeo na vile vile mwelekeo wa bajeti yake, sisi Morogoro tunamwita ndio *tall* wetu. Ndio mrefu kuliko wote, baada ya *Father Shaweji*. (*Makofi/Kicheko*)

Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Watendaji wake kwa kutuletea bajeti ambayo ina *vision*. Kwa kweli hakuna vijembe, ni kumfagilia tu kuonyesha mapungufu machache ambayo yalijitokeza yale ambayo tunayaona atayachukua. Kwa sababu tunaona ana Jimbo, kwa hiyo, ni kumwombea tu kwamba kwa hali walivyofanya yeze na Naibu Waziri wake, tunawaomba wamuweke Mungu mbele, umma kati Majimbo yeo yawarudishe. Wamefanya kazi nzuri sana katika Bunge hili. Hizo vurugu vurugu zinazotokea kwenye Majimbo yeo ni kwamba wenye akili wanajua mmeefanya nini. Ahsante sana na nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nimesema kwamba ukisisitiza sana kitu unapoteza maana. Kwa sababu mtu ukisema bara ni *Continent* na sio maana ya kusema barabara maana yake umesisitiza, hapana; barabara ni njia. Ukimfariji mtu ukamwambia pole, basi maliza hapo hapo. Usiseme polepole, polepole ni kwenda taratibu. Ukimtibu mtu ukisema tibu ni kutibia mara moja, sasa ukisema mara mbili unaweza kusema tibutibu ni kuharibu.

Baada ya kusema hayo, nasema kabisa kuna vitu vingine nitavieleza hapa vitakuwa havina msingi wowote, lakini vinaleza nidhamu ya Watanzania jinsi walivyo katika kuitekeleza nchi yao. Lakini vitu vingine vilikuwa havina maana kwa sababu vinafariji, vinaongeza tija, vinaongeza msimamo ingawaje havina umbo, wajih, harufu wala rangi.

Baada ya kusema hayo basi, kwa mfano kuna vitu vinakata lakini havikatiki, kama kukata tamaa; kuna vitu vinavunjika lakini havivunjiki, kama kuvunjika moyo;

kuna vitu vinaliwa lakini havishibwi, kama kula kiapo; kuna vitu vinapigwa lakini haviumii, kwa mfano kupiga kura na kuna vitu vinachapwa lakini haviumii kama vitabu. (*Kicheko*)

Baada ya kusema hayo ya utangulizi, kuna mambo yatajitokeza kwenye hotuba yangu mtakuwa mnayaona. Naanza na kitu kinaitwa *VIP Treatment* kwa watu ambaao ni wageni wanaofanya biashara katika nchi hii. Kwa nini mnawaacha Watanzania wafanyabiashara pamoja na kuunda Vyama vyao lakini mfanyabiashara mkubwa anaibuka kutoka nje anakuja hapa nchini anakuletea machungwa yake kutoka nchi za nje anakuanzishia *Shoprite* unaacha machungwa ya Matombo na kule Mkuyuni? Ile *VIP Treatment* sio nzuri kwa wageni wafujao uchumi wetu.

Narudia tena. Mwaka jana 2004 niliposimama hapa nilieleza mwanaume mmoja alivyoahdirika. Alikuwa anaangalia *TV* na wanawe. Wakati anaangalia, akasema nakwenda kuoga. Kwenda kuoga kurudi watoto wakamwita haraka: “Baba, kipindi unachokipenda Isidingo.” Baba ilibidi aachie kuoga akavaa taulo lake na shati, akasema nipo na wanangu. Yuko na familia yake chumbani pale anaangalia *TV*.

Mheshimiwa Spika, Isidingo sio kipindi kizuri sana. Akatokea mwanaume mmoja hana nguo, yule baba kuona huyu anatoka bila nguo akavua taulo lake kufunika ile *TV* ye ye amebaki vile vile. Utaratibu huo sio mzuri. Unahifadhi picha ya *video* isionekane ili kusudi uumbuke wewe. Acha siasa hii Tanzania, heshimu Watanzania kwanza wavalishe nguo. Msivue mataulo kufunika televisheni. Ahsante nashukuru sana. Sasa hivi mmelewa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lingine kuhusu viwanda vinavyokuja kwa upande wa *EPZ* bado sijafurahi. Nimesema kwenye ile sheria kwamba kuna watu ambaao wanakuja kuwekeza kujifanya kama ni Malaika wa ajabu watawawekeeni maviwanda makubwa, watachukua wafanyakazi kama 3,000 au 4,000 na kwenye takwimu hizo pia zipo. Nimetoa wafanyakazi 2,300 wa kule *SOMAS* na wale wa kiwanda cha kule sehemu za kule Tabata. Nimepata *figure* tofauti ambayo nitampatia Katibu Mkuu. Kwa sababu wale wamekuja ku-beep uchumi wetu. Nasema Tanzania haibipiki kwa uchumi. Sasa hivi kuna wataalamu wamekaa kule nao inawaudhi kwa sababu kuna watu wahuni wanatuzidi kete.

Hivyo basi, baada ya kuitisha hoja hii, simamieni vizuri Watanzania, wafanyabiashara, walaji, tuwe pamoja na Wizara hii ili kuwasaka hawa ambaao wana matatizo kama yule paka aliyesilimu. Kuna paka mmoja siku moja alichukua tasbihi, alikuwa hajui na angewauliza Waislamu mnasemaje mkishika tasbihi? Akashika tasbihi, lakini tasbihi hiyo ilikuwa dagaa. Akatunga dagaa kama mia mbili akawa anasemasema ovyo tu, paka nimesilimu kwa hiyo najilaumu tena Uislam mgumu kila siku saumu. Ni maneno aliyokuwa anasema kwenye tasbihi. Kwanza ni dhambi, sio maneno hayo wanasema Waislam.

Baada ya kusema hivyo, panya walishangaa wakauliza; kwa nini unashika dagaa na unalipenda? Akasema, si ninasilimu situmii dagaa wala panya. Panya akamwambia,

kweli? Akasema kweli. Basi panya wote duniani wakamvamia paka kwa kumshangilia wakasema mtaniua nitakosa hewa jipangeni msitari. Kujipanga msitari amewasalimu hujambo, sijambo, hujambo, sijambo wa mwisho akamwuliza wewe ndio wa mwisho akamkamata huyo huyo akamla. Wale wengine walikuwa hawana habari. Walipita mipito kumi na mbili, panya kumi na mbili wakapotea.

Panya wale wakaamua kwamba sasa tunaliwa tunamalizika, kwa hiyo, twende kinyumenyume tuone kinachotokea. Hii ndio hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara kwamba tumeamua sasa Watanzania twende kinyumenyume tuone kinachotokea. Tuliliwa tulikuwa hatuangalii nyuma. Hotuba hii inawafanya Watanzania walaji na wafanyabiashara wote wa Tanzania twende kinyumenyume tuangalie kinachotokea. Tutayagundua tu! Kwa sababu mwaka wa nzige panzi walikula. Pulizia maji utayakuta kwamba panzi nao walikuwemo ingawa tuliita mwaka wa nzige. Tutawapata tu Mheshimiwa Waziri.

Kuna viwanda vipyta vinavyokuja na mambo ambayo yanaleta bidhaa kutoka nje kusindika malighafi. Kwa nini malighafi zilizopo hapa zipigwe marufuku? Pamoja na utandawazi, lakini sio kwamba tumefungulia mlango wa kuleta kila kitu. Utandawazi utakuwa na nidhamu zake. Ndiyo ile inaitwa *Anti-dumping*. Nilidhani *Anti-dumping* ni kuzuia vitu kama hivyo, kumbe ilikuwa kuzuia bei tu!

Kwa hiyo, *Anti-dumping* ingeingiza na mambo kama haya ya kuagiza bidhaa za mbali kutoka nje kama bidhaa za Kiwanda cha Matunda kinataka matunda ya kutoka Vijiji kule Luholole, Changa, Kibwaya, Mfumbwe, Logo, Uponda, Mifuru, Hewe, Bwagiro, Nyamigadu, Mkololo, Pumba, Amini, Ludewa, Burugi na Lung'ala, basi chukua matunda huko huko. Kama kitu kinatoka Kijiji cha Kabingo Ukerewe chukua huko huko. Kama kinatoka Iganiga Nzega au Pangagani Pemba au Kwabiro Ulanga watumie huko huko waliko. Wasitoe vitu kutoka nje kuvileta hapa! Huko ni kuweka dawa viatu wakati haviumwi au kukuna nazi wakati haiwashwi. (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, *SIDO* nimefurahi sana, kuna mikopo inatolewa na *SIDO*. Wakati mmoja vijana walikuwa vikundi kama 120 katika Jimbo langu maeneo ya Ngerengere, vikundi vitatu; Mkuyuni, vikundi vitano na Kiloka, vikundi sita. Tulifanikiwa angalau kupata mikopo hii. Lakini walipotaka waongeze ule mkopo uwe mkubwa zaidi, nikawaambia kwa kweli katika *SIDO* hakuna mkopo wala galoni, ni hizo hela ndogo ndogo tuamini. Kwa hiyo, Serikali iimarishe Mfuko ule.

Upande wa *TIRDO*, *CAMATEC* na watu wengine wa *TEMDO*, tunafurahi sana kwamba kwa upande wa *TIRDO* wameamua kuwa na *plan* ya kuondoa MKUKUTA, tayari tulikuwa tumeandaa toka mwaka jana 2004. Naomba ni-*declare interest*, mimi ni Mjumbe wa Baraza la Wadhamini la *TIRDO* kwa sababu ya wadhifa wangu nilipokuwa *Chemist*. Mimi ni Mkemia kwa taarifa. Sasa nimepelekwa kule na Waziri kwenda kuangalia mambo yale na tunakwenda vizuri tu. Sasa naomba Idara nyingine hizi kama *CAMATEC* na maeneo mengine waeleze utaratibu wa jinsi ya kutumia huu mfumo wa MKUKUTA halafu uletwe nadhani Mheshimiwa Waziri ameshapewa tayari. Lakini

tupate na sisi ili Wabunge tuone kwamba kila Idara kama Wabunge sio kama *Board Members*.

Halafu lingine, ningependekeza kwamba haya Makampuni yanayotajwa hapa katika ibara ya 99, kama vile *TIRDO*, *TEMDO*, ningependa Wakurugenzi wao na Wenyeviti wao wangkuwa wanakuja kusikia hotuba zetu ili kusudi wanaporudi kwenye Bodi za Wakurugenzi waende kuwaambia walichokivuna huku. Kwa sababu wasiwe wanatuona kwenye *Star Television live* lakini kuyapata kutoka kwa Mbunge na kuyapata kutoka kwa Mwenyekiti au kwa Mkurugenzi inakuwa ni vizuri zaidi. Watakuwa wanaeneza kwenye maeneo yao ili kusudi waweze kuyapata hayo na wanapofika hapa inakuwa hali nzuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu ubadilishaji wa aina ya viwanda. Nimesikitishwa kwa kweli kupata taarifa kwamba kumbe kiwanda kile cha *UFI (Ubungo Farmers Implements)*, ambacho ni Kiwanda cha Zana za Kilimo, sasa kinabadilishwa kinakuwa Kiwanda cha Zana za Bomba. Kwa kweli, hiyo iwe *temporary* tu. Lakini vifaa vya kilimo tutapata wapi? Kwa sababu sasa hivi kuna majembe yanayoletwa kutoka nchi za nje yanavunjika ovyo, hata akilimia mtu mwepesi kama mimi linavunjika tu. Kwa vile *standard* ilitakiwa kama Mheshimiwa Msindai akishika likivunjika, hapo kweli.

Lakini mtu kama Semindu Pawa nalo linavunjika! Sasa majembe haya ya aina gani? Hawajui Watanzania tunalima mahindi ya kule kwenu Mheshimiwa Waziri sehemu za Mvingu kule kwenye Jimbo lako Ulanga kwenye miti kama ile huwezi ukachimba!

Kwa hiyo, tungeomba kabisa watu wa *CAMATEC* na watu wa *TEMDO*, *TIRDO*, *SIDO* na *TBS* wapime majembe, sio wapime *wa-samples* haraka haraka tu ghafla ghafla kwenye maduka na kuangalia halafu wayatupe. Tupilia mbali, nakwambia kabisa tena wapime kabla hayajaingia nchini hapa. Sasa kulikuwa na utaratibu upimaji wa kuvizia kwenye meli. Unafuma tu unapima pale bandarini unawaambia yasiingie nchini kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, halafu kuhusu ushirikishwaji wa vijana na akinamama katika vikundi, tungependa akina mama washirikishwe katika vikundi ili kusudi wawe na ujuzi mzuri. Nimetembelea kule kwenye viwanja vya Saba Saba nilikuomba ruhusa ya siku moja na nusu lakini bahati mbaya nimeongeza nusu, nilidhani basi ningehesabu mpaka usiku. Sasa nusu ilikuwa jana, sasa ilikuwa imekwisha na nimeombia radhi na nimeandika barua kwako.

Nilikuwa Saba Saba nilialikwa kule. Kule nimeona kwa kweli akinamama wa kutoka kila Mkoa. Safari hii ilikuwa safi sana! Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote, Mfuko wa Mama Mkapa ulifanya utaratibu mzuri sana kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara. Waliwapanga akinamama wa Mikoa yote! Kila Mkoa unakuta mambo yao pale. Sasa wale ambao walitengeneza vitu vyao vizuri nikawauliza, mnayo hatimiliki? Walikuwa hawana hatimiliki.

Halafu nikamwita bwana mmoja anaitwa Mtoto wa Unga, naona yupo, alinielimisha vizuri sana. Kwa hiyo, nikaona sasa hivi Watanzania wameamka, wanaandikisha hatimiliki zao za ugunduzi, sio hizi pamoja na mambo kama Twanga Pepeta, akina nani wale, nyimbo zao na kadhalika, kwa hiyo, wanaamua kuandika hatimiliki. Karibuni vikundi 700 vimeorodheshwa na kuandikisha hatimiliki zao. Nimefurahi sana kwamba nilikuwa nimepata moja ya mambo ya kuzungumza hapa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimesema kwamba katika mkakati huu ambao tuliambiwa juzi kwenye Semina, tulisema tutakwenda pamoja katika *Mini Tiger Plan 2020*. Tunaanza sasa hivi, tutakwenda kama mtoto anatoa viroja. Lakini kama mtu mzima kama mimi natoa changamoto, kwa hiyo, matatizo yetu tuyafanye changamoto. Kama mzee anatoa usia, kwa hiyo, kitu muhimu cha kufanya ni udhibiti wa jinsi ya utekelezaji ili kumwinua Mtanzania. Mambo haya ya kufanya ni kama yafuatayo:-

Kujituma, kujiamini, kujifunza kwa wenzetu, kujitangaza vizuri, kuwa makini na kuwajibika. Baada ya kufanya hayo, Tanzania itakuwa mbele. Kwa sababu uhuru tuliuopata tumesema tumepata uhuru kutaka kumwendeleza Mtanzania, hatukupata uhuru kutaka kusaidia nchi nyingine ambazo ziko jirani.

Leo imenisikitisha kidogo kwenye taarifa ya habari, kuna Balozi wa Pakistan amesema kwamba alikuwa hajui kama hapa kuna kitu kinaitwa majani ya chai, kwa sababu wanapokea majani ya chai kutoka Mombasa Kenya ya kwetu yanapitia Kenya. Hiyo ni kumpa sifa mwingine. Ule ni mfumo tochi, unamulika kwa wenzako lakini kwako unabaki na giza. Naomba tafadhali sana kuwe na *main set*.

Nyingine katika Kiwanda, kwa mfano watu kama Nyumbu kuna teknolojia ya hali ya juu sana. Naomba ile *TAMCO* iliyokuwa zamani ikitengeneza matrekta ya *Valmet* pale Kibaha, zungumzeni sana *TAMCO*, *Scania* na vitu vingine. Nadhani sasa pale pamekuwa *item*. Changamkieni, wapelekeni Nyumbu pale wawe na Wawekezaji wengine ili kusudi watengeneze matrekta na kutengeneza vitu vingine vidogo vidogo ambavyo vinawenza vikasaidia.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kwamba, mara nyingi wanaozungumza kwa takwimu husifiwa na wanaowasiliza na wanaambiwa kwamba wamefanya utafiti. Wale wanaozungumza kwa maneno na soga na maneno mengine, wale huwa wanalaumiwa wanapotereza mdomo. Lakini wanaopata sifa za takwimu mara nyingi wanapokwenda kuzisoma wakati mwenyewe hayupo wakikuta takwimu si sahihi, hulaumiwa wakati wenyewe hawapo, hivyo hawana muda wa kujirekebisha. Lakini wanaozungumza kwa kutumia maneno, mara nyingi hukosolewa hapo hapo, wanasema hapo sio balabala ni barabara. Sasa hupata muda wa kujikosoa pale pale.

Tumepata takwimu zenu na za Wizara mbalimbali tutakwenda kuzisoma. Tutakosoa kule kule, lakini hatutawakosoeni, tutaoa maelekezo, mtuletee majibu ya kimaandishi na sisi tutawapelekeeni kimaandishi. Tuna hakika tatarudi asilimia 99, wasiorudi ni wale tu ambao hawagombei Majimbo. Asilimia 99 tunarudi. (*Kicheko/Makofsi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naamua kuunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante. Nashukuru sana. (*Makofifi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyowasilishwa mezani, mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu wake pamoja na watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii kwa umahiri mkubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pili, kwa lengo la kuboresha hoja hii naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

(i) Kiasi cha bajeti ya shilingi 14,774,569,000/= matumizi ya kawaida na shilingi 1,626,000,000/= za maendeleo ni kidogo sana ukilinganisha na hali halisi. Kwa nini Serikali isiangalie masuala ya viwanda kwa mapana zaidi. Viwanda ambavyo vingetiliwa mkazo hasa vijijini ni pamoja na kusambaza teknolojia ya kuzalisha umeme kutokana na kinyesi (*biogas*), mitambo ya uzalishaji nishati kutokana na kinyesi cha wanyama kitaleta mabadiliko makubwa katika kuleta maendelo vijijini. Nashauri kila kijiji chenye mifugo, Wizara kupitia *Carmatic* wajengewe mtambo wa *biogas* wa kielelezo.

(ii) Mheshimiwa Spika, utamaduni au mazoea ya kujenga viwanda kwenye miji ya Dar es Salaam, Mwanza Arusha na Tanga ni hatari sana kwa maendeleo. Nashauri kila mkoa angalau ungekuwa uasili wa eneo husika kwa mfano viwanda vyta kutengeneza sigara vingejengwa Tabora, Iringa na Ruvuma.

(iii) Mheshimiwa Spika, biashara kati ya Msumbiji na Tanzania ni bubu, hakuna mfumo rasmi unaosimamia biashara hiyo, Serikali inachukua hatua gani ili kuhalalisha mfumo huo.

(iv) Mheshimiwa Spika, mwisho namwomba Mheshimiwa Waziri, aeleze utaratibu unaotumika wa kuingiza sukari kutoka nchi jirani kwa mfano kutoka Malawi bidhaa ambayo inatumwiwa kwa wingi na wakazi wa Mbinga.

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi wanayofanya. Pamoja na pongezi hizo napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa nchi yetu pamoja na nchi kadha za Afrika zimepewa fursa ya kushirik katika masoko yanayitolana na Sera za *Everything but Arms (EBA)* na *AGOA* za Jumuiya ya Ulaya (*EU*) na Amerika na kwa kuwa takwimu zinaonyesha kuwa *exports*

yetu katika soko la *EU* na *AGOA* bado yako chini sana, je, ni sababu zipi za msingi pamoja na jitihada zote ikiwa ni pamoja na kutenga *EPZ*?

Je, sasa tuna mkakati upi wa makusudi kuwa Watanzania wananaufaika na mipango hiyo ambayo hatuna hakika kama itaendelea baada ya mwaka 2008 kutokana na maamuzi ya *WTO*?

(ii) Kwa kuwa ajira inaendelea kuwa adimu katika nchi yetu, na kwa kuwa vijana wetu wengi wanahitimu kila mwaka katika taaluma mbalimbali, je, Wizara ina mpango na mkakati gani wa makusudi kuhakikisha *category* ya kazi fulani fulani katika viwanda vyetu inahifadhiwa kwa ajili ya Watanzania wenyе sifa tu?

Mheshimiwa Spika, uzoefu wangu ni kuwa nchi nyingi zilizoendelea ambao ndio wataalam wa *Free Market Economy* hawaachii tu nafasi za ajira kwa wageni. Ili kupata ajira katika nchi hizo ni lazima kupitia taratibu zilizo ngumu kweli kweli. Kwetu uzoefu unaonyesha kuwa kila mwekezaji anao uwezo na haki ya kuleta wafanyakazi wake toka nje. Serikali inatoa kauli gani na utaratibu gani wa makusudi kuhakikisha kuwa watumishi wa viwanda vyetu wa Watanzania isipokuwa tu pale utaalam husika au uzoefu unathibitika kweli haupo katika nchi yetu.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja maafisa, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa kuwasilisha bajeti yao nzuri na yenye mwelekeo wa kimaendeleo ya nchi yetu kuwa yenye mafanikio makubwa katika masuala ya kiuchumi na kimaendeleo katika karne hii ya ishirini na moja ambayo ni karne ya sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, sambamba na bajeti hii nzuri yenye kuthibitishwa na uongozi unaosimamia Wizara hii pamoja na wataalamu wao, naomba kwa Wizara hii kuongeza jitihada zake ili kuweza kufanikisha mipango na malengo yaliyopangwa katika Wizara hii katika ujenzi wa uchumi wetu wan chi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, nikinukuu hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa kumi na mbili, unaelezea juu ya sera ya viwanda vidogo na biashara ndogo, tunaelezwa katika hotuba hii kuwa Sera ya Viwanda vidogo na biasahra ndogo (*SME Policy*) iliandaliwa na Wizara na kuidhinishwa na Serikali na pia kuzinduliwa rasmi.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kumwuliza Mheshimiwa Waziri na Wizara yake hii ya Viwanda na Biashara, je, sera hii wamiliki wa viwanda vidogo na hawa wafanyabiashara ndogo ndogo pamoja na wananchi kwa ujumla wanaielewa? Kama wahusika hawa hawalewi sera hii, kuna mpango gani kwa Wizara na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwaleza wahusika hawa juu ya sera hii ya viwanda vidogo na biashara?

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuuliza kuwa katika sera hii kwa upande wa biashara ndogo inasemaje au pia inafanya nini kwa vijana wetu wanaojishughulisha na biashara ndogo hapa nchini. Vile vile sera hii imewasaidia viyi vijana wetu na wananchi wote kwa ujumla wanaojishughulisha na shughuli za biashara ndogo hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kuuliza, je, ni mafanikio gani na ni matatizo gani ambayo yamepatikana katika kuifanikisha sera hii ya viwanda vidogo na biashara ndogo kutekeleza mipango na malengo yake iliyopangiwa?

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 33 wa hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, tunaelezwa juu ya Dira ya mwaka 2025, Serikali imeandaa Sera ya Taifa ya Biashara ambayo ilizinduliwa rasmi mwezi Agosti, 2003. Ni matumiani yangu kuwa Dira hii ya Taifa itasimamiwa vizuri ili kufanikisha malengo yake yaliyokusudiwa ili kujenga uchumi na maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoolezwa kuwa lengo kubwa la Sera ya Biashara ni kujenga uwezo wa sekta binafsi, asasi na taasisi za umma katika ushindani wa biashara. Kwa kweli ninapongeza lengo hili kubwa la sera ya biashara, lakini naitumia fursa hii kuiomba na kuishauri sana Wizara hii pamoja na Serikali yetu kwa ujumla kuwa wataalam wetu katika masuala ya viwanda na biashara wafanye kazi zao kwa ufanisi kabisa na karibu sana na wahusika au walengwa wa sera hii pamoja na kuwapatia uwezo mkubwa wa kielimu, fedha na vifaa. Wahsika hawa wote ambao wanalengwa kujengewa uwezo kutopteka na sera hii ya biashara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulioanzishwa upya kwa kusainiwa mkataba wa Tume ya Kudumu ya Ushirikiano wa Nchi tatu (*Permanent Tripartite Commission Agreement*) napongeza sana kwa kusainiwa ushirikiano huu wa nchi zetu tatu za Afrika Mashariki na kwa kweli naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwaomba wenzetu hawa tuliuungana katika ushirikiano wetu huu kuwa wa kweli katika suala hili la ushirikiano wetu huu mpya. Ni imani yangu kuwa yale yaliyotokea mwaka 1977 yaliyopelekea kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu ndugu zetu hawa tuliotiliana saini ushirikiano huu mpya ndio waliokuwa na sababu ya kuvunjika kwa Jumuiya ya mwanzo tuliyokuwa nayo, jambo ambalo limeisababishia nchi yetu hadi leo tuna matatizo na waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao wanadai mafao yao ya kufanyakazi katika Jumuiya hiyo iliyovunjika.

Mheshimiwa Spika, naomba ziwekwe sheria, taratibu na Katiba ya Jumuiya yetu hii mpya tulioianzisha upya ili nchi moja itakayosababisha kuvunjika tena Jumuiya hiyo iweze kuwajibishwa Kikatiba katika maeneo yote husika.

Mheshimiwa Spika, suala hili lipewe kipaumbele sana ili kuondoa hofu tuliyonayo baadhi ya Watanzania juu ya kuwepo mafanikio kama yaliyokusudiwa kama yataweza kuafikiwa.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hii tunaelezwa pia juu ya malengo muhimu ya bajeti hii ya mwaka 2005/2006, ambapo inaelezwa kuwa mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2005/2006 utazingatia maeneo yaliyoainishwa katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Mpango huu umegawanywa katika mafungu matatu:-

- (a) Ukuaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato.
- (b) Kuboresha hali ya maisha na afya.
- (c) Utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ninaunga mkono mpango huu na ulivyogawa ni sahihi kabisa na kama utekelezaji wake utapewa kipaumbele, mafanikio yataonekana kama yalivyokusudiwa. Nautakia mafanikio.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wataalam wake.

Mheshimiwa Spika, nianze moja kwa moja kutoa pongezi kwa kazi nzuri inayofanywa na *BRELA*. Kabla ya kuanzishwa kwa *BRELA*, malalamiko na kero zilikua kubwa sana lakini vizuri sana kazi hii nzuri ikaendelezwa zaidi, kwani sasa tupo katika kugeuza dunia kuwa kijiji kimoja.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kutoa ushauri kidogo kuhusu majengo yanayotumika kama ofisi zenu, jengo hili ni la muhimu sana lakini halifai kabisa. Aidha, likarabatiwe au mtafute lingine.

Mheshimiwa Spika, wakala hizi zinafanya kazi zinazofanana hivyo zote ziunganishwe ziwe chini ya *BRELA* yaani *Business Registrations* na *Licensing Agency*, itasaidia katika utendaji kwa uzuri na rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuwaomba pia Wizara hii iangalie uwezekano wa kufungua ofisi za Kanda.

Mheshimiwa Spika, pia nichukue nafasi hii nitoe pongezi kwa *SIDO*, ningeomba kasi waliyonayo waiongeze kidogo, kwani wameweza kuzunguka karibu nchi nzima sasa kufanya maonyesho ya biashara hii kwa kweli inatusaidia sana katika suala zima la kupunguza umaskini na kukuza biashara.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri ili kusaidia zaidi wananchi kwa sehemu ambazo zina *SACCOS* mfano Wilaya ya Kilolo, Iringa tumieni nafasi hii kupidisha mikopo hiyo kwenye *SACCOS* ili iwe rahisi kwenye ukusanyaji wa mikopo na kuwafikia walengwa.

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake yote kwa kuandaa bajeti nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuelezea juu ya shughuli za Wizara kujitangaza duniani. Nilishiriki maonyesho ya Kimataifa huko *AICH* Japan, mwezi Mei, 2005, nilichokiona ni kuwa Tanzania haikuwalishwa vizuri kutokana na ufinyu wa bajeti. Wakati umefika kwa Serikali kutoa fungu kubwa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara ili iweze kushiriki kikamilifu. Nchi haiwezi kuendelea bila kujitangaza duniani.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nasema naunga mkono hoja mia kwa mia asilimia.

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na maafisa wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazozifanya. Kwa kuwa Wizara hii inafanya kazi nyingi za maendeleo hasa wakati wa kusimamia viwanda mama na viwanda vidogo vidogo, ni vizuri Serikali iwaongezee fedha kwa bajeti ijayo ili isimamie vizuri majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu naomba niuelekeze kwenye kiwanda cha kutengenezea zana za kilimo, hivi sasa nchi yetu haina kiwanda cha kutengenezea zana hizo. Hivyo naomba Serikali ilitizame tatizo hili la kuwa na kiwanda hicho

Mheshimiwa Spika, kuhusu viwanda vidogo vidogo, Wizara isimamie viwanda hivyo kwa sababu vipo viwanda vingi vya watu binafsi au vya vikundi vya ushirika, lakini uzalishaji wa viwanda hivyo vidogo havizalishi bidhaa za kutosha kwa sababu wana ushirika au hao watu binafsi hawana utalaam wa kutosha. Hivyo naiomba Wizara iorodheshe viwanda vyote na wajue matatizo ya viwanda hivyo. Vile vile yatolewe mafunzo kwa wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ipeleke watalaam katika maeneo niliyoyataja.

Mheshimiwa Spika, baada ya viwanda hivyo kuzalisha bidhaa Serikali isimamie masoko ya kuuzia bidhaa zao.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kama ifuatavyo:-

(i) Iko haja ya kutoa elimu ya ujasiriamali na huduma za kiufundi hadi katika ngazi ya Wilaya na Miji Midogo. Wananchi wetu wengi wana mitaji midogo midogo na wanaweza kukopa benki ili kuwekeza, lakini tatizo ni kukosa *relevant knowlegde* ya namna gani wafanye na wapitie wapi.

(ii) Pamoja na misamaha ya kodi mbalimbali bado kuna mkanganyiko wa maelezo ya ukusanyaji kodi toka Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Sheria ya Biashara na kutoka Wizara ya Fedha kupitia *TRA*. Wafanyabiashara wadogo wanalipa *Exorbitant Taxes* kwa biashara ambazo ni ndogo mno zisizopagwa kutozwa kodi kabisa hasa Kongwa.

(iii) Nashauri iundwe *Central Corridor Development Commission (CCDC)* ambayo pamoja na mambo mengine itafanyakazi ya kuboresha uwekezaji katika uzalishaji wa divai (*wine*) ili kukuza kilimo cha zabibu katika mikoa ya Dodoma na Singida.

Mheshimiwa Spika, pia kuboresha uwekezaji katika usindikaji wa unga wa mahindi Kibaigwa, ili tuweze kuuza katika nchi za Malawi, Zambia, Kenya na Uganda. *Potential* ni kubwa sana ya kuuza *first class maize flower*.

Mheshimiwa Spika, pia kuwezesha viwanda vidogo vya kusindika mazao ya kilimo kama matunda, karanga, alizeti n a kadhalika. Pia kuwezesha kusindika na *ku-export Kongwa Meat* kutoka ranchi ya Kongwa na pia Ng'ombe wanaofugwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, pia kuboresha huduma za *Dodoma dry port*.
Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Naibu Waziri wake na watendaji wote kazi nzuri wanayofanya katika sekta hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nitauelekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kuhusu Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara, nawapongeza wasimamizi wa maonyesho hayo ya Kimataifa (*BET*) kwa kuboresha mazingira hasa usafiri na barabara ndani ya uwanja wa maonyesho. Mwaka huu wa 2005 Saba Saba ilikuwa tulivu, usafi wa hali ya juu, kelele zimepungua, na biashara ndogo ndogo zimeondolewa barabarani kutoa nafasi nzuri ya wananchi kupita kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, mambo ya kuzingatia sasa ni:-

(a) Kuendelea kuboresha barabara za ndani ya uwanja wa maonyesho ambazo bado ni za vumbi.

(b) Kuanza kujenga eneo la kuegesha magari nje ya uwanja kwa kufikia kiwango cha Kimataifa na lami, uzio na vibanda vya ulinzi kwa usalama wa wananchi wanaofika kwenye maonyesho; na

(c) Ili (a) na (b) yafanikiwe lazima sas a Serikali itenye fungu maalumu la fedha ndani ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ili *BET* ipate uwezo wa kutekeleza hayo.

(ii) Kuhusu utoaji wa leseni za biashara kwa masharti ya kulipa ada/kodi au ushuru mwingine. Bado Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa zinatumia sheria ya leseni za biashara kama kinga yao ya kukusanya ada na ushuru katika maeneo yao. Jambo hili Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kutoa maeleo mazuri ya ufanuzi. Lakini yote yanaishia hapa Bungeni, Halmashauri bado zinaendelea kuitumia vibaya Sheria ya Leseni. Tatizo ni kwamba Wizara haina uwezo wa Kisheria kuingilia mambo ya Halmashauri bila kupitia TAMISEMI. Lakini Sheria ya Leseni ya biashara inayosimamiwa na Wizara au Waziri wa Viwanda na Biashara inapokiukwa bado Waziri wa Viwanda na Biashara anapaswa kuwajibika. Tunapendekeza mwongozo wa uhakika utolewe na uheshimiwe.

(iii) Kuhusu Sheria ya Ushindani, Vyombo vya Usimamizi wa Sheria ya Ushindani viundwe na au kukamilishwa ili haki katika ushindani itendeke. Katika kipindi hiki ambapo bado wananchi wengi na walaji wengi hawajielewa vizuri na kujua haki zao ndani ya Sheria hii wananchi kutoa na kudai haki zao kutokana na kukiukwa kwa Sheria hii kuwepo kwa chama cha walaji ni hatua moja. Lakini chombo hicho hakitoshi chama cha wafanyabiashara kipewe elimu ya juu ya Sheia ya Ushindani na mwenendo wa vyombo vyake ili viweze kuwawasilisha wafanyabiashara.

(iv) Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza uwezo wa *SIDO*, imekuwa inafanya kazi nzuri katika kujenga sekta ya viwanda vidogo vidogo. Kutokana na ukubwa wa nchi *SIDO* inahitaji kuongezewa mambo muhimu yafuatayo:-

(a) Kuongeza vituo vya *SIDO Estates* katika Wilaya ambazo bado hazina maeneo ya mafunzo, ikiwepo Wilaya ya Muheza.

(b) Mheshimiwa Spika, kuongeza uwezo wa *SIDO* katika kugharamia uandikishaji wa michanganuo kwa vikundi mbalimbali vya uzalishaji Wilayani na Vijijini.

(c) Mheshimiwa Spika, pia kuongeza uwezo wa *SIDO* kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali vya uzalishaji na kuvieleza kugeuka kuwa viwanda vidogo vidogo vya kisasa hasa katika sekta za usindikaji wa matunda na maziwa na kadhalika.

(d) Mheshimiwa Spika, kuongeza uwezo wa *SIDO* katika kuwezesha vikundi mbalimbali kuboresha bidhaa zao, kuboresha vifunganishio (*padaging*) na kutafuta masoko kwa bidhaa zinazozalishwa na vikundi au viwanda vidogo.

Mheshimiwa Spika, kuptitia Kamati ya Uwekezaji na Biashara, naunga mkono hoja.

MHE. AISHA P. MAGINA: Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Kwanza nampongeza sana Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na timu yake kwa kazi nzuri wanazofanya katika wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kuhusu *Export Processing Zone (EPZ)* ya Kibaha utekelezaji wake wa kazi unaanza lini maana tangu kituo hiki kitangazwe hadi leo hatujui kinachoendelea pale ni vizuri mambo yakawa wazi.

Mheshimiwa Spika, maonyesho ya Saba Saba napenda pia kupongeza mabanda ya maonyesho mwaka huu yiliboresha sana kuliko miaka iliyopita hasa mabanda ya akinamama wameboresha sana maonyesho yao, nawapongeza sana. Lakini kuwa tatizo nililiona la ajira mbaya ya watoto ambapo kuna watoto wadogo wamewekwa kama masanamu au vikatuni wamevalishwa kama vikatuni kuanzia juu hadi chini wamefunikwa hadi macho na midomo. Sijui wanapumua vipi na mbaya zaidi wanashinda juani kuanzia asubuhi hadi jioni jua lote linaishia kwenye miili yao. Usipoangalia vizuri unaweza kufikiri siyo binadamu kwa jinsi walivyovalishwa, sasa, je, hawa watoto wanaajiriwa na nani na wanalipwa kiasi gani kulingana na kazi ngumu wanayofanya ya kusimama juani toka asubuhi hadi jioni.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye usafanuzi wa kina kuhusu Wizara yako. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, je, Serikali ina sababu gani za msingi kuhamisha Kiwanda cha Magodoro Dodoma na kusababisha wananchi kukosa ajira? Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua kiwanda hapa Dodoma (*DOWICO*)?

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya kutekeleza agizo linalotaka kila Wizara itoe taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2000. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, yako mengi yanayotusibu wakazi wa Mikoa ya watu wakulima Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

(i) Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya. Nini hatma yake? Je, ni kweli mwekezaji hapatikani wa kukiendesha? Je, mpango wa Zimbabwe kutaka kushirikiana na ZZK ulioishia wapi? Umuhimu wa zana za kilimo zenyenye ubora na wa viwango bora ni budi upewe kipaumbele ili tusiletewe majembe na zana nyingine hafifu na kusababisha wizi wa *culverts* za mabati magumu nchini kwa ajili ya kutengeneza majembe ambayo yanaonekana imara na ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, vituo vya urafiki kwa ajili ya zana za kilimo, kama *CARMATEC, TEMDO* na kadhalika havijapewa msukumo wa kutosha na vingine vimeanza kufa. Nini hatma ya vituo kama hivi ambavyo ndivyo baadaye vingesaidia kujenga mazingira ya kujitegemea kiuchumi?

Je, Wizara inatambua kuwa Rukwa imezungukwa na nchi ambazo kupitia Ziwa Tanganyika ingeweza soko kubwa sana la bidhaa iwapo tu Serikali itaimarisha miundombinu ya Mkoa na kuhamasisha wawekezaji wengi. Nchi kama *DRC, Zambia, Burundi, Rwanda* zote zinahitaji biashara mbalimbali na sisi. Hivyo kati ya maeneo ya kufikiriwa kuwa na *EPZ* ni pamoja na Rukwa.

Mheshimiwa Spika, naomba niishukuru *SIDO* kwa kuandaa maonyesho ya zana, bidhaa mbalimbali mkoani Rukwa kwa mwaka huu wa 2005. Hii ni heshima kubwa kwetu. Tunaomba Wizara isaidiane na *SIDO* katika kuratibu maonyesho haya ili matatizo yaliyojitokeza kwenye maonyesho yaliyotangulia huko nyuma. Pia suala la ubora wa vifaa vinavyopelekwa uangaliwe.

Nashauri wafanyabiashara wakubwa toka Dar es Salaam na sehemu nyingine wawe wanakaribishwa ili waweze kuhakkishia wazalishaji wadogo masoko ya mazao yao na labda kupendekeza njia nzuri za kuandaa mazao yao. Si vizuri washiriki wa maonyesho hayo, wakaja na bidhaa nyingi lakini wakarudi nazo.

Mheshimiwa Spika, biashara ya vyuma chakavu vina madhara mengi nchini. Mojawapo ni wizi wa vyuma umeongezeka hata baadhi ya *covers* za mifereji. Lakini pia inasadikiwa kuwa nondo zinazotokana na vyuma chakavu hazina ubora unaotakiwa. Je Wizara inalifahamu hilo na inalishughulikiae tatizo hilo?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa waliojiandikisha kusema kwa mdomo wote wamepata nafasi, sasa tunasitisha shughuli za Bunge ili tutakaporudi mchana watoa hoja waweze kuhitimisha hoja yao.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 06.25 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)

Hapa Naibu Spika (Mheshimiwa Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti

NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla sijajibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, napenda kuungana na wenzangu kutoa rambirambi kwa familia za Wabunge wenzetu waliotutoka kwa kipindi chote cha miaka mitano, Mungu azilaze roho za marehemu mahala pema peponi, *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ningependa kumshukuru sana Waziri wangu Mheshimiwa Dr. Juma Ngasongwa na wafanyakazi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa msaada mkubwa walionipa kuniwezesha kufanya kazi yangu kwa ufanisi mkubwa kwa kipindi chote nilichokuwa hapa Bungeni.

Sasa napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kawe kwa ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi chote cha Ubunge na nawaahidi kama watanichagua kuendelea kushirikiana nao zaidi nitakaporudi Bungeni na sasa nina uzoefu mkubwa na nimekomaa sana (*Makofi*)

Mwisho lakini sio kwa umuhimu, ningependa kuishukuru familia yangu, mume wangu mpendwa Theophil Mlaki na watoto wangu Nambua, Mcharo na Lawrence kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa walionipa kwa kipindi chote cha Ubunge wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napenda kujibu hoja za Wabunge kama ifuatavyo nikianza na hoja ya Msemaji Mkuu wa Upinzani, nitajibu kwa ufupi na Mheshimiwa Waziri atamalizia hoja kuhusu *AGOA*. Nashukuru kuwa ametambua kwamba mpango huu ulianzishwa ili kusaidia kuongeza ajira nchini na uchumi kwa ujumla, lakini kwa masikitiko wawekezaji walisitishwa kutokana na kuwepo kwa migogoro ya mara kwa mara baina ya wafanyakazi na waajiri kwa sababu ya maslahi yao na vile vile mazingira ambayo wao wamesema hayakuridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na migogoro kadhaa mpaka kiwanda kikafungwa na kusimamisha uzalishaji. Labda naomba nitoe masikitiko yangu kwa hali hiyo kwa sababu Serikali tulikuwa tunania nzuri kabisa kuwasaidia wawekezaji waweze kuanzisha viwanda hivi ili kuweza kuongeza ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikiongeza ufanuzi ni kwamba wale wafanyakazi walipata mafunzo ya bure kwa miezi mitatu hadi sita na hii ni gharama kubwa sana kwa mwekezaji. Baada ya mafunzo hayo uzalishaji ulipoanza tu wakaanza na kima cha chini ambacho ni shilingi 45,000 lakini pia kulikuwepo na *over time* ambazo walikuwa wanalipwa kwa kipindi walichokuwa wanafanya kazi za ziada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kiwanda kinachoanza sio rahisi kuanza kulipa fedha nyingi papo hapo kabla hata hawajaanza kupeleka bidhaa nje. Tuliomba wafanyakazi wawe na subira na baadaye walishindwa kusubiri wakaanza migomo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusema kwamba mazingira hayakuwa mazuri, hiyo sio kweli kwa sababu katika soko la *AGOA* wanunuzi wanakagua kwanza mazingira kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinazingatiwa, vyakula vinakuwa ni vizuri, vyoo, hali ya hewa katika majengo yao iwe ya kuridhisha, kwa hiyo, kwa kusema hivyo hapa kuwa na matatizo, matatizo waliyolalamikia ilikuwa zaidi maslahi yao ambayo ilikuwa mshahara wa kima cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile walilalamika kwamba kusiwepo na *NSSF* au *PPF*, lakini wafanyakazi wenyewe pale waliulizwa na walipoona marupurupu yanayotolewa na mashirika haya mawili ni mazuri, walitamani na wao kuingizwa ili pia mwajiri wao aweze kuwaongeza pesa katika michango yao na sasa *incentives* za *NSSF* na *PPF* tunasikia zinazidi kutangazwa na kuwa nzuri hata kutolewa tiba ambayo wafanyakazi wengi wangependa kuijunga wakijua mwisho watafaidika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nijibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, ambaye ameeleza vizuri kabisa kwamba angetamani *EPZ* iendelezwe mpaka Mwanza. Ni kweli nilienda Mwanza kutizama uwezekano wa kuanzasha *EPZ* pale na hasa kutizama maeneo yaliyokuwa yameachwa ya *Nyanza Sheet Glass* na tuliporudi tulishirikiana na *PSRC* kuhakikisha kwamba maeneo hayo tunayachukua na kuyahamishia *NDC* ambayo ndiyo wakala wa *EPZ* na sasa tunatafuta wawekezaji ili waendeleze eneo hilo.

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba Mheshimiwa Stephen Kazi, tunamshukuru kwa jinsi anavyotetea Jimbo lake la Mwanza Mjini na hakika uwezekano utakapopatikana tutahakikisha wameweza kupata wawekezaji kama maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningepenada kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mcemba, ambalo ameeleza kwa kirefu kabisa kuhusu elimu ya biashara itolewe sambamba na ubora wa bidhaa unaozingatia viwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya aina mbalimbali yanatolewa ili kuwapa ufahamu wajasiriamali na kuwaongeza uwezo. Kwa mwaka 2004/2005 jumla ya wajasiriamali 1,126 walipewa mafunzo ya ujasiriamali hasa elimu ya biashara kuititia mafunzo maalum ya usindikaji wa vyakula yalitolewa kwa wajasiriamali 2,600 na wengi wao walikuwa wanawake. Ili kuhakikisha bidhaa inayozalishwa inatengenezwa kwa ubora unaokidhi viwango, utaratibu umeandaliwa ambapo mashirika ya *SIDO* na *TBS* yatashirikiana kuhamasisha na kuwaelimisha wazalishaji kukidhi viwango. Aidha, *SIDO* inashirikiana na Taasisi ya Jumuiya ya Madola kuboresha ufungashaji wa bidhaa 30 za viwanda vidogo kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mwanne Mcemba pia alitaka kujua vijana wabunifu wanasaidiwaje kuendeleza ubunifu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kumjibu Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Tabora, kuwa wabunifu hawa watasaidiwa

kuendeleza ubunifu wao kwa kuingizwa kwenye utaratibu wa kitamizi (*incubator*) ili kuwapatia huduma za misingi za kuwawezesha kuzalisha bidhaa zao na kuziboresha zile ambazo wamezibuni. Chini ya utaratibu huo, wabunifu watapewa huduma za kiufundi, masoko, kifedha na ushauri wa karibu ili kuhakikisha bidhaa hizi zinatengenezwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia chini ya utaratibu huu, watapewa fursa ya kutafuta taarifa na uzoefu kwa wazalishaji wengine kupata uzoefu kupitia kwenye mtandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kuongeza kujibu swal la Mheshimiwa Mwanne Mchomba, ambalo alisema kwamba, kwa nini miradi ya *SIDO* inakuwa maeneo ya Mijini tu na sio maeneo ya vijijini? Ni kweli kutokana na utaratibu ambao tumetoa katika kijitabu chetu cha *SIDO* inaonyesha kwamba asilimia 86 ya mikopo imepelekwa mijini na asilimia 13 tu imekwenda vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda tukiri kwamba hii ilikuwa kutokana na uwezo wa Serikali na *SIDO* kwa wakati huo kuweza kuwafikia wananchi wa vijijini. Lakini sasa ningependa kweli kutamka kabisa kwamba uwezo tumeupata, tumeshakuwa na magari ya kufika mpaka vijijini na tumeongea mara nyingi hapa Bungeni kuelezea kabisa jinsi ambavyo tutakwenda katika vijiji na kila Mkoa unao Afisa ambaye anashughulikia masuala hayo. Kama Mkoa wako hauna gari tungeomba utuambie kabla hatujamaliza muda wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningenda nijibu sasa swala la Mheshimiwa Fatma Said Ali, ambalo ameelleza kuhusu kuongeza mikopo kwa akinamama. Utoaji wa mikopo unazingatia maombi yaliyopelekwa kutoka kwa jinsia zote mbili. Aidha, kupitia mfuko wa *NEDF* katika kipindi cha mwaka 1994 mpaka 2005, jumla ya mikopo 20,521 ya thamani ya shilingi bilioni 7.1 litolewa kwa waombaji kama ifuatavyo:-

Wanawake 10,800, wanaume 9,300. Labda hata nisipoendelea hapo inaonyesha kabisa kwamba wanawake wana asilimia kubwa kuliko wanaume kwa kuchukua mikopo hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa vile vile niendelee kujibu swal la Mheshimiwa Fatma Said Ali, ambaye ameuliza kuhusu kuanzisha shughuli za *SIDO* Zanzibar. Hili suala limekuja sio tu kwa Fatma limekuja kwa Wabunge wengi wanaotoka Zanzibar na wengependa kweli mafanikio ambayo yanapatikana huku bara pia yaweze kupatikana kule Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya kuanzisha *SIDO* Na. 28 ya mwaka 1973, ilielekeza huduma za shirika zitolewe Tanzania Bara, hivyo kufuatana na Sheria tunashindwa kutoa huduma hasa za mikopo huko Zanzibar. Hata hivyo tunatoa huduma za mafunzo na menejimenti mara kwa mara tunapohitajika. Hivi karibuni ilifanyika kozi ya usindikaji huko Pemba na warsha ya menejimenti na masoko Unguja. Pamoja na hayo pia tulimshauri Waziri mwenzetu wa Zanzibar wa Biashara kuhusu kuanzisha mpango kama huu wa *SIDO* katika Tanzania Visiwani, kwa sababu ukisema ule ukweli imesaidia sana watu wengi na wengi na wafanyabiashara nchi nzima ni wa biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Fatma Said Ali, pia aliuliza ushirikiano wa Wizara na wadau kwamba Wizara ifanye warsha kubwa na wadau kufahamu matatizo yao na kuwawezesha kuingia katika soko la nje. Hii ni kweli tunashukuru sana na Wizara imeandaa na inaendelea kuandaa warsha mbalimbali zinazoelezea masuala ya masoko ya nje kama sehemu ya majadiliano na utekelezaji wa mikataba ya biashara ya kimataifa nay a kikanda ndani ya *East African Community, SADC* na *WTO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Fatma Said Ali, aliendelea kueleza kuhusu tatizo la *packaging* na akaomba lipatiwe ufumbuzi. Ningependa kumweleza kwamba utekelezaji wa hatua ya kupata ufumbuzi wa kudumu kwa suala la packaging inachukua sura ya kujenga kituo kipyta, *Tanzania Packaging Technology Centre* ambayo itajengwa pale *TBS* kama mhimili wa kuendeleza sekta hii. Mwaka huu Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 150, kwa ajili ya kukamilisha majengo, yapo mawasiliano ya karibu ya kupata msaada wa wafadhili kwa ajili ya vifaa vyta mafunzo ya wataalam. Serikali ya Denmark, Switzerland na Benki ya Dunia wameonyesha nia ya kusaidia katika suala hili. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swal la Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mbunge wa Muheza, ambalo ameomba kuongezwa kwa vituo vya *SIDO* huko Muheza. Jumla ya maeneo mapya 92 yameainishwa kwa ajili ya matumizi ya wajasiliamali wadogo katika nchi nzima. Kati ya maeneo hayo tayari ujenzi umekamilika katika soko la Songea Mjini, Mchikichini, Ilala, Rangi Tatu, Temeke na Kawe, Kinondoni. Kituo cha Muheza kitajengwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini, MKUKUTA ambao tumeongezewa kama alivyoongea Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake ya bajeti. Kwa hiyo, zikipatikana usiwe na wasiwasi tutajitahidi kuja kutizama huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujibu swal la Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, ambaye anasema anapenda kuelezwu jinsi ya kusaidia vijana vijijini ili waweze kuzalisha mali. Ni kweli ili kuwapa uwezo wa kujiajiri hasa huko vijijini mipango ifuatayo imetekelzwa na *SIDO*. Kwanza kutoa mafunzo katika usindikaji, kutengeneza chaki, kubangua korosho, useremala, ukamuaji mafuta, usokotaji, utengenezaji sabuni na bidhaa za mianzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tumetoa mafunzo ya ujasiriamali, mafunzo haya yamelenga kutoa ufahamu wa mazingira, uzalishaji ama biashara. Jumla ya kozi 863 zilishirikisha wajasiriamali 17, 084 na wengi wa washiriki hawa ni vijana. Serikali kwa kupitia Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa imetenga maeneo 92 kwa ajili ya kuanzisha uzalishaji wa biashara huko Wilayani. Pia kuna mfuko wa vijana ambao unatoa mikopo kwa wajasiriamali wakiwemo vijana ambao nimetaja mzunguko wake sasa hivi unafika bilioni 7. Mikakati hii inalenga kusaidia vijana kuanzisha miradi midogo midogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sasa nijibu swala la Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru sana kwa wazo lake la kusema tuwe na *database* ambayo anamaanisha kwamba tuwe tuna *information* itakayowawezesha wafanyabiashara kuanza biashara kwa urahisi na ikiwezekana basi mtu atengenezewe mpaka mchanganuo na aonyeshwe maeneo na apatiwe fedha. Mimi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge hii ndiyo njia pekee ambayo itasaidia nchi yetu kuweza kuendelea. Kwa sababu niseme labda ile hali tuliyokuwa nayo tangu zamani ya kutokufanya biashara, ili kumwezesha mtu kufanya biashara inabidi twende kwa urefu au kwa mapana namna hiyo. Tumeliona hili na tumeshaanza kulifanyia kazi kama Serikali. Tafiti mbalimbali zimefanyika na mashirika kama *ESRF* na mashirika ya Umoja wa Mataifa kama *UNIDO* yamefadhilli stadi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano umefanyika utafiti jinsi ya kuweza kupata mafuta ya kupika, *palm oil* au mafuta ya mawese ambayo michikichi ndiyo inatoa mawese, zinaota sana maeneo ya Kigoma, *UNIDO* wameshafanya utafiti na tayari tunao utafiti mzima. Bidhaa kama korosho, chai na ngozi vyote hivyo vimefanyiwa utafiti. Sasa tuko tayari kuweza kuunganisha juhudini zetu na kuwapatia wawekezaji mbalimbali.

Kuhusu *godown* ambazo ziko Moshi, namshukuru sana Mheshimiwa Philemon Ndesamburo ambaye ameona uchungu katika maeneo hayo kusema kwamba kuna ma-*godown* mengi yamekaa tupu kule Moshi. Mimi niliyaona hayo na nilitembelea Mkoa wa Kilimanjaro, kwanza tunashukuru sana tuna Mkuu wa Mkoa pale Mama Hilda Ngoye ambaye anatizama na kuhakikisha kwamba biashara, viwanda vinaanzishwa pale Moshi. Tumeshakwishafanya *investment forum* na tumealika wengi pamoja na watu kutoka nje ili kuhakikisha kwamba tunawavutia wawekezaji kuweza kurudi katika Mkoa wa Kilimanjaro. Nilikwenda pale na nikatembela yale ma-*godown*.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyaona hayo ma-*godown* nilirudi Serikalini kwa wenzangu na kuyaomba, yako makubwa sana kwa mfano kuna ma-*godown* ya *National Milling* ambayo yalikuwa yanatumika kama *strategic grain reserve* ya nchi. Lakini sasa hivi yamehamia zaidi Arusha, kwa hiyo, tukatizama pale tukakubaliana Kiserikali kwamba kama anapatikana mwekezaji ambaye anahitaji kuanza kufanya kazi mara moja kwenye yale ma-*godown*, Serikali tungekuwa tayari kumpa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini naomba kumwambia Mheshimiwa Philemon Ndesamburo kwamba ziara yangu haikuzaa matunda, kwa sababu wazee walioniita pale Moshi wengi wazee wangu walikuwa na matarajio makubwa sana na Serikali na kusema kwanza tumempata kijana wetu na yuko katika Wizara hiyo. Lakini nasikitika kusema kwamba wengi nilivyowapa changamoto walinionyesha kwamba hawako tayari kuanza hivyo viwanda. Wengi ambaao nisingependa kuwataja hapa walinionyesha kwamba wamekwisha wekeza katika mahoteli na niliwaonyesha kwamba sio kwamba tutawapa *godown*, tuwape na pesa tuwape na mradi bila wao wenyewe kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kama tunakupa bilioni moja, kwa Mfuko wa Dhamana tunataka na wewe angalau utoe shilingi milioni 300. Kwa hiyo, nilichofanya cha kwanza niliwaita matajiri wa pale Moshi, labda Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, hakuwepo siku hiyo na nikawaeleza kwamba ma-*godown* yapo, pesa Benki

Kuu tutadhamini hiyo mikopo na biashara ambayo sasa hivi inachanganya ambayo ipo ni biashara kadhaa. Wote niliowaona walinionyesha kwamba hawako tayari kufanya miradi au wamekwisha wekeza katika miradi mingine. Lakini sijakata tamaa nawasiliana na Mkuu wa Mkoa, bado tuko tayari, tumeainisha maeneo kadhaa na tunawaomba wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wawasiliane na sisi kuhakikisha kwamba tunaweza kutumia majengo haya na kuanza biashara kama walivyotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono hoja asilimia mia. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha leo asubuhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa Bungeni kwa kauli na kwa maandishi, lakini vile vile napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa William Shellukindo, kwa maelezo yake mazuri ambayo yalitolewa na Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, ambaye ni kaka yangu wa siku nyingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru sana, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, ambaye aliwasilisha maoni ya Upinzani hapa Bungeni kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Freeman Mbewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii walikuwa 19 pamoja na Naibu Waziri, Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kauli walikuwa sita pamoja na Naibu Waziri wanakuwa saba na Waheshimiwa walichangia kwa maandishi ni 12 akiwemo wa mwisho kabisa Mheshimiwa Raphael Mlolwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niwataje kwa majina, kwanza ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro ambaye alitoa maoni kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Mheshimiwa Adelastela Mkilindi, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Semindu Pawa na Mheshimiwa Rita Mlaki, Naibu Waziri.

Waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao, Mhehimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud na Mheshimiwa Job Ndugai, Mbunge wa Kongwa.

Wengine ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Raphael Mlolwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nипитie hoja za Waheshimiwa Wabunge, kwanza ya Kamati. Kamati nawashukuru sana kwa kusema hapa mbele ya Bunge kwamba Ofisi yetu kwa kweli hairidhishi na mimi nakubali hairidhishi na waliochangia maelezo haya sio Kamati tu, hata Mheshimiwa Venance Mwamoto, tumekubali kwamba hairidhishi. Tumefanya juhudhi nyingi kwa kweli za kutaka kuhama pale, mojawapo tulitaka kuchukue jengo la *NASACO* lakini *NSSF* wakatuwahi, tukataka tupewe kiwanja ili tujenge, nalo hilo limekuwa gumu, ingawa labda wenzetu wa *BRELA* watakajapojenga, tutapata nafasi humo.

Lakini vile vile tumefanya juhudhi zingine za kutafuta majengo Dar es Salaam ambayo yako wazi na tukifanikiwa basi tutahamia. Kwa kweli mahala pale tulipo kwa hadhi ya Wizara ya Viwanda na Biashara hapafai na tutaendelea kujitahidi kupata mahali pazuri zaidi, tukihamia Dodoma tutakuja Dodoma hakuna neno, sisi tuko tayari kuja Dodoma hatuna matatizo kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa vile vile na hoja ya kuhusu suala la utekelezaji wa Kanda za Maendeleo hususani Kanda ya Mtwara na Kanda ya Kati yaani *Mtwara Development Corridor* na *Central Development Corridor* ziundiwe *Comission*, hili nalo liliezwa na Kamati lakini vile vile na Mheshimiwa Job Ndugai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kweli imekabidhi jukumu hili kwa *NDC* ambayo kwa kweli hilo ndiyo kazi yake sasa, kazi imechelewa kutokana kwa kweli na sio na *NDC*, kazi imechelewa kwa sababu hatukuwa na makubaliano rasmi. *Mtwara Development Corridor* ni ya nchi nne, ni Tanzania, Malawi, Msumbiji na Zambia, sasa mpaka mwaka jana mwezi Desemba, Wakuu wa Nchi walipotia saini mkataba sasa kazi rasmi imeanza lakina kabla ya hapo ilikuwa ngumu kwa nchi moja kuwekeza fedha nyingi katika jambo ambalo wenzake hawajafanya *commitment*

Kwa hiyo, sasa *commitment* ipo na sisi tutaendelea na kuratibu kama tulivyopewa jukumu hili na nina hakika sasa mambo yatakwenda vizuri zaidi. Kanda ya Kati na yenyelezo sio Tanzania peke yake, inahusisha nchi za Rwanda na Burundi lakini vile vile *Democratic Republic of Congo*, kwa hiyo, nchi nazo hapa zitakuwa nne.

Kwa hiyo, na lenyewe lazima lifanye vizuri kwa lengo la kuhakikisha kwamba nchi zote hizi kwanza wanakuwa na mkataba na Tanzania kuhusu jambo hili na wote wanachangia katika kuendeleza kanda hii ya Kati, kwa maana ya kwamba kuna miradi pale mikubwa ya usafiri wa reli, mawasiliano, barabara na yote hayo lazima yazingatiwe kwa madhumuni ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Kanda ya Kati katika nchi zote nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati pia ilizungumzia suala la kutangaza bidhaa za Tanzania, hili tunalifanya kupitia *BET*, kama mnavyoona kupitia Maonyesho ya Kimatafia ya Dar es Salaam. Lakini vile vile *BET* inakwenda hata nchi nyingine kushiriki. Hiyo ndiyo sehemu ya kutangaza, lakini lazima tukubali vile vile kwamba ufinyi wa bajeti ndiyo unakuwa kikwazo, lakini nia ipo.

Kambi ya Upinzani walileta hoja ya kuhusu suala la anuani za kudumu za makampuni, hili lipo, lipo katika Taasisi yetu ya *BRELA* na vile vile katika Ofisi ya Ukurugenzi wa Biashara, hawa wanajulikana kama kuna mtu anahitaji takwimu hizi zinapatikana. Kwanza ni sehemu ya Kisheria, kwa mujibu wa Sheria ya Leseni ya Biashara ya mwaka 1972 ambayo inataka watu hawa watambuliwe na anuani zao kamili ziko na kwa maani hiyo hizo zipo kama mtu anahitaji zinawezakupatikana.

Sheria *of course* inafanyiwa marekebisho kama nilivyosema hapa leo Bungeni na kufanyiwa marekebisho huku kutaongeza wafanyabiasha wengi zaidi na hawa wote pia tutawarekodi ili wajulikane walipo.

Kulikuwa na suala la *Chief Executive Officers Scholarship Fund*, wachangiaji ni nani na watumishi wangapi wamekwenda? Mpango huu ni changamoto ulioanzishwa na Wakuu wa Mashirika ya Kimataifa yalipo Tanzania ili kukidhi haja ya kupata wataalam wa Kitanzania walisomea katika vyuo hapa nchini na kupata sifa ambazo wanaweza kumudu majukumu yao kikamilifu. Kwa hiyo, hawa ndiyo waliochangia na hili jambo linatokana na vikao vya *Tanzania National Business Council* ambalo Mwenyekiti wake ni Rais wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mfuko huu unasimamiwa na Wizara ya Sayansi na Teknolojia na Elimu ya Juu, nimewasiliana nao hivi leo baada ya hoja hizi kwa lengo ya kupata maelezo ya kujibu swali la Mheshimiwa Freeman Mbewe, Msemaji wa Upinzani. Kimsingi maandalizi ya mfuko yapo katika hatua za mwisho ikiwa ni pamoja na kupata asasi itakayosimamia utekelezaji wake. Wachangiaji ni Serikali ambayo imeahidi kutoa kiasi cha dola za kimarekani milioni 2 ambayo ni sawa sawa na shilingi bilioni mbili. *Chief Executive Officers* wa sekta binafsi nao wameahidi kuchangia shilingi bilioni mbili, utekelezaji utaanza katika mwaka huu wa fedha wa 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya *Tanzania National Business Council* ni nini? Majukumu yake makubwa ni kwamba kutoa fursa kwa Serikali na sekta binafsi kukaa pamoa na kujadili masuala yanayohusu biashara, jambo hili ni zuri na tumelianza katika miaka hii miwili tunaendelea vizuri, ambako vikao vyake kama nilivyosema mwanzo Mwelyekiti wake ni Rais mwenyewe. Kila baada ya miezi mitatu au minne tunakutana ili kujadili masuala yanayohusu maendeleo ya biashara na uwekezaji ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Fatma Said Ali, alizungumzia suala la ushirikiano wa Wizara na wadau, Wizara ifanye warsha kubwa na wadau kufahamu matatizo yao kuwezesha kuingia masoko ya nje. Jambo hili linafanyika, linafanyika siku zote na tutaendelea kulifanya kwa mfano kuna masuala ya *East African Community* huwa tunakaa nao tunazungumza, masuala ya *SADC* hata masuala ya *WTO* na hata baadhi ya Wabunge hapa wameshiriki katika vikao hivi na tumewahi kwenda nao nje kwa ajili ya kuhuduria mikutano inayohusu Taasisi hizi. Kwa hiyo, wafanyabiashara hawa wakubwa wanashiriki kikamilifu. Napenda pia niseme kwamba uwezo wetu wa bajeti siyo mkubwa lakini tutakapopata fedha zaidi tutashirikisha watu wengi zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko tatizo la *packaging* ambalo lipatiwe ufumbuzi. Napenda kutoa taarifa hapa kwamba Serikali imetoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa *Packaging Technology Centre* ambayo iko chini ya TBS kama mhimili wa kusimamia ubora wa bidhaa ndani ya nchi yetu na fedha zilizotolewa ni shilingi milioni 150. Kwa hiyo, jambo hili linaendelea vizuri na tunaamini kwamba Serikali zingine zitasidia kwa mfano Serikali ya Denmark, ya Uswiss na Benki ya Dunia wameonyesha nia ya kutusaidia katika jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko hoja zilizotolewa na Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mheshimiwa Semindu Pawa. Hizi zote napenda kuzitolea maelezo kama ifuatavyo:-

Kwanza, hakuna mfumo rasmi wa kusimamia biashara baina ya Tanzania na Msumbiji kiasi kwamba biashara iliyopo ni bubu na nadhani hatua ya kujenga daraja lile la Umoja nadhani litaweza kufanya biashara hii iwe rasmi zaidi kuliko ilivyo sasa. Lakini tunaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Msumbiji ili tuweze kukamilisha jambo hili kwa uzuri zaidi.

Kuna utaratibu gani unatumika kuingiza sukari nchini kutoka nchi za jirani hususan sukari kutoka Malawi kwa Wilaya ya Mbinga. Mahitaji ya sukari nchini inasemekana ni tani 340,000. Uzalishaji nchini ni tani 224,000. Mauzo ya nje kwa mwaka 2003/2004 yalikuwa tani 23,000 hivyo kiasi kinachobakia cha tani 201,000 kilitumika katika soko la ndani. Pengo la tani 139,000 linafidiwa kwa kuagiza kutoka nje.

Katika msimu ambao viwanda havizalishi yaani Januari hadi Juni kila mwaka, Serikali hutoa maelekezo kwa wafanyabiashara kuingiza sukari ili kufidia pengo hilo linalojitokeza. Lakini kule mipakani kuna biashara kama nilivyosema ya bubu. Sasa hiyo biashara tunataka tuihalalishe kwa kujenga uhusiano wa kibiashara kati ya nchi yetu na nchi za jirani. Kwa hiyo, hili litasimamiwa vizuri baadaye. Lakini kazi ya kuagiza sukari inafanywa na Shirika la Sukari, ndiyo linalotoa kibali, siyo kuagiza, linatoa kibali ambalo liko chini ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Tanzania imepewa fursa ya kushiriki katika masoko yanayotokana na Sera za *EBA* na *AGOA* lakini matumizi ya fursa hizo ni ya chini mno, ni sababu gani na zipi za msingi zinazochangia hali hii licha ya jitihada zetu za pamoja za kujenga *EPZ*?

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya msingi ni uwezo mdogo wa ushindani katika Sekta binafsi katika masoko ya nje. Hii ndiyo sababu ya msingi. Hatua mbalimbali zimechukuliwa kujenga uwezo wa ushindani ikiwa ni pamoja na marekebisho ya Sera za kiuchumi yaani *Macro-economic Policy Framework* hususan kupunguza mfumuko wa bei, kurekebisha taratibu na sheria za utendaji katika sekta binafsi kama vile sheria za ajira, sheria za ardhi, taratibu za utoaji leseni na kazi hii inaendelea.

Vile vile kupata ufumbuzi wa kudumu wa matatizo ya upatikanaji wa uhakika kwa bei nafuu zaidi kwa umeme. Hili la umeme hili na maji ndiyo linatukwamisha katika

kushindana vizuri katika masoko ya Kimataifa kwa sababu kwa mfano chukua mfano wa *South Africa*, umeme kule *kilowatt* moja ni senti 4 za dola ya Kimarekani wakati kwetu hapa 8 mpaka 9.

Kwa hiyo, hata mkizalisha bidhaa lazima zenu zitakuwa hazishindani vizuri katika soko la namna hiyo. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tunalitilia mkazo na tunaendelea kulisimamia na nimelisema leo asubuhi. Lakini vile vile juhudzi za kuwezesha upatikanaji wa mtaji na taaluma kwa ajili ya sekta binafsi zinaendelea. Hizi ni hatua za upeo wa muda na wakati na mipango vile vile inafanywa kwa ajili ya upeo wa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, anaulizia suala la sera ya viwanda na biashara ndogo, inasema nini na inafanya nini kuhusu biashara ndogo. Ujenzi wa uwezo wa kutekeleza sera ya Taifa ya biashara, masuala mawili. Suala hili linafanyiwa kazi katika programu mbalimbali zinazoteklezwa kwa misaada ya wahisani inayolenga kuendeleza biashara na kutumia fursa za masoko zinazotokana na mfumo wa utandawazi kama vile *JITAP* na *Intergreated Framework*. Pia suala hili limepewa kipaumbele chini ya mpango wa MKUKUTA kwa mwaka huu wa fedha 2005/2006 nalo nimelisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano ndani ya *EAC*. Anatumaini kuwa yaliyotokea mwaka 1977, hayatatokea tena safari hii na mimi nadhani hivyo hivyo na mimi nakubaliana naye kabisa kwamba hili halitatokea tena, kwa nini, kwa sababu tumefanya maandalizi mazuri zaidi kuliko huko nyuma na ule mkataba ndiyo maana unakwenda hatua kwa hatua. Hatua ya kwanza ambayo tumeanza mwezi Januari mwaka huu ni ile ya Umoja wa Forodha, hatua ya pili itakuja ya *Common Market*, hatua ya tatu ya *Monetary Union* na hatua ya mwisho ni ya *Federation*, ndiyo maana wale amba wanataka ku-*fast track federation* huwa tunawashangaa kidogo kwa sababu hii hatua ya kwanza, kwanza itekelezwe na itekelezwe vizuri ili tuende hatua hizo zingine mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko pia tatizo lililoulizwa na Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni kuhusu tatizo la kodi kubwa kwa wanaofanya biashara ndogo ndogo na mkanganyiko uliopo katika suala hili baina ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Mamlaka ya Mapato. Kwa kweli hakuna mkanganyiko, sasa hivi hapa kwanza wanaouza biashara ndogo ndogo, leseni zote zimefutwa mpaka shilingi milioni 20. Hutakiwi tena upate tatizo la leseni, kwa hiyo, nadhani hili sasa limekamilika.

Mheshimiwa Aisha Magina, tatizo la ajira ya watoto wadogo katika Maonyesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam, wanavalishwa nguo kama vikatuni mwili mzima na kukaa juani siku nzima hata kushindwa kupumua. Watoto hao walajiriwa na nani na wanalipwa kiasi gani kulingana na ugumu wa kazi hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu ni kwamba, wakati wa Maonyesho wapo wazazi wanaokwenda kwenye Viwanja vya Maonyesho na watoto wao. Aidha, viro vivutio kwa

watoto katika mabanda haya, mojawapo ya vivutio hivyo kwa mwaka huu ilikuwa hivyo vinyago (*musks*) vilivyokuwa vinatolewa na baadhi ya washiriki kwa watoto hao.

Hata hivyo Wizara haikubaliani na utaratibu huo wa kuwaajiri watoto wadogo kwa ajili ya kufanya promotions za bidhaa. Wizara haikubaliani na hili. Wizara itachunguza na ikibaini kuwa kuna mshiriki aliyetumia watoto kwa njia hii, basi hatua zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kuwapa washiriki wote masharti ya kutowaajiri watoto katika Maonyesho yajayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Herbert Mntangi, wanazungumzia kuhusu kuboresha barabara za ndani ya Uwanja pamoja na *car park*, Wizara itenye fungu maalum. Hatua za kuongeza maeneo kwa ajili ya kupanua maegesho ya magari kwenye Viwanja vya Maonyesho, zimeanza kuchukuliwa, kama safari hii umekwenda pale ni tofauti kama ulikwenda mwaka jana. Tumeongeza maeneo ya kuegesha magari hata pia tueongeza milango, ule msukumano na msongamano uliotokea mwaka jana, mwaka huu tena haukutokea.

Mwaka huu mambo yalikuwa murua kabisa, lakini tutaendelea kuboresha miundombinu ile, maana sijui kama Waheshimiwa Wabunge mnafahamu kwamba katika Viwanja hivi vya Maonyesho, Kiwanja chetu kile cha Mwalimu Nyerere cha Dar es Salaam, kinapitwa tu na kiwanja cha namna ile cha Cairo na vile vya Afrika Kusini. Kwa hiyo, tumepiga hatua nzuri kuweka Kiwanja chetu katika hali nzuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja ya Kambi ya Upinzani kuhusu viwanda vilivyobinafsishwa vinafanya shughuli tofauti na zile za viwanda hivyo kabla ya kufanya hivyo. Hoja hii naikubali isipokuwa tu mfanyabiashara binafsi anazingatia faida. Pale anapoona mchepuo ule au line ile ya *production* haiwezi kumletea faida, lazima atabadilisha. Msingi kwa sisi kama Serikali ni kwamba kile kiwanda kinazalisha. Hilo la kwanza. Lakini la pili, kinaajiri watu na tatu kinalipa kodi. Msingi huo ndiyo muhimu zadi kuliko line ya *production*.

Je, ni viwanda vingapi vimechukuliwa na Wizara kutopteka na kubadilisha shughuli. Kwa kweli hili sisi hatuoni tatizo kwa hiyo, hatujachukua kiwanda kwa sababu hii. Sababu tunaweza kuchukua ni ya kwamba kama yule mtu kanunua kile kiwanda lakini hazalishi na kiwanda kile ni cha Serikali, yule ndiyo tunamnyang'anya. Tunamnyang'anya kwa lengo la kukitangaza upya ili apatikane mwekezaji mwenye uwezo. Hicho ndiyo tunafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini katika viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa ajili ya fursa ya *AGOA*, wafanyakazi wana migogoro kutopteka na maslahi na wanalipwa mishahara ya shilingi 45,000. Hili jibu lake ni kwamba, matatizo katika viwanda hivi yanatokana na madai ya wafanyakazi kutaka ongezeko la mishahara wakati hali hairuhusu. Hili ni kweli kwa sababu gani, kiwanda kimeanza mwaka jana, leo unataka mshahara uongezeko, umezalisha lini mpaka uweze kulipwa mshahara huo unaotaka uongezeko?

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane hili. Kama tusipofanya vizuri hili, tutakimbiza wawekezaji kwa sababu mwekezaji yeyote anayeku ndani ya nchi hapa anataka kupata faida na faida yake inatokana na uzalishaji bora. Sasa kuna matatizo, sasa matatizo haya lazima tuyazingatie kwa lengo la kufanya ajira ipatikane lakini hapo hapo mwenye kiwanda pia aweze kunufaika. Kwa mfano kiwanda hiki cha *Star*, nitoe mfano, kiwanda hiki kilitumia gharama kubwa kwa ajili ya mafunzo ya wafanyakazi pamoja na kutekeleza masharti ya wanununzi. Kwa sababu kiwanda kile ni cha *AGOA* kina masharti ya kutekeleza kule Marekani, lakini kabla ya kuanza kilifundisha wafanyakazi kwa miezi mitatu kwa gharama yake, ndiyo maana tumemwomba hapa Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo kwamba atenge Chuo kimoja cha *VETA* kwa ajili ya kufundisha wataalam wa sekta ya nguo hasa *garments*, vinginevyo itakuwa gharama sana na itakuwa siyo kivutio kwa nchi yetu watu kuja kuwekeza ndani ya nchi. Kwa hiyo, ina pande mbili suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *MWATEX*, Mheshimiwa Spstephen Kazi. *MWATEX* ni kiwanda ambacho kilichukuliwa na *LAURJ*. Kwa mujibu wa sheria ya ufilisi, kampuni yoyote ikiuzwa kwa utaratibu wa ufilisi, wadai hutangaziwa ili wapeleke madai yao na malipo yao hutokana na fedha zinazopatikana kutokana na mauzo ya mali husika na wafanyakazi huwa wa mwisho kulipwa. Hii ndiyo sheria yenye inavyosema. Sasa kazi hii ambayo inafanywa na *LAURJ* ambayo ni ya Waziri wa Fedha, inaendelea haijakamilika. Kwa hiyo, hawawezi kulipwa sasa, watalipwa pale itakapokamilika na wao watalipwa mwisho. Lakini sisi tutaendelea kupiga debe ili na wao katika kulipwa humo walipwe, wasikose kabisa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Richard Ndasa, ameleta maswali makubwa hapa. Kwanza suala la bei ya vitu vyaa bidhaa, halafu majembe, mabati, saruji, sukari, viwango vyaa ubora wa majembe, uwepo wa kuwa na utaratibu wa kuwa na *feasibility study* na *Debtor Bank* ya miradi, hili lililetwa na Mheshimiwa Philemon Ndesamburo.

Sasa majibu ni ya kwamba suala la bei kwa sasa hivi, Serikali haiwezi kuliingilia, si tumekubaliana hapa kwamba sasa ni uchumi wa soko, nisiseme soko huria ama uchumi huria siyo sahihi. Sahihi ni kwamba tuna uchumi wa soko ambao bei inazingatia nguvu za soko. Kwa hiyo, sisi kama Serikali hii kazi tuliisha iacha, na hii ndiyo sera ya Chama chetu cha Mapinduzi kwamba mambo haya tusiyaingilie sisi.

Lakini ubora wa majembe, kwa kweli sisi kama Serikali kwa kupitia *TBS*, tumesimamia barabara, tatizo kuna baadhi ya watu wanaingiza majembe ambayo hayana ubora unaotakiwa. Sasa ni jambo la viongozi wote na wananchi na Askari Polisi watuarifu ili hatua zichukuliwe kwa watu hao wanaoingiza majembe siyo halali. Sisi suala la ubora tunasimamia na mfano mzuri wa *condom* kama mnakumbuka mwaka juzi nadhani. *Condom* zilikuja mbovu, tukazikataa na kweli zikarudishwa. Tunataka *condom* imara na majembe yawe imara. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kubadilisha kiwanda cha *UFI*, kitengeneze mabomba, kwanza mabomba yale ni maalum kwa ajili ya mradi ule, tungeagiza nje,

tungetumia fedha nyingi zaidi. Sasa kupata hapa ndani ya nchi ni nzuri, hiyo ya kwanza na ukiwa na kiwanda ndani ya nchi yako ni jambo jema, si ndiyo maana yake ya *Industrialization process*. Kwa hiyo, kuwa na kiwanda ndani ya nchi ni vizuri lakini hoja ya kwamba kiwanda kile kimebadilisha kutoka majembe kwenda kwenye mabomba, hili suala lenyewe kwanza hatukumpata mwekezaji aliyetaka kuwekeza katika majembe, sasa mnafanyaje!

Hapa kuna mtu anasema mimi natengeneza mabomba, baadaye huyu Bwana atatengeneza majembe ya trekta yale *ma-plough*, ndiko anako kwenda na kiwanda kile kama umetembelea sasa ni kizuri kuliko kilivyokuwa nyuma na kimeajiri watu wengi zaidi. Sasa sisi Serikali tumefurahi, kwanza, tumepeata mabomba na baadaye tutapata *ma-plough* ya matrekta, lakini pili tumepeata ajira, kubwa zaidi, lakini tatu, *infrastructure* ile, miundombinu ile ni mizuri zaidi kuliko ilivyokuwa wakati wa *UFI*.

Kwa hiyo, katika mambo ya uchumi lazima hapa unakosa hapa unafaidika. Kwa hiyo, msingi hapa ni nini, msingi ni kuendelea kusimamia ubora wa majembe, siyo kung'ang'ania majembe yatengenezwe *UFI*, kwa sababu *UFI* ilishindwa, kiwanda kilifungwa na sisi kama Serikali hatukuweza tena kukiendeleza. Kwa hiyo, hilo jambo ni la muhimu kwa namna hiyo.

Suala la utekelezaji wa *EPZ* Kibaha utaanza lini. Anauliza Mheshimiwa Aisha Magina na Mheshimiwa Semindu Pawa. Pale tutaanza kutekeleza tutakapopata fedha, la kwanza. Lakini pili tutaanza kutekeleza atakapopatikana mwekezaji. Tukipata mwekezaji atakwenda pale. Tulimpata mwekezaji mmoja lakini tukavutana hapo, akahamia Dar es Salaam na hili ndiyo jambo la muhimu hili, mkimpata mwekezaji mchangamkie, mkivutana naye atahama tena heri huyu Bwana anahamia Dar es Salaam, Mbagala. Lakini huyu angweza kuhamia Uganda, angweza kuhamia Kenya.

Kwa hiyo, ni muhimu wakati wote tunapopata wawekezaji hawa tuwachangamkie na ndiyo maana hapa naweza kumshukuru sana Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro kwa juhudhi anazofanya za kuvutia wawekezaji Mkoani mwake. Mimi namunga mkono *a hundred percent* katika jambo hili kwa sababu ndiyo jambo tunatakiwa tufanye sisi viongozi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Herbert Mntangi na Mheshimiwa Fatma Said Ali, wanazungumzia suala la sheria ya ushindani ili iweze kufanya kazi hasa kwa watu wale walaji au watumiaji. Sheria inataka Waziri atue *National Consumer Advocacy Council*. (*Makofit*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili nimelifanya tayari na muda mfupi itatangazwa lakini naendelea vile vile kuunda Tume yenyewe, tunaendelea vizuri na itakapokamilika mtagaziwa ili kwa shabaha ya kwamba katika uchumi wa soko panapokuwa na ushindani wa haki ndipo inakuwa nzuri. Kama hakuna ushindani wa haki inakuwa ni jambo baya kwa wananchi. Kwa hiyo, hili tunalismamia vizuri nami ninahakika litakamilika vizuri hapo tutakapokamilisha mambo ya uundaji wa Tume na

vile vile Baraza sijui la walaji au tuseme la watumiaji, labda Kiswahili kizuri ni watumiaji ili waweze kusimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umenitupa mkono. Naomba nimalizie kama alivyomalizia mwenzangu Naibu Waziri na vile vile tumejifunza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuwapongeza na vile vile kuwashukuru familia zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, familia zetu kwa kweli zina tuvumilia sana hasa watu kama sisi tunaosafiri mara kwa mara, maana hata Bungeni hapa mara nyingine sionekani, lakini natumwa mambo ya *WTO* mambo ya Septemba na kadhalika. Mwezi Septemba kuna mukutano mkubwa wa Wakuu wa Nchi na sisi tulikwenda kuwaandalia kule New York, tumekaa siku nane kule. Sasa unarudi hapa unakuta mama peke yake na watoto na nini, basi inakuwa ni matatizo. Kwa hiyo, tunaomba tuwashukuru sana hawa jamaa na ndugu zetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 - *Administration and General...* 3,793,025,300/=

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo na Bajeti ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu Kamati yangu iliunga mkono isipokuwa kuna mambo kidogo ambayo tu nataka yaweze kuwekwa sawa sawa. Ni hili fungu 44, programU 10, kifungu 1001, kifungu kidogo 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu Mheshimiwa Waziri atusaidie kuweka katika kumbukumbu mambo tuliyozungumza naye kwenye mukutano tuliofanya tarehe 6 kule Dar es Salaam ambayo hakuweza kuingiza kwenye hotuba yake kwa sababu ilikuwa tayari. Pia, Kamati yangu haikuweza kuingiza kwenye taarifa ya Kamati kwa sababu ilishaandaliwa tayari na ni mambo ambayo nadhani kwa wananchi na Taifa kwa jumla ni muhimu. Ni mambo mawili ambayo tunataka tupate maelezo ili Serikali ya Awamu ya Nne kwa kweli iyaendeleze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni kuhusu maonyesho, kuna maombi ya wananchi kwamba muda hautoshi, yalikuwa ni mazuri sana na wangetaka yawe ni wiki mbili. Waziri atuhakikishie kwamba jambo hili litaendelezwa maana hoja za wananchi si za kuacha hivi hivi tu.

Suala la pili ni kuhusu maonyesho haya na sera yetu ya Viwanda Vidogo na vya Kati (*Small and Medium Enterprises*) kwamba zingekuwa na siku maalum ya Maonyesho ya Viwanda Vidogo na vya Kati ya Kitaifa ukiacha ya Kimataifa kwa sababu wakichanganywa na hawa wakubwa wa Kimataifa hawapati nafasi ya kuweza kushughulikiwa kwa undani na matatizo yao kuondolewa. Kwa hiyo, hoja hii si yangu binafsi, ni ya Kamati ndiyo maana sikuweza kuweka katika mchango wangu. Nashukuru sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwa kukumbusha haya mambo mawili na ni kweli wakati tukiyazungumza hayakuwemo katika hotuba zetu, ya kwake na ya kwangu. Lakini nilijibu pale kwamba hili ni suala ambalo ni zuri sana. Suala la kuongeza siku ni zuri na hii siyo mara ya kwanza, hata maonyesho yale ya zamani yalikuwa ni ya siku tano, baadaye yakaenda siku saba, leo tuna siku kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilikuwa nasoma kwenye gazeti nadhani la Mtanzania, mtu mmoja aliandika barua akisema pia maonyesho haya yaongezwe yawe wiki mbili. Sasa siwezi kutamka hapa leo kwamba nitaongeza, hapana. Tutakachofanya ni kwamba ujumbe huu kama nilivyo sema siku ile tutashauriana na wenzetu Wizarani kwa sababu muda wetu sasa ni mfupi, labda wenzetu watakaokuja hao ndiyo itakuwa moja ya mapendekezo yetu kwao ili wafikirie suala hili la kuongeza muda. (*Makofi*)

Kuhusu Maonyesho ya Kitaifa kwa ajili ya viwanda vidogo, hili nalo halina mgogoro kwa sababu hivi sasa tumeanza. Tumeanza kama Mheshimiwa anavyofahamu tuna maonyesho ya Kikanda. Mheshimiwa Mwanne Mcemba, katukumbusha hapa kwamba yalikuwepo Tabora na yalikuwepo mengine Kagera na mengine yalifanyika Kigoma na mengine Tanga, mengine yalifanyika Iringa na mengine Mwanza na mimi siyo mchoyo, huwa naomba Mawaziri wanaohusika katika maeneo hayo ndiyo wayafungue kama moja ya kujenga mshikamano katika jambo hili. Kwa hiyo, hili tutaendelea kulifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hili la siku maalum ya viwanda vidogo na vya kati peke yake, nalo ningependa tulijibu kwamba, tutalizungumza ndani ya Wizara na liwe moja ya mambo ambayo wenzetu watakaokuja walifanyie maamuzi, kwa kweli ni jambo zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa maandishi na nilitaka maelezo tu, sina tatizo na mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Nimeulizia Kiwanda cha Magodoro Dodoma. Hiki kiwanda kilikuwa kinasaidia sana ajira katika Mkoa wa Dodoma, kilihamishiwa Dar es Salaam, lakini hadi leo kwenye *TV* utaona, Magodoro Dodoma. Sasa je, kuna mpango wa kukirudisha Dodoma hicho kiwanda? (*Kicheko*)

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijua kwamba Kiwanda cha Magodoro cha Dodoma kiliungua moto, lakini waliendelea kutangaza magodoro ya Dodoma. Lakini ni muhimu kutofautisha kati ya mahali yanapotengenezwa na lile *brand name*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, *Coca cola* ilitoka Marekani, lakini inatengenezwa sehemu zote duniani siku hizi na kila mahali inaitwa *Coca cola*. Kwa hiyo, niko tayari kwenda kuwahimiza magodoro Dodoma warudi Dodoma. Ahsante. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	207,438,700/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	2,008,134,000/=
Kifungu 2001 - <i>Industry</i>	5,205,775,300/=
Kifungu 3001 - <i>Commerce</i>	3,122,646,500/=
Kifungu 3004 - <i>Trade Practices Bureau Agency</i>	317,549,600/=
Kifungu 3005 - <i>Trade Practices Tribunal</i>	120,000,000=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	100,000,000/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	1,526,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

T A A R I F A

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2005/2006 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila ya mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe makisio ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki. (*Makofî*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara yalipitishwa na Bunge*)

NAIBU SPIKA: Makadirio ya Wizara hii yamepitishwa rasmi na Bunge hili. Hapo ndiyo tumefikia mwisho wa shughuli za leo. Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

(*Saa 12.02 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumanne
Tarehe 12 Julai, 2005 saa tatu asubuhi*)